# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 2 Februari, 2021

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Kwaya ya Bunge Iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

**SPIKA:** Ahsante sana Kwaya yetu ya Bunge. *Excellent. (Makofi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Naomba tukae. Wabunge wapya wabakie hapo nje mpaka tutakapowakaribisha. Wengine tuchukue nafasi zetu haraka.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kikao chetu, naomba kutoa pole kwenu wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Marehemu Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara aliyefariki tarehe 21 Januari, 2021 nchini India alikokwenda kwa ajili ya kupata matibabu na kuzikwa tarehe 26 Januari, 2021 nyumbani kwake Dongobesh, Mkoani Manyara.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima naomba tusimame kwa dakika moja tumwombee ili Mwenyezi Mungu ampumzishe kwa amani.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa muda kwa ajili ya kumwombea Marehemu Mhe. Martha Jachi Umbulla)*

**SPIKA:** Bwana alitoa, Bwana ametwaa. Jina lake lihimidiwe. Amina. Tunaweza kukaa.

Najua muda mrefu mmekuwa hamko pamoja, lakini hiyo isiwe sababu ya kutosikilizana ndugu zangu Waheshimiwa. Sasa mko Bungeni kila mmoja anayepiga *story* aache, anayegeuza kiti, aangalie mbele kwa Spika. Naomba tuwe na utulivu ndani ya ukumbi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuahirisha Mkutano wa Kwanza wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 30(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwa nyakati tofauti tofauti tulifanya shughuli za kuapisha Kiapo cha Uaminifu Wabunge 27 kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

Wabunge 19 Viti Maalum kutoka CHADEMA, Wabunge wanne wa Majimbo kutoka Chama cha *ACT* Wazalendo na Wabunge watano wa kuteuliwa na Rais. Sasa nawakaribisha humu ndani kwa kuanza na Wabunge watano wa kuteuliwa ambao ni Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho na Mheshimiwa Profesa Shukrani E. Manya. Wabunge hawa wa kuteuliwa watano naomba waingine ndani ya Ukumbi wa Bunge sasa. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge wa Kuteuliwa na Rais waliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Pia tuliwaapisha Wabunge wanne kutoka Chama cha *ACT* Wazalendo, nao nitawaomba waingie kama wako hapo nje, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa Salum Mohamed Shaafi. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge kutoka Chama cha ACT Wazalendo waliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana, pia tuliwaapisha Wabunge 19 wa Viti Maalum kutoka CHADEMA ambao naomba niwataje kwanza halafu ndiyo waingie; Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Asya Mohamed, Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mheshimiwa Sophia Hezron Mwakagenda, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mheshimiwa Anatropia Rweikiza Theonest, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza.

Sasa nawaomba waingie ndani ya ukumbi wa Bunge, wachukue nafasi ya viti vyao. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge wa Viti Maalum kutoka CHADEMA waliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Baada ya kuwakaribisha wenzetu hao ambao kwa niaba yenu ningependa kuwapongeza sana kwa kupata fursa ya kuwa Waheshimiwa Wabunge Kikatiba. Sasa tuendelee na shughuli. Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 13 Novemba, 2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Maswali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaanza kuulizana maswali, nafikiri mnaweza mkauona ukumbi wetu kwa wale ambao mna jicho la kuweza kuangalia kumbukumbu mtaona kuna kazi kubwa sana ambayo imefanyika hapa. Huko juu taa karibu zote zilikuwa zimekufa, hata mzingo huo mwingine, lakini pia rangi na sasa hivi hata ukidondosha sindano chini unaiona. Naomba tumpigie makofi Katibu na timu yake kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Sasa kweli huu ni mjengo kweli kweli! Ndiyo maana watu wanapambana kweli kweli kuja mjengoni hapa maana mjengo unapendeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali letu la kwanza kabisa kwa Bunge la Kumi na Mbili amepewa heshima Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kuliuliza.

Mheshimiwa Getere. Sijui yuko upande gani sasa maana mnakaa upya. Ahsante nimekuona.

## MASWALI NA MAJIBU

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba swali langu namba 295 lipate majibu.

**SPIKA:** Naomba urudie, maana hilo swali lako mimi silifahamu. Angalia *Order Paper.*

Na. 1

### Tatizo la Madawati

**MHE. BONIFACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani endelevu za kuondoa tatizo sugu la upungufu wa madawati kwenye baadhi ya shule za msingi na sekondari nchini?

**SPIKA:** Swali lako ni namba moja kabisa, sio 295, hapana, Kwa hiyo kila muuliza swali lazima uwe umeshaangalia swali lako ni namba ngapi ili uweze kuliuliza.

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Mheshimiwa Silinde tafadhali na yeye ni mara ya kwanza anajuka kujibu maswali, kwa hiyo makofi ni muhimu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kabla sijaanza kujibu swali namba moja la Mheshimiwa Mwita Getere, naomba kwa idhini yako nitoe shukrani kwanza kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kushinda uchaguzi, lakini vilevile kuweza kuingia ndani ya Bunge. Pia kwa kipekee kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa ambayo amenionesha kwangu mpaka kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo nahudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nikishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa imani yake kubwa ambayo wameionesha kwangu kwa kunipa nafasi ya kugombea na mwisho wa siku kunisaidia kampeni na kushinda kwa kishindo. Nakishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa niishukuru familia yangu. Mama yangu mzazi kwa kuwa nami katika kipindi chote mpaka kufikia hatua hii ambayo leo nimefikia...

**SPIKA:** Sasa majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika,

sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mwita Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, changamoto ya wanafunzi kukosa madawati katika shule za msingi na sekondari imetokana na mwitikio mkubwa wa wazazi kuandikisha wanafunzi shuleni baada ya Serikali kuanzisha mpango wa utoaji wa elimu bila malipo ambapo idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kwenye shule za msingi na sekondari umeongezeka maradufu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawati ambapo mpaka sasa mwaka 2015 kulikuwa na madawati 3,024,311 na mpaka sasa hivi kufikia mwezi Septemba 2020 Serikali imeongeza madawati kufikia madawati 8,095,207 ambapo kumekuwa na ongezeko la madawati 5,070,899.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu wa madawati, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya utengenezaji wa madawati kwenye miradi yote inayotengewa fedha za ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari na kuhamasisha wananchi na kuwashirikisha wadau na asasi mbalimbali katika utengenezaji wa madawati pamoja na kuendelea kutenga fedha ya matengenezo ya madawati kwenye Halmashauri kupitia mapato ya ndani. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kama unalo swali la nyongeza.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza kwenye Bunge lako hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, suala la madawati limekuwa ni suala sugu sana katika nchi yetu. Swali langu la kwanza, nataka kujua Serikali ina mpango gani sasa wa kuwa na mfuko maalum au mfuko wa kudumu ambao utafanya hili tatizo la madawati liweze kupungua katika nchi yetu na hasa katika Jimbo langu la Bunda, upungufu wa madawati kwenye shule za msingi na sekondari ni mkubwa sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sasa hivi nchi yetu kuna wanafunzi wanaenda shuleni hasa sekondari. Kuna mkanganyiko wa kusema twende na madawati, wengine wananunua wazazi, wengine wanasema Serikali inaleta.

Mheshimiwa Spika, nini tamko la Serikali kwenye suala hili la madawati katika shule za sekondari? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE: DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimjibu Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, maswali yake mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ametoa kama pendekezo la Serikali kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kutatua tatizo la madawati. Jambo hili nafikiri ni jambo jema na sisi kama Serikali tunalipokea. Hata hivyo, pamoja na kupokea wazo ambalo amelileta la kuwa na mfuko maalum, lakini bado naweza kueleza kwamba hili suala la upungufu wa madawati mashuleni Serikali imeendelea kukabiliana nalo, lakini na sisi kama Wabunge tuna wajibu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, moja, kwanza sisi Wabunge ni Madiwani katika Halmashauri zetu. Pia katika halmashauri tunapswa kuwa na mipango ya kutumia fedha za ndani kuhakikisha kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya kutatua tatizo la madawati.

Mheshimiwa Spika, vilevile sisi ni Wenyeviti wa Mifuko ya Jimbo. Kwa hiyo, kama kuna changamoto katika halmashuri yako sehemu ya fedha za Mfuko wa Jimbio unaweza kuzitumia katika kutatua tatizo la madawati. Aidha, unaweza kutafuta wadau mbalimbali ambao wanaweza kusaidia kuhakikisha kwamba tunaondoa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana hoja kwamba watu wengi wamekuwa wakilazimishwa ili mwanafunzi aingie darasani lazima mpaka ulipe mchango wa dawati ama utoe dawati. Msimamo wa Serikali ambao aliutoa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ni kwamba wanafunzi wote wanapaswa kujiunga bila kuwa na masharti, kama hilo linaloletwa la kusema kwamba lazima mtu atoe dawati ndiyo asajiliwe shuleni.

Kwa hiyo, msimamo wa Serikali bado uko palepale na tutaendelea kusimamia huo msimamo wa Serikali kama ambavyo Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameagiza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila baada ya miaka 10 tumekuwa tukifanya sensa ambapo sensa hii pamoja na mambo mengine inaonesha mtawanyo wa umri na kwa hiyo, ni rahisi kufanya maoteo ya watoto wanaoingia shuleni. Kwa kuwa, tatizo hili la mawati limekuwa likitokea kila mwaka inapotokea tunaanza msimu mpya wa masomo, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kutumia takwimu zinazotokana na sensa kujiandaa vizuri kulimaliza tatizo hili badala ya kutokea mwaka hadi mwaka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Mheshimiwa David Silinde, tafahdali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape Nnauye, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimuondoe hofu, Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inatumia takwimu sahihi kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto za madawati na wanafunzi mashuleni. Ndiyo maana nimeeleza katika moja ya mpango wa Serikali ambao sasa hivi upo ni kwamba kila darasa linavyokuwa linajengwa ni lazima liwe na madawati ama kama ni shule lazima iwe na miundombinu yote. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu tu ya kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto ya madawati mashuleni.

Mheshimiwa Spika, lakini pili na kwa kifupi ni kwamba sisi tuna huo mpango na nimhakikishie kabisa kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano, hiyo kero ya madawati mashuleni tunayo na tutaieleza katika mpango wetu wa bajeti wakati utakapofika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, mtaona tumetumia dakika 20 kwa swali moja, sasa tuendelee. Mheshimiwa Rehema Juma Migila, Mbunge wa Ulyankulu.

Na. 2

**Kufungua Shule ya Sekondari Isike**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, ni lini Shule ya Sekondari Isike iliyopo katika Kata ya Igombe itafunguliwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Isike ilijengwa katika makazi ya wakimbizi kwa lengo la kuhudumia wakimbizi na watoto wa jamii inayowazunguka. Mwaka 2012, Serikali ilitoa maelekezo kwa wakimbizi wote waliokuwa wanaishi katika Kambi ya Ulyankulu warejee kwa hiari nchini kwao. Katika kutekeleza agizo hilo, wakimbizi walirejea makwao na wachache waliomba uraia na kuendelea kuishi katika maeneo hayo, hivyo shule ilibaki na wanafunzi wachache sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuwahamisha wanafunzi waliobaki na kuwapeleka katika Shule ya Sekondari Ulyankulu. Kwa kifupi, kufungwa kwa shule hiyo kulitokana na kuzingatia matumizi sahihi ya rasilimali watu, fedha na vifaa pamoja na mazingira salama na bora kwa wanafunzi kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa wanafunzi wa eneo hilo wamepelekwa na kupangwa katika Shule ya Sekondari Ulyankulu. Serikali itafungua Shule ya Sekondari Isike kama itabainika kuna mahitaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Migilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ambayo hayajaniridhisha, naomba niseme kwamba shule ile ilifungwa kwa sababu alizozitaja lakini mpaka dakika hii Shule ya Sekondari Ulyankulu imefurika wanafunzi mpaka wamehamishiwa Shule ya Sekondari Mkindo ambayo sio ya bweni.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwarudisha wale wanafunzi ambao wanatembea umbali mrefu na kuwaongezea wazazi gharama ambazo hazihitajiki?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, shule ile imefungwa sasa hivi haifanyi kazi ya aina yoyote imekuwa ni makazi ya ngedere na nyani, hali ambayo inasababisha wananchi na Serikali waone kwamba walitupa nguvu zao za bure na za rasilimali fedha pasipokuwa na sababu ya maana.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuirudisha tena kwa sababu mahitaji yamekuwa ni makubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, wanafunzi hawapo sasa wamehamia ngedere. Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Waziri wa Nchi, TAMISEMI, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri wangu kwa kujibu vizuri maswali yote yaliyokuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Rehema Migilla kuwa Mbunge wa Ulyankulu, dada yangu hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lake tumelichukua kwa sababu tunafahamu eneo lile lilikuwa la wakimbizi, lakini wewe ndiyo uko *site* kule unaona mahitaji yote ya msingi. Hivi sasa namuagiza Afisa Elimu wetu wa Mkoa wa Tabora aende akafanye tathmini ya haraka atuletee majibu ya haraka ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia watoto wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo siyo shule hiyo pekee, hata ile shule ambayo juzi katika ziara tulipokuwa na Mheshimiwa Rais tumetoa melekezo, shule hizo zifanyiwe harakati za haraka kama ikiwezekana tuzifungue haraka.

Lengo letu kubwa ni Watanzania waweze kupata huduma vizuri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tuendelee na swali la tatu. Kwa sababu ya muda, yale matangazo ya mwanzo yamekulaa muda wetu kidogo. Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga.

Na. 3

**Mradi wa Mwendokasi – Awamu ya Tatu**

**MHE. JERRY W. SILAA** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Mwendokasi awamu ya tatu toka Gongolamboto mpaka Kariakoo ambao umeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam *(DART)* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendeayo haraka maarufu kama mwendokasi unaotekelezwa katika awamu sita katika barabara zote kuu Jijini Dar es Salaam zenye urefu wa kilometa 146.2.

Mheshimiwa Spika, awamu ya tatu ya mradi wa mabasi yaendayo haraka inatekelezwa katika barabara za Nyerere, Bibi Titi, Maktaba, Azikiwe na Uhuru kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongolamboto zenye urefu wa kilometa 23.6 ikiunganishwa na awamu ya kwanza na ya pili ya mradi huu katika vituo vikuu vya mabasi ya Kariakoo, Gerezani na Kivukoni.

Mheshimiwa Spika, kazi inayoendelea sasa ni tathmini ya zabuni zilizowasilishwa ili kumpata mkandarasi atakayeanza kujenga awamu ya kwanza ya mradi, kwa maana ya *Lot 1,* inayohusisha ujenzi wa barabara, kwa maana ya *road works,* vituo vidogo vya mabasi pamoja na kituo kikuu cha mabasi cha Gongolamboto.

Mheshimiwa Spika, zabuni ya kazi ya ujenzi awamu ya pili, inayojumuisha ujenzi wa karakana ya Gongolamboto, Kituo Kikuu cha Mabasi cha Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere pamoja na vituo mlisho vya *Jet Club,* Banana na Mombasa, zabuni yake haijatangazwa kutokana na mabadiliko ya usanifu wa karakana ya Gongolamboto baada ya eneo la karakana hiyo kubadilishwa kutokana na sehemu kubwa ya eneo la awali kuathiriwa na mradi wa reli ya kisasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu katika mapendekezo ya awali ulikuwa ufike kwenye eneo la Pugu na kwa kuwa sasa mji umekua kwa kasi na wote mnafahamu Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani vimeungana, je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kutekeleza mradi huu mpaka eneo la Pugu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutumia historia ama matokeo ya mradi wa awamu ya kwanza kutoka Kimara

mpaka Kariakoo na Posta wakati miundombinu imejengwa na sasa wafanyabiashara ndogo ndogo wanafanya biashara kwenye miundombinu hii mipya, je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuunganisha miundombinu ya mradi huu wa mabasi yaendayo haraka na masoko yatayoingiza wafanyabiashara kwenye maeneo haya ya vituo mlisho vya Banana, Mombasa na Gongolamboto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali haya, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali ndugu yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mawazo ni mazuri na tukifahamu kwamba Jiji la Dar es Salaam linazidi kutanuka, lakini *design* ya kwanza ilikuwa inatuelekeza tunaishia mahali fulani. Si hivyo tu, tulifikiria hata sehemu ya barabara inayoenda Mbagala, sasa hivi inaishia pale Mbagala Rangi Tatu, tulikuwa tunafikiria jinsi gani tutafanya tufike mpaka pale mbele ya Kongowe.

Kwa hiyo, haya yote ni mawazo mazuri, wataalam wetu wataendelea kuyafanyia kazi, lakini tuna *phase one* ya *design,* kama tutakuwa na *variation* yoyote tunaweza tukaifanya katikati ya kazi yetu lakini lengo letu ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma vizuri, hasa hii ya mwendokasi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili la kuhakikisha haya mabasi yanapita katika vituo vya kutoa huduma; ni kweli na hata ukiangalia katika ujenzi wa soko letu la Kisutu pale Dar es Salaam, Ilala moja ya jambo kubwa ni kutengeneza daraja linalounganisha mwendokasi na kutengeneza soko. Wataalam wetu wa *TANROADS* na wale ambao wanafanya ujenzi walikuwa wanaendelea na kazi hiyo. Kwa hiyo, hilo jambo ni kipaumbele chetu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, hata kuwa na *pack* maalum kwamba mtu akiondoka sehemu fulani anaweza akaacha gari lake na kuweza kusafiri. Hayo yote ni mambo ambayo tunayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika awamu hii tutaenda kufanya maboresho makubwa kwa lengo kubwa miundombionu hii na usafiri wetu huu unakuwa safi na salama kwa wasafiri wote wa Jiji la Dar es Salaam.

**SPIKA:** Ahsante, tunahamia Wizara ya wananchi ya Kilimo. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, kwa niaba yake Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, nilikuona.

Na. 4

**Kupeleka Pembejeo kwa Wakati**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MHE. AIDA J. KHENANI)** Aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapelekea wakulima pembejeo kwa wakati?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kurudi tena ndani ya Bunge. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali huratibu mahitaji, upatikanaji, usambazaji, matumizi na kuhakiki wa ubora wa

pembejeo za kilimo ili ziweze kufikishwa kwa wakulima kwa wakati zikiwa na ubora stahiki. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati. Mikakati hiyo, ni pamoja na kupata mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo kutoka kila Mkoa kabla ya msimu wa kilimo kuanza, kuwasiliana na makampuni ya pembejeo na kuyahimiza kusambaza pembejeo hizo mapema kulingana na mahitaji ya kila Mkoa kabla ya msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, wakulima kupitia Vyama vyao vya Ushirika wanahimizwa kuainisha na kuwasilisha mahitaji ya pembejeo mapema kwa Mamlaka ya Mbolea Tanzania *(TFRA)* ili waweze kununua mbolea wanazohitaji kwa wakati kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja ambao katika mwaka 2020, wakulima wa Mikoa kama Iringa, Mbeya waliingiza mbolea moja kwa moja kutoka kiwandani katika nchi za Morocco na China. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya uzalishaji na uagizaji na uthibiti wa mbegu bora na viuatilifu nchini ikiwemo kuhamasisha uzalishaji wa pembejeo hizo ndani ya nchi ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa pembejeo kujenga maghala makubwa kwa ajili ya kuhifadhi pembejeo hususan katika maeneo yenye mahitaji makubwa ili kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo kwa wakati wote. Utekelezaji wa mpango huu ulianza mwaka 2019 ambapo Wadau wa Maendeleo wakiwemo *African Fertilizer and Agribusiness Partnership* waliwezesha ujenzi wa jumla ya maghala 12 mwaka 2019 yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani za mbolea 50,000 katika Mikoa ya Kilimanjaro, Morogoro, Arusha, Iringa, Rukwa, Njombe na Songwe. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha pembejeo nchini ili kuongeza upatikanaji wake kwa wakati na bei nafuu kwa wakulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia, nimekuona.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali, kuna shida kubwa sana kwa waletaji wa pembejeo kwenye majimbo yetu. Jimbo la Rungwe linalima sana mazao ya viazi, lakini kumekuwa na ucheleweshwaji wa pembejeo. Tunaomba kujua Serikali inafanya mbinu gani ya kuhakikisha wanaoagiza pembejeo wanaleta pembejeo kwa wakati kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wawekezaji na hasa hao wabia ambao mnawapa kazi hiyo ya kusambaza pembejeo wanaleta pembejeo nyingine hazina viwango na hivyo kusababisha kupata mazao hafifu kwa kuwa pembejeo iliyoletwa si sahihi kwa wakulima wetu. Je, ni hatua gani itachukuliwa kuhusiana na suala hili? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza utaratibu wa kuagiza pambejeo tunatumia mfumo wa *bulk procurement.* Utaratibu huu *tender* hutangazwa ambapo waagizaji wote wa mbolea wanakuwa wamesajiliwa na wanashindanishwa na kupewa *time limit* ya uagizaji na ku-*deliver* katika kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, mfano kwa mwaka huu mahitaji yetu ya mbolea kwa nchi nzima ni jumla ya tani 700,000 na ambazo zinatakiwa ziwe *delivered* kuanzia mwezi wa 11 na jambo hilo limeendelea na mpaka sasa hatujapata tukio lolote la ukosefu wa pambejeo katika mikoa yetu. Kwa hiyo, kama kuna *case* inahusu maeneo ya Rungwe, nitamuomba Mheshimiwa Mbunge anipe hiyo *specific case* li tuweze kuifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubora, Wizara ya Kilimo kupitia mamlaka yetu iliyokuwa ikiitwa *TPRI* ama kwa sasa inajulikana kwa mujibu wa sheria tuliyopitisha katika

Bunge lililopita *TAFA,* tunafanya ukaguzi katika maduka yote yanayouza pembejeo. Pale ambapo tutakutana na pembejeo *fake* tunachukua hatua za kuwapeleka Mahakamani. Mpaka sasa kuna zaidi ya kesi tano za wasambazaji ambao walikutwa wana pembejeo *fake.*

Mheshimiwa Spika, ili kulitatua tatizo hili sasa hivi kwa sababu biashara ya pembejeo inafanyika katika wilaya, Wizara ya Kilimo sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za kuanzisha kitu tunaita *Customer Service Centre* ambapo mkulima popote alipo katika nchi hii ataweza kupiga simu bure pale ambapo aidha kakutana na pembejeo *fake* ama kapata tatizo lolote la kiuatilifu ama tatizo la ugonjwa katika eneo lake na sisi kuweza kumhudumia kwa wakati. Tunachukua hatua hii ili kupunguza tatizo la *gap* ya muda kati ya athari inapotokea mpaka pale huduma inapoenda kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachosisitiza unapoenda kununua pembejeo popote hakikisha umepata risiti ya muuzaji ya *EFD* ili tutakapokuta kuna tatizo tuweze kumchulia hatua. Hili la Rungwe, kama kuna *special case,* karibu.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, litaulizwa na Mheshimiwa Saashisha, hili jina gumu sana, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ulizwa swali lako Mheshimiwa.

Na. 5

**Mashamba Yaliyochukuliwa na Vyama Vya Ushirika – Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Mashamba yaliyochukuliwa na Vyama vya Ushirika Wilaya ya Hai yameshindwa kuendelezwa huku Wananchi hawana mashamba ya kulima:-

Je, kwa nini Serikali isiyarudishe mashamba hayo kwa Wananchi?

**SPIKA:** Waheshimiwa huyo ndio Mbunge wa Hai. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kumjibu Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hai ina jumla ya mashamba 17 yanayomilikiwa kihalali na Vyama vya Ushirika. Mashamba hayo yana jumla ya ekari 10,139.5 kati ya hizo ekari 7,769 zimekodishwa kwa wawekezaji na ekari 580 zimepewa taasisi mbalimbali ili kuweza kuongeza mapato katika Vyama vya Ushirika husika na jumla ya ekari 1,789 zinatumika na wanachama wa Vyama vya Ushirika kwa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama kunatokea kusuasua kwa matumizi ya mali za Vyama vya Ushirika ikiwemo mashamba, ni jukumu la Serikali kusaidia Vyama hivyo kuendeleza mali hizo. Mathalani, Aprili, 2020, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilituma Timu ya Wataalam Wilayani Hai kufanya tathmini ya mashamba yote yanayomilikiwa na Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na uwekezaji unaofanyika na kutoa ushauri kwa vyama hivyo kuhusu uwekezaji husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini iliyofanyika, mwezi Julai 2020, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilitoa Mwongozo kwa Vyama vya Ushirika vinavyomiliki mashamba kuyaendeleza na kufanya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo ili kuwanufaisha wanachama na kwa sasa mashamba yote yanatumika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaendelea kufanya urasimishaji wa mali zote ikiwa ni pamoja na mashamba yanayomilikiwa na Vyama vya Ushirika na kuweka mikakati endelevu ili mali hizo ziweze kutumika kwa manufaa ya wanachama wa ushirika na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuchukua mashamba yanayomilikiwa na Vyama vya Ushirika, bali itaendelea kusimamia na kushauri vyama kuendeleza mashamba hayo kwa kutekeleza mipango ya uwekezaji itakayonufaisha Wanachama wa Vyama vya Ushirika. Aidha, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wanachama au viongozi wa Vyama vya Ushirika watakaobainika kutumia mashamba hayo kwa maslahi binafsi.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru japo sijaridhishwa hata kidogo na majibu ya Serikali kwa sababu malalamiko ya wananchi kwenye vyama hivi ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali la kwanza la nyongeza; kwa kuwa kumekuwa na malalamiko makubwa ya ubadhirifu wa Vyama hivi vya Ushirika, Bodi hizi kuwa wababe, kutoshirikisha wananchi, lakini pia mashamba haya kukodishwa pasipo tija kwa wananchi. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa wa kuunda Tume Maalum itakayoshirikisha vyombo vyote vya dola kwenda kufanya uhakiki wa mashamba haya yote 17?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa tunaona Sheria ya Ushirika ya mwaka 2013 haitoi fursa kwa viongozi wa ngazi ya mkoa kushuka chini kuweza kuona kinachoendelea kwenye vyama hivi vya ushirika. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kufanya mabadiliko ya sheria, ili sasa viongozi wa ngazi ya mkoa waweze kushiriki na kuona nini kinaendelea kwenye vyama hivi vya ushirika?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhali, Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna changamoto za baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Ushirika kuhusishwa na ubadhirifu na Serikali imekuwa ikichukua hatua mara kwa mara. Tumeona hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali katika Vyama vya Ushirika vya Tumbaku, tumeona hatua ambazo Serikali imechukua katika Vyama vya Ushirika vya Pamba, tumeona hatua ambayo Serikali imechukua katika Vyama vya Ushirika vya Mkonge.Hatua hizi zote zimechukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba kwanza mali zilizoibiwa za vyama vya ushirika zinarudishwa kwa wanachama, lakini mbili kuwachukulia hatua viongozi wote waliohusika na kuwapeleka katika vyombo vya sheria.

Suala ambalo analisema la uwepo wa Tume, ipo Timu Maalum chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inafanyakazi hii na imekuwa ikiendelea kufanyakazi hii katika maeneo yote yanayohusu vyama vya ushirika na kama kuna specific case inayohusu Wilaya ya Hai namkaribisha Mheshimiwa Mbunge aje atueleze Wizarani na tutashirikiana naye kuhakikisha kwamba ubadhirifu kama upo katika maeneo ya Hai ya Vyama vya Ushirika vya Wilaya ya Hai, au Mkoa wa Kilimanjaro tutaweza kuchukua hatua kama ambavyo tumechukua hatua katika masuala yanayohusu mali za *KNCU*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya sheria kwanza ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tukaelewa dhana ya ushirika ni dhana ya hiyari. Ushirika siyo mali ya Serikali ni mali ya washirika, lakini Serikali inaingilia kwenye masuala ya ushirika kwasababu ya *public interest* kwasababu ile inakuwa ni mali ya umma ndiyo maana tunayo Tume ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upungufu wa kisheria Wizara ya Kilimo sasa hivi inaipitia sheria na mwaka jana ilikuwa tuilete ndani ya Bunge ili kuweza kuihuisha iweze kuendana na mahitaji ya sasa, badala ya kuwa ushirika wa huduma uwe ushirika wa kibiashara kwa maslahi ya wanaushirika. Kwahiyo suala la kisheria tunaliangalia na ni suala *genuine* ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema na muda ukifika tutaileta sheria ndani ya Bunge ili iweze kwenda

na wakati, lakini siyo kuifanya Serikali i-*control* ushirika bali tunatengeneza sheria kuufanya ushirika ujiendeshe wenyewe kwa maslahi ya washirika na kutengeneza *governing bodies* ambazo zitausimamia ushirika kwa maslahi ya wanaushirika.

**SPIKA:** ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mpaka sasa kwa kweli nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote,*so far* uandishi wa maswali unazingatia kanuni yetu, yaani ukiyatazama toka tulivyoanza maswali ni *brief* na yanajielekeza moja kwa moja kwenye kitu ambacho Mheshimiwa Mbunge anauliza. Kwahiyo nakupongezeni sana na ningependa kuwatia moyo tunavyoendelea maswali yenu mnayotunga yawe hivyo, siyo unaandika swali nusu ukurasa, ukurasa mzima, inakuwa haieleweki mtu anataka kuuliza kitu gani. Kwa kweli maswali ya leo ni mazuri sana.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Zacharia Paul Issay, Mbunge wa Mbulu Mjini, uliza swali lako.

Na. 6

**Ujenzi wa Barabara ya Mbulu – Haydom**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa lami barabara yenye urefu wa Kilometa 50 toka Mbulu kwenda Haydom ambayo ipo kwenye mpango wa Bajeti tangu 2019/2020, 2020/2021?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe, ni Mbunge wa Ileje huyu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)**alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kujibu swali na ni mara yangu ya kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa

Mbunge. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, pia nikishukuru sana chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuniteua na hatimaye kunipitisha kuwa mgombea wa Jimbo la Ileje, lakini niwashukuru sana....

**SPIKA:** Sasa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba nijibu swali laMheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika,Barabara ya Mbulu - Haydom yenye urefu wa kilometa 70.5 ni sehemu ya barabara yaKaratu – Mbulu – Haydom– Sibiti – Lalago – Maswayenye urefu wa kilomita 398 inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali (*Preliminary Design*) wa barabara hii (kupitia mradi wa *Serengeti Southern Bypass*) ili kuijenga kwa kiwango cha lami umekamilika. Kazi hii ilifanywa na Kampuni iitwayo *H.P. Gauff Ingenieure GmbH & Co. KG – JBG* mwaka 2016 kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa wananchi wa Mbulu pamoja na Hospitali ya Haydom, Serikali ilianza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi kwa sehemu ya Mbulu – Haydom yenye urefu wa kilomita 50 kwa kiwango cha lami, ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020, ilitenga Shilingi milioni 1,450.00 na mwaka wa fedha 2020/2021, imetenga Shilingi milioni 5,000.00. Ujenzi wa barabara hii utatekelezwa kwa njia ya Kusanifu na Kujenga (*Design and Build*) na zabuni ya kazi hii itatangazwa wakati wowote katika mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, zimetengwa shilingi milioni 401 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issaay kama kuna swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Swali langu, barabara hii iliyojibiwa na Serikali muda huu ina miaka miwili kwenye bajeti ya Serikali na barabara hii tumeiombea kura kwa maeneo yote ya Majimbo matano ambamo barabara hii inapita.

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko yangu kwa majibu ya Wizara kwa kuwa tumebakiza miezi minne ya bajeti ya mwaka huu wa fedha unaoisha. Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kuombea barabara hii kura kutoka Karatu, Mbulu Mji, Mbulu Vijijini mpaka Maswa inawapa changamoto na imani ndogo wananchi wanaotuchagua na kutufikisha hapa tulipo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika barabara hii ninayoizungumza sisi Mbulu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi na viongozi wengine wakuu, walipokuja kwenye kuomba kura walitegemea sana kauli ya Serikali juu ya utekelezaji wa barabara hii kuanzia Jimbo la Karatu, Jimbo la Mbulu Mji na Jimbo la Mbulu Vijijini hadi huko Maswa. Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa kujibu kiu na imani ya wananchi wa Majimbo yote matano kwa barabara hii ambayo ni muhimu iliyoko juu ya bonde la ufa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kujibu swali la nyongeza, lakini nimshukuru Mungu sana na

nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani kunipa nafasi ya kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimjibu ndugu yangu wa Mbulu kwamba anafahamu na wananchi wa Mbulu na Manyara kwa ujumla wanafahamu juhudi za Serikali kuweza kuwakwamua wananchi kwa kujenga na kuimarisha barabara za maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba katika juhudi za kuwasaidia wananchi wa Mbulu tumejenga daraja la maghala kwa gharama kubwa na wananchi sasa wanapita.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hivyo tu tumejenga daraja la Sibiti kwa nia ya kuwanusuru wananchi katika maeneo hayo, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wanafahamu na wanaona na maboresho ya barabara katika barabara hizi ukitoka Karatu kuja Mbulu kupita Kilimapunda barabara zimeimarishwa ili kuwasaidia wananchi katika uzalishaji kwa ajili ya utalii, kwaajili ya kilimo na nataka kusema hivyo kwa ajili ya vipaumbele na upatikanaji wa fedha Serikali inafanya juhudi kubwa kuwasaidia wananchi wa Mbulu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge hata hizo kilomita 50 ambazo zimewekewa mpango kazi wa kujengwa, kilomita 50 ilikuwa ni kipaumbele kwa kuwasaidia wananchi ambao kuna sehemu kubwa wanazalisha mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika,kwahiyo Mheshimiwa Mbunge na wananchi niwatoe tu hofu, mpango ambao upo, majibu mazuri ya Naibu Waziri aliyoyajibu hapa ikitekelezwa kwa kweli wananchi tunaenda kuwasaidia sana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nawaona Wabunge wa Majimbo yote matano mmesimama, lakini sehemu kubwa ya hii barabara hasa kule Kilimapunda iko kwa Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali hili muhimu sana la nyongeza. Kwa kuwa amesema katika majibu yake ya msingi kwamba ametenga milioni 401 na ni wazi haiwezi kujenga barabara na Rais ameahidi mara mbili kwenye vipindi vyake viwili, je, haoni sasa aje na mpango mzuri wa kujenga barabara hii kwa kuitengea fedha?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalize tu mwenyewe kwa vile nimeanza. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na anafahamu na niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kama walivyosimama, nilipokuwa Naibu Waziriwa Ujenzi nilitembelea sana maeneo haya kwa sababu ya upendo mkubwa sana wa Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kwa shida ambazo niliziona katika maeneo haya. Jiografia ya maeneo haya siyo nzuri Mheshimiwa Spika ndiyo maana kama nilivyosema awali kwamba Serikali imetenga fedha kuweza kuwakwamua wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu hata ile barabara kuja Babati imeendelea kutengenezwa naamekuwa na mradi wa kilomita mbili za lami pale kwake ni kwasababu Serikali ina upendo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais sana kwasababu katika juhudi za kutengeneza barabara za nchi hii tumeshuhudia kipindi kilichopita madeni ya wazabuni kiasi kikubwa sana yamelipwa na hii inaashiria kwamba tutaenda kutengeneza barabara kwa kasi kubwa zaidi, ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwasababu ya muda Waheshimiwa nawaona, lakini tuendelee na swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Amar safari hii anakaa upande gani? Aah pale pale afadhali tuendelee Mheshimiwa.

Na. 7

**Ujenzi wa Barabara ya Kahama – Busisi**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza: -

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Barabara ya kutoka Kahama - Nyang'holongo – Kharumwa – Nyijundu – Busolwa - Ngoma hadi Busisi Sengerema kwa kiwango cha lami itatekelezwa?

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika,Barabara ya Kahama - Nyang'holongo - Kharumwa - Nyijundu - Busolwa - Ngoma hadi Busisi Wilayani Sengerema (yenye urefu wa kilometa 162.99), inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS).* Barabara hii inaunganisha mikoa mitatu ya Shinyanga, Geita na Mwanza kupitia Wilaya za Msalala (Shinyanga), Nyang'hwale (Geita) na Sengerema (Mwanza).

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii, hivyo inatafuta fedha za kufanya usanifu, ikiwa ni maandalizi ya kuijenga barabara hiyo, kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya shilingi milioni 581.827 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Aidha, Wizara kupitia *TANROADS* inaendelea kufanya matengenezo mbalimbali ya barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Ahadi hii ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami imeahidiwa kwa awamu mbili za Marais wetu, akiwemo Rais Jakaya Mrisho Kikwete, mwaka 2010 alikuja Jimboni kwenye kampeni na akaahidi barabara hiyo kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Pia Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli naye alikuja 2015 naye aliahidi hivyo hivyo ujenzi wa barabara hyo kwa kiwango cha lami.

Swali ni lini fedha hizi zitapatikana kwasababu sasa hivi ni miaka 10 tunaahidiwa utafutaji wa hizo fedha, ni lini fedha hizo zitapatikana kwa ajili ya upembuzi yakinifu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili,kwa kuwa barabara hiyo inafungua mikoa mitatu na sasa hivi Wilaya ya Nyang'hwale inakimbia kiuchumi, barabara hayo yanaharibika na vumbi jingi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale, hususan pale Karumwa wananchi wanapata adha kubwa kwa vumbi kwasababu magari ni mengi.Je, ni lini Serikali itakomesha vumbi hilo na kuweza kuwanusuru wananchi wa Jimbo hilo na kuweza kuwanusuru wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale hususan Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale Karumwa kupata maradhi mbalimbali yakiwemo *TB*?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mafupi, swali la kwanza ni lini?Kuwasaidia watu wa Karumwa huko.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nassor Mbunge wa Nyang'hwale. Ni kweli barabara hii imeahidiwa na Mheshimiwa kama alivyosema Mheshimiwa wa Awamu ya Nne na Mheshimiwa wa Awamu ya Tano, lakini ni azma ya Serikali na ndiyo mpango wa Serikali kwamba katika Awamu hii ya Tano, kipindi cha pili, barabara zote zinazounganisha mikoa na wilaya lazima zitajengwa kwa kiwango cha lami. Kwahiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaamini katika kipindi hiki Serikali itapata fedha na

barabara hii itajengwa. Barabara hii pia hata ukienda kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ipo imeahidiwa,kwahiyo ninahakika Serikali itatekeleza.Kwa maana hiyo tutakapokuwa tumejenga kwa kiwango cha lami maana yake hata lile vumbi linaloonekana Karumwa litakuwa limeondoka ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa miradi ya barabara limekuwa tatizo sugu, ninapozungumza ujenzi wa barabara wa kutoka Kisolya, Bunda, Nyamswa, ahadi na uanzaji umechukua takribani miaka 15. Sasa nataka kujua ni lini barabara hiyo itakamilika kwasababu ikishakamilika kuanzia Kisolya inakuja Bunda Mjini kwenda Nyamswa inaunganika na barabara ya Serengeti na ni kilio cha muda mrefu cha Wilaya ya Bunda na wananchi wa Mkoa wa Mara, lini itakamilika baada ya ahadi na uanzaji takriban imechukua miaka 15? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, tafadhali Elias Kwandikwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, bado nanukia nukia ujenzi. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tujifunze tu kushukuru kwa sababu najaribu kuangalia miradi ambayo inaendelea sasa hivi kwenye Mkoa wa Mara, Mheshimiwa Ester dada yangu anacheka pale, kuna miradi kemkem.

Mheshimiwa Spika, labda nimkumbushe tu Mheshimiwa, kweli barabara ya Bulamba-Kisorya, ilichelewa lakini imekamilishwa. Kuna mradi wa kutoka Kisorya kwenda Nyamuswa tayari mkandarasi ameshapatika, barabara

inajengwa. Iko barabara ya kutoka Makutano – Nata - Sanzate imejengwa na kuna mradi kutoka Sanzate kwenda kule Serengeti na harakati za kujenga barabara kwenda kule Arusha zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Bulaya nimkaribishe tu Bungeni na anafahamu kwamba Serikali inafanya kazi kubwa sana katika Mkoa wa Mara. Kimsingi niseme Mheshimiwa Rais ameyapendelea sana maeneo hayo na kuyapa kipaumbele ili wananchi wa Mara waweze kupata barabara nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ningeanza kutaja miradi iliyoko Mara nadhani Mheshimiwa Ester anafahamu, nafikiri niishie tu hapo. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa jibu la uhakika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuhamie Wizara ya Nishati, nawaona lakini muda kama mnavyoona hauko upande wetu, swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini.

Na. 8

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Umeme Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi wa Kibaha Mjini ambao maeneo yao yalitwaliwa kwa ajili ya mradi wa umeme wa Msongo wa KV 400 kutoka Kinyerezi hadi Arusha?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Nishati, wananchi wa Kibaha Mjini wanataka fidia. Anayesimama ni Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini, Naibu Waziri Nishati. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa makofi hayo yanaashiria nyota njema.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, basi nichukue nafasi fupi kuwashukuru wanachama wa Chama cha Mapinduzi lakini nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi, niwashukuru wana Jimbo la Bukoba Mjini na nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi hii ya kutekeleza kipande hiki cha majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvetry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya uthamini wa mali za wananchi katika mradi wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kilovoti 400 kutoka Kinyerezi kupitia Kisarawe, Kibaha hadi Chalinze ilifanyika kati ya mwaka 2015 na 2016 ili kuwezesha pamoja na mambo mengine wananchi wanaopitiwa na mradi kulipwa fidia na kupisha ujenzi wa mradi huo. Taratibu zote za uandaaji wa taarifa na majedwali ya fidia zilikamilika mwezi Machi 2020. Fidia kwa ajili ya maeneo kati ya Kiluvya (Kisarawe) hadi Chalinze ni takriban shilingi bilioni 21.569.

Mheshimiwa Spika, aidha, malipo haya yanahusisha Halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Chalinze. Kwa sasa taratibu za kuhamisha fedha za fidia kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda *TANESCO* ili kuwalipa fidia wananchi hao zinaendelea. Fidia ya wananchi hao italipwa mara tu baada ya taratibu hizo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Wilaya za Ilala, Ubungo, Kisarawe, Kibaha na maeneo ya Chalinze waliopisha mradi huo kuwa na subira wakati Serikali inakamilisha taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri na wananchi wa Kibaha Mjini wanaunga mkono jitihada za Serikali za maendeleo hususan katika sekta ya umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kama unavyoona ni takribani miaka sita sasa na leo ni mara ya nne nauliza swali hili hapa Bungeni. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri atoe kauli thabiti kwamba malipo haya kwa wananchi wa Mnalugali, Boko, Sofu, Zegereni watalipwa lini fidia hii ili sasa na wenyewe waweze kushiriki na kufurahia miradi hii mikubwa ya umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, miradi ya umeme katika Mji wa Kibaha na hususan *peri-urban* na *densification* imekuwa ikisuasua na haijakamilika. Miradi hii imepita pembezoni mwa wananchi wengi na wanalalamika kwamba hawakuweza kufikiwa na miradi hii. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha sasa miradi hii inakamilika na wananchi wanapata umeme ili kufaidi maendeleo na matunda ya nchi yao?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Waziri mwenyewe wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi la Mheshimiwa Koka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli usanifu wa mradi huo ulianza miaka mingi toka miaka mwaka 2015 na 2016 lakini baadaye tulipoanza kutekeleza mradi mkubwa wa Julius Nyerere mwaka 2018, tulifanya usanifu upya ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakuwa ni mpana na endelevu. Mradi huu ambao unahusisha fidia ya wananchi wa Kibaha utahusisha pia fidia ya wananchi wa kutoka

Kinyerezi, Kiluvya, Chalinze, Kibaha mpaka kufika Dodoma na unaelekea mpaka Singida.

Mheshimiwa Spika, taratibu kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, tumeanza kufanya matayarisho ya malipo na sasa tumetenga shilingi bilioni 21.56 kwa ajili ya kuwalipa wananchi wote. Wananchi wa Kibaha peke yake ambao wanafika 432 wenye jumla ya shilingi milioni 932 malipo yao yameshaanza kutayarishwa. Malipo hayo yanakwenda sambamba na ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme kutoka mradi mkuu wa Julius Nyerere utakaofua *megawatt* 2,115 kutoka Rufiji-Chalinze, Chalinze-Dar es Salaam (kilometa 115) na pia Chalinze-Dodoma, ambapo tumetenga jumla ya shilingi milioni 32.82. Kwa kuwa ujenzi wa mradi wa huu utaanza kabla ya mwezi Juni, ni matumaini yetu na kwa maandalizi mazuri ya watu wa Wizara ya Fedha tutaanza kuwalipa wananchi kabla ya mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na suala la *peri- urban* na *densification*, tumeanza programu ya kupeleka umeme kwenye maeneo yote ya ujazilizi. Maeneo ya kutoka Dar es Salaam mpaka hapa Dodoma takriban vitongoji 12,822, utekelezaji umeanza katika maeneo Dar es Salaam hadi Kibaha kwa vitongoji 272 ambapo vitongoji vya Mheshimiwa Koka vimo. Pia tunapeleka umeme kwenye *peri-urban* anayoizungumza Mheshimiwa Koka kwa maeneo yanayofanana na vijiji ya Kibaha ambayo siyo vijiji kwa kwa gharama ya shilingi 27,000 na utekelezaji umebaki mitaa 12 kati ya mitaa 128. Mradi huu unakamilika mwezi Mei, mwaka huu.

Napenda kumwambia Mheshimiwa Koka awape taarifa wananchi wa Kibaha kwamba *peri-urban* na *densification* katika eneo lao inakamilika mwezi Mei, mwaka huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, swali la nyongeza, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara, naomba kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana na changamoto iliyopo Ngara, wananchi wa Jimbo la Ngara ambao laini ya umeme kutoka Rusumo kwenda Burundi imepita hawajalipwa fidia mpaka leo. Je, ni lini Serikali italipa wananchi hao fidia ambao wamekuwa wakisubiria kwa muda mrefu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatekeleza mradi wa kutoka Rusumo hadi Nyakanazi na Nyakanazi hadi Kigoma na takribani vijiji 39 vitapitiwa na mradi huu. Tathmini imeshakamilika, malipo yameshakuwa *verified* na tunatarajia kabla ya mwezi Machi kuisha tunaanza kulipa fidia wananchi wa Ngara ambao wanafikia 212 kwenye vijiji 12 vya Ngara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awape taarifa wananchi wa Ngara na mimi baada ya Bunge hili tutakwenda kukaa na Mkuu wetu wa Wilaya ili kupitia malipo wananchi waanze kulipwa mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata, bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Nishati, litaulizwa na Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Na. 9

**Ujenzi wa *Sub-station* ya KVA 220 Nyakanazi**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa kujenga *Sub-station* ya Nyakanazi (KV 220) toka Rusumo na Geita utakamilika ili kuondoa tatizo la kukatikakatika kwa umeme Biharamulo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Byabato Lujwahuka.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* linatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 kutoka Geita - Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 144 ambapo Mkandarasi Kampuni ya M/S *Kalpataru Power Transmission Ltd* kutoka nchini India anaendelea na kazi za mradi. Hadi sasa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na kituo cha kupoza umeme umefikia asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, gharama ya mradi ni EURO milioni 45 sawa na takriban shilingi bilioni 117.79. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Machi, 2021. Ni mategemeo ya Serikali kuwa mradi utakapokamilika utaimarisha na kuboresha hali ya upatikanaji umeme katika maeneo ya Wilaya ya Biharamuro na maeneo mengine ya jirani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa sababu amenihakikishia kwamba mradi unakamilika Machi mwaka huu, napenda sasa kupata kauli ya Serikali kwa sababu bado tuna vijiji takribani 25 pale Biharamulo ambavyo havina umeme, kwa hiyo, labda ningehakikishiwa na Serikali sasa

kwamba wakazi wa Biharamulo wajipange kwa ajili ya kusambaziwa umeme kwa sababu jibu ilikuwa tuko *low voltage* ndio maana hatukusambaziwa umeme katika vijiji vingine. Kwa hiyo, labda nipate kauli ya Serikali kutuhakikishia kwamba vijiji vilivyobaki baada ya kukamilika mradi huu vitaweza kupata umeme pia? Ahsante sana.

**SPIKA:** Uhakika huo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, uniwie radhi sana ili niweze kusimama kwa ajili ya kuongeza majibu na nimesimama kwa sababu hivi karibuni nilitembelea Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, Biharamulo wana vijiji takribani 79 na bado vijiji 27. Hivi karibuni pamoja na Mheshimiwa Mbunge nilitembelea vijiji hivyo, tumeshakamilisha matayarisho yote na si kwa Biharamulo peke yake.

Napenda nitoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba vijiji vyote ambavyo havijapata umeme 2,159 kati ya vijiji 12,268 tunaanza kuvipelekea umeme kuanzia tarehe 15 mwezi huu ndani ya miezi 18, nimeona nianze na taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Biharamulo umeme ambao tunajenga ambao kwenye jibu la msingi umeelezwa wa kutoka Geita-Nyakanazi, Nyakanazi-Rusumo na Nyakanazi-Kigoma ni mwarobani kwa kuwapatia umeme wananchi wa Biharamulo na Mkoa wa Kagera na mikoa ya Geita pamoja na Kigoma. Mradi wenyewe peke yake kabla ya kupeleka umeme kwenye mpango wa *REA* utapeleka vijiji 32 na katika vijiji 32 vijiji saba ni vya Biharamulo, ikiwemo Nyakafundwa, Kalenge, Kasonta pamoja na Nyanyantakala, Mavota mpaka Nakahanyia vyote vitapelekewa umeme.

**SPIKA:** Jamani nafikiri Mheshimiwa Waziri anastahili makofi. Nasema hivyo maana anavijua vijiji vyenu kuliko nyie Waheshimiwa Wabunge, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chiwelesa alishauliza swali nyongeza tuhamie Wizara ya Afya Waheshimiwa ni kwa sababu ya muda tu. Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini. Sijui anakaa upande gani sasa hivi, itachukua muda mpaka kujua nani anakaa wapi.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa namba 19, lakini hata hivyo nashukuru, basi naomba swali naomba lijibiwe kama lilivyoulizwa.

**SPIKA:** Swali lako ni Na.10 sijui hii *confusion* imetoka wapi.

Na. 10

**Kutotoza Malipo Huduma za Uzazi wa Mpango**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa bila malipo huduma za uzazi wa mpango na za afya kwa Wajawazito na Watoto chini ya umri wa miaka mitano kama Sera ya Afya inavyoelekeza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Wizara ya Afya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Godwin Aloyce Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama hapa mbele, nitumie fursa hii kumshukuru Mungu, kushukuru Chama changu, kumshukuru Rais wetu kwa kutupa nafasi hii. Pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Siha kwa kuendelea kuniamini lakini nimshukuru mke wangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sera ya Afya ya mwaka 2007, ukurasa wa 19, kifungu 5.3.4 ambacho kinahusu Afya ya mama na mtoto na Tamko la Sera Kipengele (c) Sehemu ya (i), inaelekeza huduma bila malipo kwa Huduma za Afya ya Uzazi na Watoto chini ya miaka mitano. Baadhi ya maeneo wamekuwa wakifanya kinyume na tamko la kisera na hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa pale wananchi wanapotoa taarifa. Katika kipindi cha mwaka 2015-2020, Serikali ilitoa huduma kwa wenye uhitaji bila malipo likiwemo kundi hili zenye thamani ya bilioni 880.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Wizara inawaagiza Waganga Wakuu na Mikoa na Wilaya ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa utekelezaji wa sera na miongozo ya afya katika ngazi ya mkoa na halmashauri kutimiza kikamilifu majukumu yao kwa kushughulikia haraka kero na malalamiko ya wananchi pia utekelezaji wa suala hili ambalo siyo tu ni tamko la kisera lakini pia ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndicho chama kilichounda Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu, nilikuona.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza naomba niulize, je, Wizara hawaoni kwamba sababu mojawapo inayoweza kusababisha malalamiko au kutotekelezeka kwa sera hii ni ile hali ya kuzi-*upgrade* hii vituo vyetu vya afya na zahanati zetu? Kwa mfano katika Manispaa ya Iringa, hospitali yetu ya Frelimo ilipandishwa hadhi kuwa hospitali ya Manispaa tangu mwaka 2013 lakini mpaka sasa inapokea mgao kama kituo cha afya. Katika hospitali ile tuna takribani akina mama 300 mpaka 350 wanaojifungua pale kila mwezi. Unaweza ukaona hiyo inachangia kwa sababu mahitaji ya watu wanaokuja pale yanakuwa makubwa kuliko mgao wanaoupata.

**SPIKA:** Yaani Mheshimiwa Hospitali ya Frelimo pale kila siku kumi wanajifungua?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Endelea na swali lako Mheshimiwa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu hospitali yetu ya Frelimo, kwanza tulikuwa na Hospitali ya Wilaya imepandishwa hadhi na kuwa hospitali ya rufaa, kwa hiyo, wilaya tumepewa ile iliyokuwa kituo cha afya Frelimo kuwa hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, ile hospitali yetu iliyokuwa ya wilaya imekuwa hospitali ya rufaa, hivyo, wagonjwa wengi sana wamekuwa wakienda pale na kwa kuwa bado tunapata mgao kama kituo cha afya imesababisha sasa wagonjwa wengi kuwepo pale na akina mama wengi wanaojifungua kukosa ile huduma bure. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka, tangu 2013 jamani kwamba na sisi Iringa tupewe mgao kama hospitali ya Wilaya?

**SPIKA:** Ahsante sana, swali la pili fupi.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, swali la pili, niombe tena Serikali ione, je, hii migao inayokuwa inakinzana yaani unaipandisha hospitali hadhi halafu unaipa mgao wa kile kiwango cha awali, hawaoni hiyo inaweza kuwa ni sababu mojawapo ya malalamiko kwamba Sera hii haitekelezeki?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, afya ya uzazi, wajawazito na watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza alivyouliza swali lake ni suala ambalo tunahitaji tufuatilie tujue *specifically* kwamba kwenye hospitali yake mgao wake uko kwa namna gani.

Nikitoka hapa Mheshimiwa Mbunge tutakaa pamoja tuangalie ukweli wa hilo unalosema. Nimekwenda Hospitali ya Mbozi, wanatumia shilingi milioni 415 kwa mwaka kutibu kinamama na watoto, kwa hizi huduma zinazotolewa bure lakini wanapata *OC* kutoka Serikalini shilingi milioni 485 kwa mwaka, maana yake ukitoa hizo huduma wanabaki na zaidi ya shilingi milioni 60 kwa mwaka ambazo ni zaidi ya matumizi kwa huduma hizi ambazo zinatolewa bure.

Mheshimiwa Spika, hata ukienda Hospitali ya Mkoa wa Mbeya wamepewa dawa za shilingi milioni 53 pamoja na kuhudumia akina mama wakauza wakapata shilingi milioni 157 lakini mwisho wa siku wakaenda kununua dawa za shilingi milioni 29 maana yake ni chini hata ya dawa walizoziuza. Kwa hiyo, kimsingi ukiangalia tunahitaji tupate ushirikiano kwa Wabunge na viongozi wote ili tuhakikishe haya mambo tunaweza tukaya-*solve* kwa pamoja kwa sababu mengi ni ya kitendaji kule chini.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, lakini tunaenda kwenye bima ya afya kwa wote haya mambo yataweza kutatulika kwa urahisi zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kundi kubwa la watu wenye ulemavu wana vipato duni na hivyo inawapelekea kushindwa kumudu gharama za matibabu. Je, Serikali inaonaje ikiwatambua kama ilivyofanya kwa wazee na kuwapatia vitambulisho vya huduma za afya bila malipo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa swali hilo nzuri. Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Mbunge ni swali nzuri sana, lakini kwa sababu tunaenda kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, naamini wakati wa mjadala haya maswali yote na kuwahudumia watu wa namna hiyo tutaweza kupata namna ya kufanya. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunawatakia kila la kheri Wizara ya afya katika jambo hilo mnalojiandaa nalo maana Bunge lililopita tulihangaika nalo sana.

WaheshimiwaWabunge, bado tupo Wizara hiyo hiyo ya Afya, swali litaulizwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na. 11

**Dawa za Shinikizo la Damu Kutolewa Katika Ngazi ya Zahanati**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini dawa za shinikizo la damu hazitolewi katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Mollel kwa nini dawa za shindikizo la damu hazitolewi katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma,Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dawa za kutibu shinikizo la damu zimegawanyika katika makundi kulingana na namna zinavyofanya kazi na athari zake,hivyo basi utoaji wake unazingatia utaalam na uwezo wa kitaaluma, ndiyo maana kuna dawa hutolewa katika ngazi za Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa na Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ushauri mzuri wa Mheshimiwa Mbunge unatekelezeka, Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli imepeleka wataalam wengi wenye shahada ya udaktari mpaka ngazi ya kituo cha afya kwa lengo la kuhakikisha huduma nyingi na bora kama ulivyoshauriwa na Mheshimiwa Mbunge zinapatikana kuanzia ngazi ya chini na pia dawa hizi zimehusishwa katika mwongozo mpya wa matibabu nchini ili ziweze kutumika mpaka ngazi ya kituo cha afya na zahanati.

**SPIKA:** Sasa mbona Wizara ya Afya hamjajibu swali, sijui labda Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza sikusikia kama wamekujibu endelea.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, mgao wa fedha wa kununulia dawa kwa mwaka huu wa fedha zimeenda mara moja tu katika vituo vyetu vya afya na zahanati zetu na isitoshe fedha hizo zinakatwa juu kwa kwa juu kwenda kulipia deni sugu lililopo Bohari ya Dawa. Swali langu kwa Serikali, je, Serikali inamkakati gani kuhakikisha deni linalipwa na dawa zinapatikana katika zahanati na vituo vyetu vya afya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nataka kujua Serikali inampango gani kuhakikisha kwamba mgao wa fedha wa kununulia dawa haukatwi juu kwa juu kwenda kulipia deni hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Maswali yanakuwa mengi ndiyo maana mnaona Wabunge hata wakiweka ya

nyongezawanakwenda pembeni kidogo, lakini Naibu Waziri tuanze na lile la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:-**Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri, sijui mlivyokubaliana lakini tuanze na lile la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, *yes.*

**SPIKA:** Aliuliza kwa nini dawa za shinikizo la damu hazitolewi katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya na wewe umejibu vizuri kwamba sasa hivi hata watu wenye Shahada za Udaktari sasa wanapangwa kwenye vituo vya afya, kwa hiyo mmekubali kwamba sasa dawa za shinikizo la damu zitatolewa katika vituo vya afya au bado hamjakubali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, msisitizo uliowekwa nikwamba dawa za shinikizo la damu zinatolewa kulingana na zinavyofanya kazi, lakini na athari zake. Kwa sababu kuna dawa ambazo zinaenda kugusa moyo moja kwa moja na kuna dawa ambazo hazigusi moyo. Sasa utoaji wake unazingatia utaalam na uwezo wa wataalam wenyewe. Kwa hiyo, wakati tunaamuliwa ndiyo maana sasa utaona wakati kunadawa sasa hivi mpaka sasa zinatolewa kwenye zahanati, vituo vya afya, lakini inakwenda mpaka kufika rufaa.

Mheshimiwa Spika, kuna dawa zingine haziwezi kutolewa huko kulingana na utaalam ulioko katika sehemu husika. Kwa hiyo, sasa tunakwenda kuboresha kushuka chini kuhakikisha sasa wataalam ambao walikuwa wanapatikana tu katika hospitali za wilaya na za mikoa wanaanza kushuka chini sasa kuwepo kwenye maeneo hayo. Pia kuna mwongozo mpya ambao umetengenezwa ambao utaenda sasa kusaidia hizo dawa ziweze kupatikana kila mahali, ndicho ambacho tulimaanisha.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la nyongeza, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa sababu katika meseji nyingi ambazo nimekuwa nikirushiwa na Waziri na ambazo nilikuwa nazipata, tumepata meseji zake sana zinazokwenda kwenye *service delivery*. Bado narudi pale pale kwamba tunahitaji, ukiangalia nilieleza na nikasema kwamba umeona nimetoa mfano wa hospitali, nitoe Hospitali ya Katavi, tumekwenda Hospitali ya Katavi nao wamepewa dawa zenye thamani ya milioni 41, lakini wakauza hizo dawa pamoja na kuhudumia akinamama na watoto wakapata milioni 112, mwisho wa siku wakaenda kununua dawa za milioni...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali alilouliza Mheshimiwa Hawa Mchafu kama la nyongeza ni *national problem.*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** *Yes*.

**SPIKA:** Hela zinakatwa juu kwa juu...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, sawa, nakuja hapo. Kwa hiyo ukiangalia dawa za milioni 22 maana yake amenunua chini ya pesa aliyopata *MSD*, kwa maana hiyo ni kwamba utakuta utekelezaji kule chini kuna uwezekano wa hospitali zetu kuuza dawa na kupata pesa ya kutosha kupeleka kule na kuweza kuhudumia wananchi. Sasa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hujamsikia swali lake naomba ukae ulisikie tena swali lake. Mheshimiwa Hawa Mchafu nakupa nafasi uulize tena swali lako. Ngoja aulize tena swali ili wamsikie,*issue* siyo majibu,*issue* ni kumjibu swali ambalo mtu ameuliza. *(Makofi)*

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi tena. Mheshimiwa Waziri mgao wa fedha wa kununulia madawa kwa mwaka huu wa bajeti tuliokuwa nao, umeenda mara moja tu kwenye

vituo vyetu vya afya na zahanati zetu na isitoshe fedha hizo zinakatwa juu kwa juu kwenda kulipa deni sugu lililopo Bohari ya Madawa.Nataka kujua sasa mkakati wa Serikali juu wa ulipaji wa deni lililopo *MSD* na dawa ziendelee kuwepo katika vituo vyetu vya afya na zahanati zetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, wanampango gani kuhakikisha mgao wa fedha unaopangwa kwenda kununulia madawa haukatwi juu kwa juu kwenda kulipia deni?

**SPIKA:** Si mnaona Waheshimiwa Wabunge maswali yenyewe yalivyo, kwa hiyo ninatarajia majibu yaende kufuatana na swali hilo lilivyo. Mheshimiwa Dkt. Gwajima, Waziri mwenyewe wa Afya, tafadhali majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako tukufu kujibu swali naomba kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuifanya siku ya leo iwepo katika ramani ya mipango yake.

Mheshimiwa Spika, pili naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kuona kwamba natosha kuwa sehemu ya chombo hiki tukufu cha kuleta maendeleo katika nchi yetu. Tatu naomba nimshukuru sana familia hususani mume wangu *Advocate,* wakili msomi Metusela Gwajima Mpenzi wangu sana pamoja na watoto wetu...*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sasa majibu ya maswali ya nyongeza.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**Mheshimiwa Spika, Evelyn, Mary Mkubwa, Mary Mdogo na Victoria Gwajima.

Sasa Mheshimiwa Naomba nijielekeze kwenye swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu kuhusu dawa.

Mheshimiwa Spika, kweli dawa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha zimekwenda mara moja, lakini katika mfumo huu wa sekta ya afya tunapopeleka dawa kutoka *MSD,* sheria ni *cash* na *carry* kwamba ulipe ndiyo upewe hizo dawa, kwa kipindi kirefu vituo vyetu vimekuwa havitekelezi vizuri usimamizi wa *cost sharing* ile *user fees* pamoja na bima ili zirejeshe zile pesa huko. Hata hivyo, Serikali imeendelea kupeleka hizi dawa kule kwao, baada ya kuona kwamba wana madeni tukaweka utaratibu kwamba wao sasa wanaruhusiwa kwenda pale *MSD* wakasaini *contract* kwamba hizi pesa zisikatwe kwanza tupeleke kule tukafanye ule mzunguko turejeshe. Wengine wamefanya hivyo wanapelekewa hizo dawa kwa utaratibu huo wa makubaliano watalipaje deni, wengine hawafanyi hivyo. Kwa hiyo, nimelipokea, nimelichukua naomba nikawasiliane huko kwenye halmashauri tukaone tatizo liko wapi wa kutekeleza hiyo *offer*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la nyongeza la kwamba tutaendeleaje kuhakikisha kwamba pesa zinaenda na Serikali inaendelea kulipa hilo deni. Serikali inampango na mipango yake ni mipana kuimarisha makusanyo ambayo yamekuwa yakivuja sana kule kwenye hivi vituo, lakini pia kufuatilia matumizi ya zile bidhaa tunazopeleka kule. Hivi sasa ninavyosema kuna timu zetu ziko kule zinafanya ukaguzi. Kwa hiyo, msingi mkubwa hapa ni kwamba tunavitaka vituo viende *MSD* viingie makubaliano lile deni halitakatwa kiasi cha kuwanyima zile bidhaa zao, watachukua bidhaa tutaendelea kuimarisha ili nao watekeleze sheria ya *cash and carry*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Maswali ya afya yanahusu uhai wa watu, kwa hiyo ndiyo maana tumeyapa kipaumbele kikubwa. Pia Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri ametaja kabisa yeye ameolewa maana hapa kuna visumbufu sumbufu ni vizuri... *(Kicheko)*

Tunaenda Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wetu wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Tarimo tafadhali uliza swali lako.

Na. 12

## Vigezo vya Kupata Mkopo wa Elimu ya Juu

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi la kukosa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wenye ufaulu mzuri waliomaliza kidato cha sita kwenye shule binafsi kwa madai kuwa wanafunzi wanaosoma shule binafsi wazazi au walezi wao wana uwezo wa kuwalipia ada ya chuo.

Je, Serikali katika kuleta usawa kwenye fursa hii ya mikopo ya elimu ya juu haioni haja ya kutoa mikopo hiyo kwa kuzingatia ufaulu wa wanafunzi wote?

**SPIKA:** Swali hilo lijibiwe na Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Mbunge wa Mafia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele kwenye Bunge lako tukufu, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniona na kuniamini kwamba na mimi naweza nikawa miongoni wa watu wa kuweza kumsaidia.

Mheshimiwa Spika,baada ya hayo sasa, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inawalenga vijana wenye sifa za kitaaluma za kujiunga na taasisi za elimu ya juu lakini hawana uwezo wa kumudu gharama za elimu. Upangaji na utoaji mikopo unaongozwa

na Sheria ya Bodi ya Mikopo (Sura 178) ambayo inabainisha sifa za msingi za mnufaika ambazo zinajumuisha.Awe Mtanzania; awe amedahiliwa kwenye chuo kinachotambulika; awe ameomba mkopo, asiwe na vyanzo vingine vinavyogharamia masomo yake. Aidha, kusoma shule binafsi za sekondari siyo kigezo cha mwanafunzi mwombaji kunyimwa mkopo wa kugharamia elimu ya juu. Wapo wanafunzi waliosoma shule binafsi na wanapata mkopo baada ya kuthibitisha uhitaji wao kwa mujibu wa vigezo vya utoaji mikopo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa mujibu wa sheria tajwa, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ina mamlaka ya kuweka utaratibu wa kubaini wahitaji. Kwa sababu hiyo, Bodi huandaa mwongozo unaopaswa kuzingatiwa na waombaji na kuweka masharti ya utoaji mikopo kwa mwaka husika. Sifa za ziada zinazoainishwa kwa waombaji ni pamoja na; uyatima, ulemavu au wazazi wenye ulemavu na wale ambao masomo yao ya sekondari au stashahada yalifadhiliwa ambapo katika kundi hili wapo waombaji wengi waliosoma katika shule za sekondari za kulipia.

Mheshimiwa Spika, nashauri Waheshimiwa watusaidie kutoa elimu ili kuwezesha jamii kubadili mtazamo huu. Aidha, wawashauri waombaji wajaze kikamilifu fomu za maombi na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Bodi wakati wa uombaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kuambatanisha nyaraka zote muhimu ili kuepuka uwezekano wa mwanafunzi mwenye sifa stahiki kukosa mkopo kutokana na kutojaza kwa usahihi fomu ya maombi ya mkopo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la nyongeza Mheshimiwa Tarimo tafadhali.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia ningeomba niende mbele zaidi kwa sababu uhalisia unaonesha wanafunzi wanaosoma shule za binafsi hawapati mkopo *either* wote au kiasi, lakini pia kwa sababu ya umuhimu wa baadhi ya fani kama udaktari na gharama kubwa ya kusomesha watoto

kwenye fani hizo, Serikali inaonaje kuwa na mpango wa muda mrefu ili wanafunzi wote wameweze kupata mikopo kwa asilimia mia moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo, ni lini Serikali inaweza kusomesha watoto wote elimu ya chuo kikuu kwa asilimia mia moja ya mkopo, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyotokana na jibu langu la msingi, Serikali inaendelea kupanua wigo wa bajeti katika Bodi yetu ya Mikopo. Kwa hiyo naomba nilichukue suala la Mheshimiwa Mbunge kwa vile kutoka mwaka 2017, Serikali imeweza kuongeza bajeti katika bodi ya mikopo kutoka bilioni 427 mpaka hivi sasa tuna bilioni 460. Kutokana na hivyo basi, wanufaika ni wengi na wanaendelea kuongezeka kutoka wale laki moja katika kipindi cha mwaka 2015 mpaka kufikia laki moja na arobaini mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapoongeza bajeti hii tuna hakika tunaweza kufanya *coverage* kubwa ya wanafunzi. Naomba kutoa taarifa katika waombaji wa mwaka huu wale wa mwaka wa kwanza maombi yote yalikuwa 66,000, lakini waliopata jumla karibu walikuwa 55,000. Kwa hiyo tunaendelea kuongeza ule wigo kwa lengo kuhakikisha kwamba wanufaika wanakuwa wengi zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante; ni dhahiri kwamba Watanzania wengi ambao unakuta wamemaliza kidato cha sita na wengine ambao wanasifa za kwenda vyuo vikuu wanatamani sana kupata mikopo ya elimu ya juu ili tuweze kuwa na wataalam wa fani mbalimbali. Mikopo hii inapotolewa tumeweka riba kubwa sana ya asilimia kumi na tano ambayo ipo katika sheria ya 2016 na penati ya asilimia sita. Hivyo, tunakuta wanufaika wengi ambao ni watoto wa familia maskini wanashindwa kulipa au

kubeba huu mzigo. Je, ni lini sasa Serikali italeta mabadiliko ya sheria hii angalau tupeleke kwenye *singledigit* kwa maana ya asilimia nane au tano ili tuwe na lengo la kutoa wajuzi na siyo kugeuza kama chanzo cha mapato? Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza swali lake la nyongeza ukiangalia kwa kiasi kikubwa haliendani na swali la msingi, lakini kwa sababu ya umuhimu wa masuala ya Bodi ya Mikopo, ningependa kwanza kuonesha kwamba mwombaji wa kwanza anasema wanafunzi wote wapate mikopo, lakini mwombaji wa pili anasema makusanyo wapunguze.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha Mfuko huu wa mikopo ilikuwa ni kwamba watu wafanye marejesho, mikopo ijiendeshe yenyewe kama vile *revolving fund* yaani yale marejesho yakikusanywa yatosheleze kuwapatia wanafunzi wengine. Kwa hiyo, ukiangalia hata sasa makusanyo ya mikopo yanachangia asilimia 46 ya bajeti ya mikopo. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba umuhimu wa kurejesha mikopo upo na asilimia 15 ambayo mwanafunzi anakatwa, anabaki na asilimia 85 ya mkopo wake, tukumbuke kwamba mkopo wa Bodi ya Mikopo ndiyo uliotangulia kabla ya mikopo mingine na Kanuni za Utumishi makato ni kwamba mtumishi anatakiwa abaki na theluthi moja ya mshahara.

Mheshimiwa Spika, nawasihi wanaochukua mikopo, waone umuhimu wa kulipa na wale wenye fedha wasisubiri kukatwa hiyo asilimia kumi na tano, kumi na tano ili wanafunzi wengine waweze kunufaika kama wao walivyonufaika, wakaweza kupata ajira. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa Wabunge watusaidie kutoa elimu kuonesha umuhimu wa kurejesha mikopo kwa sababu marejesho hayo ndiyo yanawasaidia wengine kupata mikopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na swali langu nililokuwa nauliza, ameuliza Mheshimiwa Matiko. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Niliona Mbunge mmoja kule mwisho, utataja jina lako Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Hivi karibuni tumepata kuona kupitia mitandao, mwanafunzi aliyejulikana kwa jina Asia ambaye alifaulu vizuri masomo yake ya sayansi amepata *division two* ya *point* kumi na moja, lakini mwanafunzi huyu alikosa mikopo bila sababu ya kueleweka, ni mpaka baada ya kujiweka wazi mitandaoni na kulia sana ndipo *Loan Board* ikaweza kumpa mkopo mwanafunzi huyu.

Naomba kuiuliza Serikali; mwanafunzi huyu ambaye alifaulu vizuri, tena mtoto wa kike na masomo ya sayansi, imekuwaje akakosa mkopo na ni kigezo kipi walikitumia baadaye kumrudisha ili kuweza kupata mkopo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali lako ni zuri sana Mheshimiwa Mwanaisha lakini ni *very specific,* linahitaji muda. Mimi namuagiza tu Mheshimiwa Waziri afanye utaratibu wa kukutafutia jibu hilo halafu mtaongea kwa wakati wenu. *(Makofi)*

Tuendelee na Mheshimiwa Edward Kisau OleLekaita, Mbunge wa Kiteto, uliza swali lako.

Na. 13

**Ujenzi wa Chuo cha VETA Kiteto**

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika Jimbo la Kiteto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga vyuo vya ufundi stadi ikiwa na lengo la kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi katika kila mkoa na kila wilaya. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilitenga jumla ya shilingi bilioni 48.6 kwa ajili ya kujenga vyuo 29 vya *VETA* katika ngazi za wilaya ambavyo kwa sasa viko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili kuendelea kutekeleza azma yake ya kuwa na chuo cha ufundi stadi katika kila mkoa na wilaya nchini ikiwemo Wilaya ya Kiteto. Aidha, endapo Halmashauri ya Kiteto inayo majengo ambayo yanakidhi vigezo vya kutumika kwa *VETA,* Wizara yangu itakuwa tayari kununua vifaa kwa ajili ya kuwezesha majengo hayo kuanza kutumika mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali na yenye kutia moyo.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kama tuna majengo ambayo yana hadhi yuko tayari kununua vifaa, je, atakuwa tayari hata ndani ya Bunge hili wakati linaendelea, kutembelea Kiteto ukiongozana na mimi kukagua baadhi ya majengo tuliyonayo ili tuweze kuangalia kama hilo linawezekana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Vyuo vya *VETA* ni muhimu sana kwa taifa letu na hususan kwa vijana; na kwa kuwa Wilaya ya Kiteto ni wilaya kongwe sana nchini, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwahakikishia wananchi wa Kiteto kwamba Wilaya ya Kiteto *VETA* iko kwenye *priority list* na Chuo cha *VETA* kitajengwa kwa manufaa ya Taifa letu? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Juma Omar Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kutembelea Kiteto liko wazi, nitamuomba Mheshimiwa Mbunge baada tu ya kikao hiki tuweze kuonana ili kuiweka ratiba yetu vizuri ya kwenda kuona huko Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili alilolizungumza ni dhahiri, nilibainishie tu Bunge lako Tukufu kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali ina azma thabiti ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga vyuo vya *VETA* katika kila wilaya na mkoa nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, vijana wetu hawa pamoja na kupata taaluma katika vyuo hivi vya *VETA,* tuna vyuo vyetu vilevile vya *FDC.* Mfano, hukohuko Kiteto Chuo cha Wananchi cha Tango kinafanyiwa ukarabati mkubwa na kitaanza kutoa fani za mifugo, kilimo, umeme, ushonaji na uwashi. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge vijana wetu sasa wanaweza kwenda kujipatia

taaluma zao pale, lakini tuna vyuo vingine vya *VETA* vilivyoko katika Mkoa wa Manyara ambapo napo vilevile wanaweza kwenda kupata mafunzo hayo. Hata hivyo, suala la mpango wa Serikali wa kujenga vyuo vya *VETA* katika kipindi kijacho tutakapopata fedha tutahakikisha tunapeleka chuo katika Wilaya ya Kiteto. Ahsante.

**SPIKA:** Tumalizie na Wizara ya Madini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda na swali la Mheshimiwa Anthony Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe.

Na. 14

**Kufufua Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2019 ya kufufua mradi wa uzalishaji wa makaa ya mawe Kiwira itatekelezwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nami kwa vile nasimama kwa mara ya kwanza mbele ya Bunge lako Tukufu, nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia Mheshimiwa Rais kwa imani aliyonipatia kutumika katika utumishi huu mtukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira ulikabidhiwa Serikalini kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* mwaka 2013 kwa lengo la kuuendeleza. Katika jitihada za kuuendeleza mgodi huo ambao ni wa chini ya

ardhi, *STAMICO,* kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* wanaendelea na mpango wa pamoja wa muda mrefu wa kuzalisha umeme zaidi ya MW 200 kutoka katika mgodi huo. Makubaliano ya Ushirikiano *(MoU)* yako hatua za mwisho kukamilika kabla ya kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapitio.

Mheshimiwa Spika, tayari timu ya wataalamu wa *STAMICO* na *TANESCO* wametembelea eneo la mradi kwa lengo la kutambua mahitaji halisi ya uendelezaji wa mradi huo. Aidha, maandalizi ya kuhuisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi ya mwaka 2007 yanaendelea. Katika taarifa hiyo, tathmini ya awali inaonesha kwamba jumla ya mashapo yanayokadiriwa tani milioni 93 yapo katika eneo hilo na gharama zinakadiriwa ni jumla ya Dola za Kimarekani milioni 480 ambazo zitahusisha kuchimba makaa ya mawe, kujenga mtambo wa kuzalisha umeme na kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka eneo la mradi yenye urefu wa kilometa 100.

Mheshimiwa Spika, malengo ya muda mfupi ni kuendelea na uchimbaji wa makaa ya mawe kwa matumizi ya viwanda vya ndani na nje ya nchi. Kwa sasa uchimbaji huo unaofanywa na *STAMICO* unaendelea katika eneo la Kabulo ambapo tangu mwaka 2017 uchimbaji ulipoanza hadi kufikia Desemba, 2020 Shirika limezalisha tani 50,949 za makaa ya mawe na kuuza tani 29,686.56 zenye thamani ya shilingi 2,264,472,998.70. Baadhi ya makaa hayo yameuzwa kwenye viwanda vya simenti nchini vikiwemo viwanda vya *Mbeya Cement, Lake Cement* pamoja na kampuni ya *Sanflag* ya Jijini Arusha.

Mheshimiwa Spika, Shirika limefanya tathmini ya ukarabati wa miundombinu ya mgodi wa chini wa Kiwira kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa makaa ya mawe ili kuendelea kuvipatia viwanda malighafi hiyo, lakini pia ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uzalishaji mkubwa kwa ajili ya mitambo ya kuzalisha umeme pindi makabuliano na *TANESCO* yatakapokamilika. Aidha, shirika liko katika maandalizi ya mwisho ya kuanza ukarabati wa miundombinu hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nadhani kila mtu anajua faida ya mradi wa makaa ya mawe pale *Kiwira Coal Mine.* Kwanza huu mradi ulikuwa unazalisha ajira zaidi ya 2,500 kabla haujaisha na mara kwa mara suala hili limejadiliwa hapa kwenye Bunge lako tukufu. Mwaka 2006 iliahidiwa na Wizara hii kwamba huu mradi utaanza mara moja, chini ya Naibu Waziri kipindi kile, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani; mwaka 2018 pia ikajadiliwa hivyo kwamba mradi utaanza mara moja, sasa hivi tunaambiwa tena kwamba wako katika hatua za mwisho.

Je, ni lini ukarabati wa mgodi huu wa mawe utakamilika na tunategemea kuajiri watu wangapi? Kwa sasa hivi katika sehemu hii ndogo tumeajiri watu 28 tu lakini *capacity* ya kwanza ilikuwa ni watu 2,500.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini Serikali itatoa ahadi ya uhakika kwa sababu 2016 tumeahidiwa, 2018 tumeahidiwa, sasa hivi tunaambiwa tena mradi utaanza; ni lini Serikali itatoa ahadi ya uhakika ambapo sasa tutapata ajira za kutosha kwa wananchi lakini pia tutapata za huduma za kiuchumi kwa Wilaya za Rungwe, Kyela pamoja na Ileje? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Prof. Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa majibu katika swali la msingi, ni kweli kwamba Shirika liko katika maongezi na *TANESCO* ili kukamilisha hatua za mwanzo kwa ajili ya uchimbaji kuanza. Napenda Mheshimiwa Mbunge ajue kwamba taratibu za uchimbaji zinahusisha upembuzi yakinifu kwa sababu unapokuja kuwekeza unawekeza fedha nyingi. Kwa hiyo, tunapokuwa tunasema kwamba upembuzi yakinifu unafanyika, lengo ni kwamba tunapoingia katika uchimbaji tuweze kuingia kwa namna ambayo tunajua kile kilichopo, fedha inayoingizwa na hatimaye kupata faida.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tuko katika maongezi na kuhitimisha hatua hizi, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili litafanyika baada ya kuhitimisha hatua hizi za mwanzo. Ajira zinazotarajiwa kupatikana tunaweza tukazipata baadaye baada ya kuwa tumemaliza upembuzi wote yakinifu kwa ajili ya mradi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa majibu hayo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa *Engineer* Magesa, Mbunge wa Busanda.

Na. 15

**Maeneo ya Mgodi yanayomilikiwa na STAMICO bila Kuyatumia**

**MHE. BRYCESON T. MAGESSA** aliuliza:-

*STAMICO* inamiliki maeneo yenye dhahabu lakini haiyatumii huku wachimbaji wadogo wakiwa hawana maeneo ya kuchimba.

Je, kwa nini Serikali isiwapatie wachimbaji wadogo maeneo hayo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Profesa Shukrani Manya.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bryceson Tumaini Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* ni kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini. Katika kufanya hivyo Shirika limekuwa likifanya kazi kwa karibu sana na wachimbaji hao katika kuhakikisha kwamba wanaongeza uzalishaji katika

maeneo wanayochimba. Kupitia mkakati huo, Shirika pia limekuwa likitoa maeneo yake kuwapatia wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwaendeleza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018, Shirika lilitoa maeneo ya uchimbaji kwa vikundi 15 vya wachimbaji wadogo vilivyoundwa katika eneo la Lwamgasa (Geita) kwa usimamizi wa viongozi wa Kijiji na Afisa Ushirika yenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.08. Vilevile, mwaka 2019, Shirika liligawa pia eneo la leseni ya Buhemba kwa vikundi vya wachimbaji wadogo waliopo Ilasaniro Mkoani Mara lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1.2 na jumla ya leseni ndogo za uchimbaji 15 ziligawiwa. Aidha, kwa kushirikiana na mbia Shirika lilitoa leseni tatu katika eneo lake la mradi wa Buckreef (Geita) kwa wachimbaji wadogo wa maeneo hayo yenye jumla ya kilomita za mraba 7.2.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa sasa hakuna maeneo ambayo yanamilikiwa na *STAMICO* bila kuendelezwa. Shirika linaendelea kuendeleza maeneo yake kwa kufanya utafiti ili kujua kiwango cha mbale kilichopo kabla ya kuanza uchimbaji. Pia Shirika limeanza kuendeleza leseni yake ya dhahabu ya Buhemba kwa kushirikiana na mbia na uzalishaji unatarajiwa kuanza Septemba mwaka huu 2021. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Magesa, swali la nyongeza la mwisho.

**MHE. BRYCESON T. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, ni lini atakuwa tayari yeye na *STAMICO* twende kupitia katika maeneo ambayo mimi najua bado kuna tatizo ili tuweze kumaliza matatizo yaliyopo kule?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa *STAMICO* kazi yake, pamoja na majukumu mengine, ni kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo waliopo Busanda wengi wanabahatisha kujua dhahabu iko wapi. Je, ni lini *STAMICO* itakuwa tayari ama kuwakodisha vyombo au

kujitolea ili waweze kutambua mahali wanapochimba kuna madini au hakuna badala ya kubahatisha?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge Tumaini Magessa kutoka Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kikao hiki nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ipo tayari kutembelea Jimboni kwake na kuona maeneo wanayodhani kama yanahitaji kugawiwa kwa wachimbaji wadogo au la.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Mbunge ajue kwamba Serikali imeendelea kuyatoa haya maeneo kila inapoona kuwa inafaa. Nadhani hata yeye mwenyewe katika jimbo lake ni shahidi kwamba maeneo mengi yameendelea kutengwa na kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imewathamini sana wachimbaji wadogo na ndipo wakati ambapo wachimbaji wadogo nchini wamepewa maeneo mengi sana kwa ajili ya kuchimba.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sasa hivi Serikali inaendelea kuimarisha Shirika letu la *STAMICO* na siku za karibuni shirika limeweza kununua mitambo ya *drilling* ya kwake yenyewe. Kwa jinsi hiyo, tunaamini kwamba jitihada hizi zinazochukuliwa na Serikali za kuimarisha Shirika la *STAMICO* zitawezesha sasa kuweza kupata namna ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kufanyia utafiti ili sasa tunapoelekea maeneo yanayotengwa yawe ni yale ambayo yamefanyiwa tafiti na hatimaye kuwawezesha kuchimba kwa tija. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa tumeanza vizuri, natumaini tutaendelea vizuri namna hiyo. Leo tulienda muda zaidi kidogo kwa sababu tulichelewa kuanza kutokana na masuala yanayoendana na Bunge linapoanza *day one.*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni watatu wa Mheshimiwa Spika kutoka Taasisi ya *East African Nguvu Kazi and Jua Kali Partners* ambao ni Mkurugenzi wa Taasisi huyo Ndugu Elliot Mnzava, mwalimu mstaafu; Katibu Mkuu, Ndugu Janiva Chamlomo; na Mweka Hazina, Ndugu Shairi Bin Saidi. Naomba msimame; karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambaye ni Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo wa Hoteli ya Serena ya Jijini Dar es Salaam, Ndugu Seraphine Lusala. Ahsante sana Lusala, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni wawili wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni wapiga kura wake, Ndugu Mwita Enock Isaac na Ndugu Mwise Marwa Chacha. Karibuni sana, wako pale juu. *(Makofi)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Esther Matiko kutoka Tarime Mkoani Mara wakiongozwa na baba yake mzazi Ndugu Nicholas Matiko. Wageni kutoka Tarime, leo Tarime iko hapa. Karibuni sana wageni wetu kutoka Tarime. Natumaini kila mtu hapo hana panga mfukoni, karibuni sana wapendwa. *(Kicheko)*

Naomba baba na mama yake Mheshimiwa Esther Matiko wasimame, wengine tukae. Hongereni sana wazazi na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni ndugu zake kutoka Rungwe, Mkoa wa Mbeya, Ndugu Juma Mwambero; Ndugu Michael Simon; na Ndugu Victor Joseph. Karibuni sana wageni wetu kutoka Rungwe. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni familia na marafiki zake kutoka hapa hapa Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Mwanahawa Komba. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni 62 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi wa Tanzania kutoka Mbeya, Njombe, Morogoro, Arusha na Dar es Salaam. Wanamaombi, karibuni sana wanamaombi. *(Makofi)*

Hapa hapa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa *chapel* ya Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba saa saba baada ya kuahirisha shughuli zetu hapa kutakuwa na ibada kwenye *chapel* ya Bunge ambayo iko katika Ukumbi wa Msekwa. Tushirikiane na wageni wetu hawa ili kufanya maombi kama ilivyo ada; mliombee Bunge letu kama kuna mapepo basi yaruke kabisa.

Wako viongozi saba kutoka Kampuni *Almansour Auto East Africa (Tanzania) ISUZU* na wakala wao *SASN Auto Garage Ltd,* wakiongozwa na Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo Anurup Chatterjee; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ukitaka Isuzu mpya kabisa kampuni hii inatoa huduma hizo; nadhani wana banda lao *somewhere* nyuma kule ya Msekwa, ni vizuri kutembelea kule. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Chibelela iliyoko Mkoani Dodoma ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya shughuli zake. Hii Chibelela iko katika Wilaya ya Bahi. Wanafunzi wa Chibelela! Eh, watoto wanapendekeza hawa! Hii ni Shule ya Sekondari ya Kata, lakini mnaona wanavyopendeza? Kweli elimu imekua kabisa. Hongera sana Mheshimiwa Nollo.

Mheshimiwa Nollo uko wapi wakuone watoto wako? Mheshimiwa Nollo anakaa upande gani? Jamani Mbunge wenu mmemwona? Yupo humu ndani. Hongereni sana. *No wonder* shule zetu za Kata zinapata *division one* mpaka ya *point* 11, 12 na 13 kabisa kabisa! Hongereni sana Chibelela. Ni maendeleo makubwa. *(Kicheko/Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 12 wanaosoma Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Frederick Mwita. Wanafunzi wa *UDOM*. Ooh, karibuni sana. Karibuni sana *UDOM*. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hotuba ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili, Tarehe 13 Novemba, 2020**

**SPIKA:** Tunaingia katika hoja ya wiki hii. Nimepata baadhi ya majina ya Waheshimiwa Wabunge ambao wako tayari kuchangia, lakini Spika naye huwa na dakika zake. Kwa hiyo, kama humo katika orodha hiyo na ungependa kuchangia leo, pia unaweza kumwandikia Spika moja kwa moja ili kama nina dakika zangu zimebaki hapa, unaweza ukapata nafasi.

Ukiamini kwamba utachangia Alhamisi au Ijumaa, unajidanganya; utakuta siku hiyo orodha imejaa, nafasi huna. Kwa hiyo, ni vizuri ukiwa tayari leo, kesho au keshokutwa, wewe jipange uchangie kama tulivyokuwa tumeambiana.

Kwa hiyo, watakaokuwa wachangiaji wa kwanza wanne ni Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Jafari Chege, Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete na Mheshimiwa Noah Lemburis. Kabla ya ninyi wachangiaji, basi naomba sasa nitoe nafasi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kuweka hoja mezani.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Kamati ya Bajeti mkaendelee na shughuli zenu baada ya Waziri Mkuu kumaliza.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, ni bahati iliyoje kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wa Bunge hili la Kumi na Mbili walikuwepo wakati huo Mheshimiwa Rais akihutubia Bunge lako Tukufu. Hivyo, walipata fursa ya kumsikia moja kwa moja akiainisha kuhusu mipango na mwelekeo wa Serikali kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba wakati akieleza vipaumbele mbalimbali vitakavyotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Mheshimiwa Rais aliweka bayana kuwa mambo yote muhimu yatakayotekelezwa yamebebwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025. Kadhalika, alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kutekeleza na kusimamia pamoja na masuala muhimu aliyoyaeleza kwenye hotuba yake ya kuzindua Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, sambamba na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa ahadi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa aliyoitoa wakati akizindua Bunge la Kumi na Mbili sambamba na Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba inakamilisha utekelezaji wa vipaumbele vyote ambavyo havikukamilika katika kipindi kilichopita sambamba na kusimamia ipasavyo maeneo mapya yaliyoibuliwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na

Hotuba ya Rais ya tarehe 13 Novemba, 2020 wakati akizindua Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, utekelezaji wa maelekezo yake ulianza mara moja kwenye maeneo mbalimbali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Wizara na Taasisi zote za Serikali zilichukua hatua za makusudi kuchambua hotuba hiyo, kuainisha maeneo mbalimbali muhimu ya utekelezaji sanjari na kuja na mipango ya utekelezaji na hasa wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni ndoto ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kuona kwamba Tanzania inajenga uchumi imara, shindani sambamba na kutengeneza ajira za kutosha kwa Watanzania. Hivyo basi, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutumia vyema fursa hii adimu katika kujadili na kutoa mchango wa namna ambavyo tunaweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, licha ya ukweli kwamba tayari utekelezaji wa masuala mbalimbali umeshaanza kwa kiasi kikubwa, bado michango ya Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana katika kuisaidia Serikali kutekeleza kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo tutaijadili kwenye Mkutano huu wa Pili wa Bunge lako Tukufu kwa siku nne.

Mheshimiwa Spika, nimalizie maelezo yangu kwa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba michango yenu itaheshimiwa, itathaminiwa na pia itafanyiwa kazi kwa lengo la kushughulikia kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Bunge zima. Kwa hiyo, nawashukuni sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuanzishia shughuli nzima ya Hoja ya Serikali ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Mbili, siku ya tarehe 13 Novemba, 2020. Kwenye *tablets* zenu iko Hotuba ya mwaka 2015 na Hotuba ya mwaka 2020.

Sasa moja kwa moja kama ilivyo ada, tunakwenda na dakika kumi kumi zetu. Mheshimiwa Charles Mwijage atafutiwa na Mheshimiwa Jafari Chege. Mheshimiwa Mwijage tufungulie dimba.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuwa mtu wa kwanza katika kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote, nisije nikasahau, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa hapa na hotuba alizozitoa wakati anaomba ridhaa ya kuongoza kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Rais na zile nyingine na hasa Andiko la Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inaonyesha dhahiri nia ya Mheshimiwa Rais ya kuhuisha au kujenga upya Dira ya Taifa ya 2020 – 2025. Mheshimiwa Rais nikimnukuu, anasema Taifa hili siyo maskini, lina rasilimali nyingi na anataka kwenda kwenye uchumi mkubwa. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutembea na maneno yake. Alipochukua fursa ya kuteua Baraza la Mawaziri, akachukua Wizara ya Uwekezaji akaiweka chini ya mamlaka yake, yaani yeye ndiye Waziri wa Uwekezaji na akamteua rafiki yangu awe Waziri wa Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanya hivyo kwa nia moja. Wawekezaji wako wa kila namna; na kuipeleka

nchi hii katika uchumi mkubwa, lazima uchangamshe uwekezaji. Hata mkulima yule wa nyumbani ambaye ametuwezesha kuishi miaka mitano iliyopita bila njaa, naye ni mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Rais, nashauri, ili tuweze kufikia malengo yetu, lazima vile vigezo tulivyovipitia katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kugundua kwamba vinatuwekea vikwazo, basi vyote avipeleke, aviweke chini yake kama ambavyo Bunge hili liliwahi kumshauri.Namaanisha *blueprint*. The *Blueprint of RegulatoryReform* iwekwe chini ya Rais ili Wizara na Taasisi nyingine aweze kuzielekeza namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, sifungui mjadala, lakini hata ungekuwa mganga wa namna gani uliyebobea, huwezi kujifanyia *operation* kubwa wewe mwenyewe. Wizara yoyote yenye jukumu la kukusanya maduhuli, haitakubali haraka sana kuondoa hayo maduhuli au kodi mbalimbali mpaka Mheshimiwa Rais mwenyewe aseme wewe punguza hapa, punguza hapa, punguza hapa.

Mheshimiwa Spika, nazungumza sana suala la Wizara hii anayoisimamia Mheshimiwa Rais kwa sababu jitihada ya kufikia ule uchumi wa kati na kwenye uchumi mkubwa linahusisha uwekezaji. Nami napenda nitangaze *interest*; uwekezaji ninaoushabikia ni wa zile sekta za uzalishaji *(the productive sectors)*.

Mheshimiwa Spika, tumefanya vizuri kwenye miundombinu, tumefanya vizuri kwenye elimu, sasa ni wakati wa kuhakikisha tunazidua sekta za uzalishaji, tunalima kwa tija kubwa; kama alivyoniambia Profesa Mkenda kwamba, kupungua kwa bei ya mazao siyo hoja, lakini kipato cha mkulima kisipungue, hata bei ikishuka. Sasa jibu hilo ni kuongeza tija katika shughuli na kuongeza tija katika shughuli maana yake ni uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nina falsafa, nina neno langu ninalolisema kila siku kwamba sasa tuweke

*flagship project* katika shughuli za sekta za kiuzalishaji katika kilimo, uvuvi na katika sekta za namna hiyo. Kwa sababu gani? Hoja siyo kujenga uchumi mkubwa, hoja yetu ni kujenga uchumi mkubwa ulio jumuishi. Unaweza kuzidua mafuta, ukazidua madini ya namna mbalimbali, ukawa na *GDP* kubwa, ukawa na *income per capita* kubwa sana, lakini ukawa na watu wenye matambara, ombamba; lakini sekta hizi ni *productive sectors* ambazo zinahusisha watu wengi.

Mheshimiwa Spika, yote haya yapo, tumeyashughulikia, tumehangaika nayo miaka mitano, sasa ni mwendo wa kupaa. Kwa mara nyingine namuunga mkono Mheshimiwa Rais, nasi wapambanaji wake tuko tayari kupaa naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia sekta za uzalishaji, lakini jambo moja ambalo nataka niishauri Serikali, katika maandiko iko kauli ya kwamba tuzalishe kiasi cha kutosha na ziada tuuze nje. Kwa heshima na taadhima, napenda kuishauri Serikali yangu tuondokane na falsafa hiyo. Unapokwenda kuzalisha, uende na malengo mawili makuu, ambapo lengo moja haliathiri lengo lingine. Uende kuzalisha kutosheleza soko la nchi hii na uende kuzalisha ili kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa au Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa miaka mitano tuliweza kuuza nje dola bilioni nane na kitu mpaka dola bilioni tisa. Ni mtazamo chanya, lakini siyo namba ya kujivunia, kwa sisi waumini sehemu tulipo, *locational advantage*; tungetegemea nchi hii iuze sana. Kwa hiyo, zalisheni ili kuuza katika nchi hii na kuuza nje kusudi tuweze kupata fedha za kigeni na kupata uzoefu wa masoko ya nje. Ukizalisha leo kutosheleza maisha ya nchi hii au mahitaji ya nchi hii, wenzako wanaokamata soko la nje, hutakaa kuwatosheleza au kuwaingilia kwenye masoko yao wakati wewe utakapokuwa umemaliza hapa.Ninayo mifano mingi, muda siyo rafiki.

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono tena Mheshimiwa Rais kwa kauli yake. Tunatambua kazi nzuri

tuliyofanya kwa miaka mitano; watoto wengi wamekwenda shule. Mheshimiwa Rais akasema, kipindi hiki sasa ni kuongeza ubora katika sekta ya elimu. Naungana naye, tuongeze ubora katika wanafunzi ambao wameingia katika shule zetu waweze kuwa na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila na niko tayari kutoa *album*, siyo *single* tena; naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuweka jiwe la msingi jengo ambalo limekaribia kukamilika la *VETA* ya Mkoa wa Kagera, jengo lenye thamani ya shilingi bilioni 22 linaloweza kupokea wanafunzi 800 kwa wakati mmoja. Ndiyo maana nilipofurahi nikakumbuka ule wimbo alionifundisha bibi kwamba senene ni tamu kuliko nyama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Kicheko/ Makofi)*

**SPIKA:** Huyo ndio Mheshimiwa Charles Mwijage, ambao hamjaonja senene basi mnashauriwa mwonje maana ni tamu kuliko nyama.

Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete**.**

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nami niungane na mchangiaji aliyetoka kuchangia, kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili na ni mara yangu ya kwanza wananchi wamenipa ridhaa ya kuongoza ndani ya Jimbo la Rorya, Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza nimeona namna unavyoliongoza Bunge, lakini imetupa faraja hasa Wabunge wengi wapya; kwa namna ambavyo tulikuwa tunakuona nje na hakika wewe ni kiongozi bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kabla sijasahau Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hotuba zote mbili za Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; hotuba ya kwanza ilikuwa ya kufunga Bunge na ile aliyoitoa Novemba ya kufungua Bunge. Naunga mkono hoja hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nami niseme tu kwamba hotuba ya Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ilikuwa na mwelekeo chanya, ni hotuba ambayo ina matumaini mazuri kuanzia ngazi zote na sekta zote za kibiashara na kiuchumi na shughuli nyingi za ukuaji na ustawi wa jamii kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaenda kuchangia kwenye baadhi ya maeneo ambayo nimeona angalau niweze kuchangia katika kuboresha na katika utekelezaji wake utakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu katika hotuba yake ukurasa wa 34 na 35 amezungumzia namna ambavyo Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano chini ya Chama chetu Cha Mapinduzi, ilifanya kazi kubwa sana katika uboreshaji na uinuaji wa sekta ya maji. Nichukue nafasi hii kwa moyo wa dhati sana kumshukuru Waziri mhusika wa Wizara hii. Naweza kusema, kwa muda mfupi wa miezi hii mitatu, mimi nimepata ridhaa ya kutembelewa na Waziri wa Maji. Kwa kweli nichukue nafasi hii kumpongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya. Ni imani yangu alikuwa anatekeleza yale ambayo Mheshimiwa Rais amemwagiza na ndiyo haya ambayo wananchi wetu wanatarajia kuyaona.

Mheshimiwa Spika, jimbo langu kwa asilimia 77 limezungukwa na maji; asilimia 23 peke yake ndiyo eneo la nchi kavu ambalo wananchi wanalima na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi. Kwa miaka yetu mitano kwa chama chetu na Mheshimiwa Rais wetu, alituletea zaidi ya shilingi bilioni saba kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji. Nilikuwa naiona hapa kwenye hotuba yake hapa ameisema, hizi shilingi trilioni 2.2 ambazo zimeletwa kuinua na kuboresha

sekta ya maji, sisi katika Jimbo letu ni miongoni mwa Majimbo ambayo yamepokea fedha hizi, lakini niseme tu kwamba haikutumika vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuja kufanya ziara yake, ndiyo maana nimesema nianze kumpongeza, kuna maelekezo aliyatoa kutokana na namna fedha hizi zilivyotumika. Niendelee tu kumwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kukazia hapo, kwa sababu ndani ya Jimbo langu, nina changamoto kubwa sana ya maji. Unaweza kuona hiyo asilima 77 ambayo inazungukwa na maji, lakini hatuna mradi mkubwa unaotokana na Ziwa Victoria, asilimia iliyobaki 23 ndiyo maeneo ya nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitupa fedha ili angalau fedha hizi ziweze kuinua na kuwasaidia wananchi wanyonge hasa akina mama lakini haijatumika sawasawa. Nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kukazia wakandarasi wote ambao walichukua hizi fedha za umma ili angalau waweze kurudi sasa kuweza kutimiza na kumalizia hii miradi.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukakuta mkandarasi ametekeleza mradi kwa asilimia sitini lakini amelipwa asilimia mia moja na ameuacha ule mradi hauna maji. Amelipwa zaidi ya shilingi bilioni moja na ushee. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kukazia ili tuweze kulipata hili.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amezungumza namna tulivyofanya kwa miaka yetu mitano na matarajio yake ya miaka mitano kwenye sekta ya afya. Mimi nishauri kidogo kwenye Wizara yetu hii ya Afya, ndani ya jimbo langu mimi nina vituo vinne tu vya afya lakini kiukweli kwa *population* na wingi wa watu ulivyo, vituo vya afya hivi havitoshi na unaweza ukakuta kituo kimoja cha afya kinahudumia zaidi ya vijiji 27. Kwa malengo mazuri ya Mheshimiwa Rais na naamini namna Waziri wa Afya anavyofanya kazi kwa muda toka amechaguliwa namwomba aitazame Rorya katika kipengele hiki cha upande wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu unaweza ukakuta kituo kimoja cha afya kinahudumia zaidi ya vijiji 27, kina kata zaidi ya nane lakini ndani ya hicho kituo cha afya unakuta bado hakijapata huduma ya *ambulance,* wakati mwingine kuna changamoto kubwa sana kunapokuwa na wagonjwa kumtoa kwenye kata moja kumpeleka kwenye hospitali ya wilaya au kumsafirisha kwenda kwenye hospitali ya mkoa. Kwa hiyo, naomba na lenyewe hili ili kuendana na yale mazuri ambayo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameyazungumza kwenye hotuba yake tuyaboreshe sasa tuendane na kasi hiyo katika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, la tatu, Mheshimiwa Rais amegusia vizuri sana upande wa barabara na sisi wote ni mashahidi kwa kazi kubwa iliyofanyika miaka mitano iliyopita. Tuna barabara ambayo imezungumzwa kwenye Ilani toka mwaka 2010, 2015, 2020, barabara ya kutoka Mika - Shirati, lakini inanyooka mpaka Kilongo kule mpakani. Barabara hii ina umuhimu wa aina mbili, moja ni barabara ambayo inainua uchumi ndani ya Jimbo letu la Rorya, lakini ni barabara ambayo kiusalama kwa sababu sisi tuko mpakani inaweza ikarahisisha shughuli za kiusalama ndani ya Jimbo kwa sababu ni sehemu ambayo tunapatikana kwenye mpaka wetu wa Kenya, Uganda pamoja na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Waziri husika, hii barabara kwa kipindi hiki ambacho imetajwa kwenye Ilani iingizwe kwenye utekelezaji angalau wa kupatiwa lami ili wananchi wa maeneo yale tuweze kuinua uchumi wao. Pili kama nilivyosema itakuwa ni sehemu nzuri sasa pia ya kuboresha upande wa ulinzi na usalama ndani ya jimbo.

Mheshimiwa Spika, nne, nizungumzie kidogo kuhusiana na *TARURA.* Pamoja na mambo mazuri na makubwa aliyofanya Mheshimiwa Rais, ndani ya Jimbo langu mimi la Rorya kuna shida kubwa sana ya barabara, hizi barabara za kuunganisha kata na kata na tarafa na tarafa ambapo ziko chini ya *TARURA.* Hivi navyozungumza kuna

baadhi ya maeneo hayapitiki. Bado naamini kwa sababu ni mwanzo mzuri ambapo Serikali yetu ndiyo imeanza kufanya kazi chini ya Waziri Jafo, aone namna anavyoweza kutusaidia kwenye hii sekta hii ili angalau sasa tuendane na yale mazuri yaliyotajwa kwenye Ilani yetu hii na kwenye hotuba yetu ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie kuhusiana na wavuvi. Kwenye ukurasa wa 19, Mheshimiwa Rais amezungumza vizuri sana juu ya maboresho ya kodi na tozo mbalimbali zinazotolewa upande wa wenzetu wavuvi. Wabunge wote ambao wanatoka Kanda ya Ziwa watakuwa mashahidi, ilikuwa ni kazi kubwa sana kwa mwaka jana 2020 kupata kura kutoka kwa wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu Mheshimiwa Rais ametoa mwongozo mzuri sana kuhusiana na kupitia tozo zote ambazo zinawagusa wavuvi, Wizara kwanza ikae na hawa wavuvi wawape elimu na ipitie tozo hizo. Mimi nadhani si busara nzuri sana unapomkuta mvuvi anafanya biashara haramu ukamchomea mtumbwi wake kwa sababu wakati mwingine unakuta ule mtumbwi yeye mwenyewe siyo wa kwake, ameazima au amekodisha kutoka kwa mtu mwingine. Kwa hiyo, si tu kumrudisha yule mvuvi nyuma bali unamuathiri hata yule mmiliki halali wa ule mtumbwi.

Mheshimiwa Spika, wale wavuvi ndani ya jimbo na Kanda ya Ziwa wamekuwa wanalalamika kwa muda mrefu sana. Naiomba Wizara kipindi hiki turudi sasa tuone namna gani tunaweza tukapitia tozo lakini hata maboresho ya sheria ili angalau wale wenzetu wanaofanya shughuli za uvuvi wasiendelee kila siku kulalamika kwamba wanaonewa.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba inawezekana wapo kweli wanaofanya biashara haramu na hawa sina maana kwamba tunatakiwa tuwatetee lakini wako ambao wananunua na wanapewa risiti halali kutoka kwenye maduka halali na wanakwenda kufanya biashara ile ya uvuvi. Mvuvi anakutwa ziwani ana risiti zote, ana mtego au ana

nyenzo ile ile aliyonunua lakini wale watu wanamwambia kwamba wewe mtumbwi wako hauna uhalali wowote.

Mheshimiwa Spika, natamani sana Mheshimiwa Waziri kwenye kipengele hiki, maeneo yote ya Kanda ya Ziwa wakae wazungumze na hawa wavuvi na cha kwanza kabisa tutoe elimu. Kabla ya kumkamata uvuvi na kumpa kesi ya uhujumu uchumi, ningetamani sana tukae nao tuwaelimishe kwa sababu naamini mlinzi na mtetezi wa kwanza wa hizo maliasili ni mvuvi mwenyewe. Sisi Wabunge ambao tunatoka maeneo ya uvuvi, tuko tayari kutoa ushirikiano, wapewe elimu ili tuone namna gani tunanusuru hayo maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumze kidogo kuhusiana na rasilimali zetu. Moja kati ya kazi ya Mbunge ni pamoja na kutetea na kulinda maslahi ya wananchi na Serikali yetu kwa ujumla wake. Nilisema hili kwa sababu naamini Mheshimiwa Jafo ni mtendaji mzuri na anafanya kazi na anafuatilia sana utendaji na kulinda rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna gari letu sisi ndani ya Halmashauri ya Rorya. Tulipewa gari hili na Serikali yetu kwa upendo kabisa toka mwaka 2009 lakini leo limekuwa na mkanganyiko mkubwa sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jafari, Mbunge wa Rorya.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi napenda kuungana na wazungumzaji wa mwanzo pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninyi nyote kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri

anayoifanya. Siyo yeye peke yake isipokuwa na wasaidizi wake ambao wameanza kwa spidi kubwa sana. Hongereni sana Mawaziri wangu, hongereni sana viongozi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwangu mimi nikiisoma hotuba ile nzima, ndani yake naweza kusema ni semina elekezi au ni maelekezo yanayotosha kabisa kwa Mawaziri wangu hawa kuanza kufanya kazi kwa spidi kubwa kama ambavyo wameanza. Kwa sababu ndani yake kwa mfano kwenye kila eneo Mheshimiwa Rais amejitahidi kuchambua na kueleza juu ya tamaa yake ya kuona nchi inakwendaje, lakini pili jinsi gani tamaa ile inaweza ikafikiwa ili malengo yale ya kuwasaidia Watanzania walio wanyonge yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongea kidogo katika baadhi ya maeneo ambayo naamini kabisa tunao mchango au kutoa wito kwa Mawaziri wetu ili waweze kufanya kazi nzuri kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais. Kwa mfano, naamini katika eneo la Chalinze na Tanzania ambayo sasa wimbo wetu mkubwa ni maendeleo ya viwanda, viwanda haviwezi kufanikiwa bila kuwepo kwa umeme wa uhakika. Kazi nzuri inafanywa ya kuhakikisha kwamba umeme wetu katika bwawa la Mwalimu Nyerere unakamilika na mimi binafsi yangu nitumie nafasi hii kuipongeza sana Wizara hasa kwa jinsi ambavyo wanaendelea kusimamia ujenzi wa bwawa lile lakini pia kwa ma-*engineer* wetu ambao hata juzi tulishuhudia wenyewe wakieleza katika vyombo vya habari kwamba hawana shida yoyote na kwamba malipo yanapatikana ndani ya muda. Kwangu mimi hii ni ishara nzuri lakini ni wito wangu kwa Wizara kuhakikisha kwamba wanasimamia ili ule muda ulioelekezwa wa mradi kukamilika uweze kukamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi ujenzi wa bwawa hili siyo tu kwamba unaenda kutatua kero nyingi za kimaendeleo za watu, lakini msingi mkubwa ni kwenda kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana ili ile

sera yetu ya viwanda katika Tanzania iweze kufanikiwa. Kwa hiyo, wito wangu narudia tena kwa Waziri husika ajaribu kusimamia vizuri jambo hili ili wale wananchi wetu ambao sasa hivi wameanza kulalamika kupata matatizo ya kukatika umeme mara kwa mara, jambo hilo nalo liweze kuisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo katika hotuba yake Mheshimiwa Rais alieleza kwa uzuri zaidi jinsi ambavyo anatamani kuona maendeleo ya utalii yanapatikana Tanzania hii. Unakumbuka katika moja ya maeneo ambayo Mheshimiwa Rais aliyagusia ni kutatua migogoro iliyopo baina ya vijiji na hifadhi zetu kwa maana ya kusaidia kuongeza idadi ya watalii kwenye maeneo yetu. Moja ya maeneo hayo ni eneo la Mbiki au Wami Mbiki lakini pia Hifadhi yetu ya Saadani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Mkange kule Chalinze wanalalamika sana juu ya migogoro ambayo inayoendelea lakini ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni alieleza kwamba anatamani sana kuona migogoro hii inakwisha na katika kuhakikisha kwamba migogoro inakwisha, moja ya jambo kubwa ambalo alielekeza ni urasimishwaji wa maeneo ya vijiji hivyo ili sasa wananchi waondoke katika maeneo ya migogoro. Kwa hiyo, wito wangu kwa Mheshimiwa Waziri husika, jambo hili aendelee kuliangalia vizuri kwa sababu sisi ambao tunaamini kwamba Rais wetu ana nia njema ya kusaidia wananchi wake tusije tukamuangusha kwa sisi kushindwa kufikia malengo hayo. Mimi kama Mbunge nikiwa na viongozi wenzangu ndani ya halmashauri yetu, tutakupa ushirikiano mkubwa sana Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha kwamba nia ya Rais inafikiwa katika kiwango kikubwa na ikiwezekana kiwango chenye mafanikio makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa nia yake nzuri ya kutengeneza reli ya kisasa ya *SGR* ambayo inatoka Dar es Salaam inakwenda mpaka Kanda ya Magharibi lakini pili inafika mpaka nchi jirani. Kwangu mimi huu ni ukombozi mkubwa sana, kwanza kwa barabara zetu ambazo kwa

kipindi kikubwa sana Mawaziri wamekuwa wanalalamika lakini pia wewe mwenyewe unaweza kuwa shuhuda unapotoka kipande cha Chalinze kwenda Mlandizi kimeharibika sana kwa sababu ya uzito mkubwa wa magari yanayopita pale.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kwa kufanikiwa kukamilisha *SGR* hii maana yake mizigo mizito yote itaingia kwenye treni na itakwenda katika maeneo husika na hasa yale maeneo ambayo tumetengeza miradi ya kimkakati hasa ule mradi wa *dry port* wa pale Kwala na mwingine ule wa Kahama, maana yake ni kwamba tunakwenda kutatua tatizo kubwa ambalo linaendelea kukabili Watanzania wetu. Hivyo basi zile pesa ambazo zinatumika wakati mwingine kutengeneza barabara ambazo zinaharibika ndani ya muda ambapo hazipaswi kuharibika, kwa kweli nalo tutaliondoa tatizo hilo. Kwa hiyo, kwangu mimi ni kumpongeza pia Mheshimiwa Rais na kumuahidi kwamba tuko naye bega kwa bega kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika mapema iwezekanavyo na Watanzania waendelee kupata mafanikio ambayo yeye ameyakusudia.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Rais alieleza juu ya nia yake nzuri ya kuona jinsi gani tunaweza tukachukua hii idadi kubwa ya mifugo tuliyonayo ambayo inatupa nafasi ya pili kwa idadi ya mifugo Tanzania kuwa ni sehemu ya uchumi kuwawezesha wananchi wetu. Katika eneo letu sisi la Chalinze lakini pia katika maeneo ya Pwani ya Tanzania, wanyama kwa maana ya mifugo, mbuzi na kondoo ni wengi sana.

Mheshimiwa Spika, naamini nia hii ya dhati ya Mheshimiwa Rais ambayo ameeleza kwenye hotuba yake ambapo analenga kuhakikisha miaka mitano itakapomilika zaidi ya machinjio tisa za kisasa zitakuwa zimejengwa, kwa kweli naamini machinjio haya yatakapokamilika tutakuwa tumesaidia sana kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji inayoendelea. Naamini wafugaji wetu wanahitaji kupewa elimu na siyo kugeuzwa maadui katika maeneo yao ili waonekane kwamba ni wakosefu. Pamoja na hilo ni muhimu

pia kwa Wizara kuhakikisha kwamba wanawapelekea wafugaji hawa huduma muhimu zinazotakiwa katika maeneo yale. Kwa mfano, ujenzi wa mabwawa makubwa ili waache kusafiri na mifugo kwa umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naomba kugusia kwenye eneo la elimu. Asubuhi hapa umeibuka mjadala mkubwa sana juu ya Bodi ya Mikopo na mikopo inayotolewa kwa vijana wetu. Nikupongeze wewe pia kwa kuliona jambo hili lakini kwa kweli sisi kama Wabunge sijui kama wenzangu wanaliona hili lakini vijana wetu wengi wanakosa fursa ya kusoma vizuri kwa sababu ya kukosa mikopo ya Bodi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shida kubwa ambayo mimi naiona binafsi ni kwamba katika maeneo mengi sana, vijana hawa wanapokuwa katika *level* za chini, sisi Wabunge au kupitia wahisani mbalimbali tumekuwa tunawasaidia kuwasomesha katika shule zilizo nzuri. Kwa mfano, wako vijana ambao wamesoma katika shule hizi ambazo tunasema ni *private schools* katika *level* ya *form one* mpaka *form four* lakini vijana wale baada ya kufika chuo kikuu *either* wazazi wale wamekosa uwezo au wale *sponsor* wamefariki au wale wanaowawezesha nao hawana uwezo huo, kwa hiyo, wale vijana wanajikuta kwamba wananyimwa mikopo kwa sababu ya kukosa vigezo. Wito wangu kwa Wizara iangalie historia ya mwanafunzi huyu. Kigezo kisiwe amesoma wapi, kigezo kisiwe kwamba amewezeshwa na nani, waangalie kama uwezo huo anao ili kuweza kufikia malengo mazuri aliyoyaainisha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu Bwana Aweso, Waziri wa Maji kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Wana wa Chalinze wanakushukuru na wanaendelea kushukuru katika kazi kubwa unayoendelea kuifanya. Wito wao mmoja tu ni kwamba zile pampu zinazojengwa pale Msoga na Chamakweza hebu hakikisheni kwamba zinakamilika mapema iwezekanavyo ili lile tatizo la maji linalowakabili

wananchi wale liweze kuisha na liwe hadithi ambayo imepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naunga mkono hotuba zote za Mheshimiwa Rais, napenda kusema kwamba tuko pamoja naye na ajue kabisa kwamba anao vijana ambao wanamtakia mema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mbunge wa Chalinze. Nilishamtaja Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, sasa ajiandae Mheshimiwa Noah Lemburis. Mheshimiwa Silanga kwanza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo alitoa Bunge la Kumi na Moja na Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja na niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano katika vipindi vyake vyote viwili kwa kazi kubwa na nzuri na jinsi hotuba zake Mheshimiwa Rais alizokuwa akizitoa hapa Bungeni na kwenda kujibu mahitaji ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nataka kushauri Serikali yetu ya Awamu ya Tano, katika kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais alipokuwa akihutubia Bunge hili tukufu alisema anao mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba anajenga uwezo kwa Watanzania kuwa mabilionea lakini kuhakikisha kuwa wakulima wanaweza kupata mbegu zilizo na tija. Mambo haya yanaenda sambamba pamoja na kuwa na elimu bora lakini na kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara na wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumekuwa jinsi Serikali inavyofanya kazi zake vizuri lakini nataka kutoa ushauri wangu sehemu ya uwekezaji. Wazungumzaji wenzangu wamegusia suala zima la umeme, kuna changamoto ya umeme katika maeneo mbalimbali. Namwomba sana Waziri mwenye dhamana ya nishati kuhakikisha maeneo yaliyo na

changamoto ya umeme hususan kwa Mkoa wetu wa Simiyu na Mkoa wa Katavi, tumeona jitihada zinazofanywa na Wakuu wa Mikoa kwenye maeneo husika lakini changamoto ni kutokuwa na nishati ya kutosha kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Serikali kuhakikisha inapeleka pembejeo kwa wakulima kwa muda muafaka. Tunapozungumzia utajiri kwa Watanzania tunategemea kilimo, yaani kilimo cha pamba, kahawa, tumbaku, mahindi na kadhalika. Yote haya yakitekelezwa, naamini tutaendelea kutengeneza mabilionea wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asubuhi Mbunge wa Hai kauliza swali la msingi sana na Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumzia kwamba ushirika ni hiari kwa wananchi lakini jambo hili limekuwa na sintofahamu. Serikali inasema haiingilii ushirika, ni hiari lakini kuna maeneo mfano ni hivi sasa tunavyoendelea na Bunge hili, baadhi ya maeneo choroko zimeiva ambapo mama anapeleka choroko kilo mbili au tatu lakini kunakuwa na mpango wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia stakabadhi ghalani tuelewe kwamba sisi kama Watanzania hatuna uwezo wa kuhifadhi hicho chakula au kukitumia kwa pamoja, tunategemea nchi za nje kuichukua malighafi hiyo. Hivi sasa bei za choroko ni nzuri sana zinakwenda mpaka 1,500 lakini inaporudi kwenda kwenye stakabadhi ghalani, tunarudisha umaskini kwa vijana wetu ambao wanafanya kazi nzuri ya kusaidia jitihada za maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba jambo hilo liwekwe vizuri kwa sababu kumekuwa na mwingiliano mkubwa sana. Kuna watu wanaitwa *AMCOS,* kwanza hawana maghala lakini wanasema wewe mfanyabiashara nunua sisi tunaomba utuchangie shilingi 50 kwa ajili ya maendeleo ya ushirika wetu. Ni jambo ambalo kwa kweli lisipoangaliwa linaweza likatuletea changamoto kubwa katika utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naliona, katika mitaala yetu kwenye elimu zetu za juu, tumekuwa na vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu lakini hawana mahali pa kwenda. Jambo hili ni muhimu sana likatazamwa kuanzia shuleni kuanza kuwajengea uwezo wa kujitegemea vijana wetu. Maana yake ni kwamba, vijana wetu wanapomaliza elimu ya vyuo vikuu changamoto kubwa wakitegemea wataenda kuajiriwa na ajira inapokosekana inabaki ni manung'uniko ndani ya mioyo ya vijana wetu hawa na ile elimu inakuwa haina maana kwa kuipata yule kijana, lakini ina maana akianza kujengewa uwezo akiwa darasani na hususan mwaka wa mwisho, akipewa elimu ya ujasiriamali inaweza ikatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niendelee tu kuipongeza Serikali kwa miradi mikubwa ambayo inaendelea kuifanya, lakini niiombe Serikali, imewekeza kwenye hospitali zetu za wilaya, hususan Wilaya yangu ya Itilima, jimbo jipya. Ningeomba sana sasa kupeleka vifaa tiba, vitendea kazi na wataalam kwenye maeneo hayo, ili kusudi sasa haya yote tunayoyazungumza yaendane sambamba na utekelezaji wa hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima la barabara zetu hususan kwenye maeneo ya *TARURA.* Yako maeneo ambayo ni ya kiuchumi katika vijiji vyetu, lakini barabara hizo hazipitiki, lakini na bajeti ya *TARURA* tunaipitisha pamoja ni kidogo, lakini maamuzi yale yanachukua muda mrefu sana kufanya utekelezaji wa hayo majukumu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana kwa haya niliyoyazungumza basi Serikali iyachukue na kuyafanyia kazi. Naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lembris, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nichukue nafasi hii pia kukupongeza sana wewe kwa jinsi

ambavyo unaongoza Bunge hili, lakini nichukue nafasi hii sana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amewasilisha hotuba yake na jinsi ambavyo amehakikisha ametekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, hasa kuanzia 2015 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameonesha umahiri mkubwa sana katika jambo hili. Ukiangalia jinsi ambavyo ameanza katika mwaka 2015 hadi kufikia 2020, watu walikuwa wameanza kusema labda ni nguvu ya soda, lakini kwa kweli, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, amefanya kazi kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na wasaidizi wake kwa kweli, hatuna sababu ya kutokuwapongeza, lakini katika kupongeza huko nakumbuka maneno yako ulikuwa siku moja umesema, Spika wa Bunge la Kenya alisema Mtanzania akisimama, anapongeza halafu anakaa chini, lakini utamaduni wetu Watanzania ni kupongeza. Mtu wa Kenya akienda dukani anasema nataka chumvi hasemi naomba, kama sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi, niende kuchangia kwenye maeneo mawili matatu, kama wenzangu ambavyo wamechangia. Naenda kwenye afya; Wizara ya Afya imefanya kazi kubwa sana. Katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi tunaishukuru Serikali sana kwa kutuletea fedha kwenye vituo vya afya. Kituo cha Afya cha Nduruma kimepata milioni 500, Kituo cha Mbuyuni milioni 400, Kituo cha Musa kimepata milioni 200; hii ni kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais katika kipindi chake ameboresha afya, amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kuna changamoto kubwa katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Zahanati nyingi tumewahamasisha wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi kwa ajili ya kujenga kwa dhana ile ya kila kata, kila kijiji kujenga zahanati kufikia lenta, kwa

maana ya maboma, ili Serikali iweze kumalizia. Naomba kuishauri Serikali, hasa Wizara ya Afya, ni lini sasa itamalizia hayo maboma ambayo wananchi wamejenga katika kuwahamasisha, ili basi lile lengo la kila kijiji kuwa na zahanati, ili hizi zahanati zikamilike?

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu kuna zahanati nyingi sana kama 11 katika Vijiji vya Ilkerin, Bwawani, Kigongoni kule na kadhalika. Hii itasaidia sana kukamilisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kama Mheshimiwa Rais wetu anavyojali katika masuala ya afya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Wizara ya afya kwamba, badala ya kuwapa wazee kitambulisho, ni kwa nini sasa Serikali isije kwenye sera yake irekebishe wazee wapewe bima ya afya kama watu wengine. Kwa sababu, katika kupewa vitambulisho hawapati huduma ipasavyo. Hilo nalo naomba Wizara hiyo iliangalie.

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa Madaktari; hili nalo naomba Serikali ijaribu kuangalia kwa sababu, unakuta Nesi katika baadhi ya maeneo, Serikali imejitahidi sana, lakini bado kuna upungufu katika maeneo machache. Ningeomba Serikali irudie tena kuangalia maeneo hayo kwa ajili ya kupatikana kwa Madaktari katika vituo vyetu vya afya.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara. Serikali imejitahidi sana, nchi hii ni kubwa, lakini Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba, imeunganisha wilaya na wilaya, mikoa na mikoa, lakini naomba kuna ahadi ambazo Mheshimkwa Rais pamoja na viongozi wengine wameweza kutoa katika ziara na hasa wakati wa kampeni, basi katika bajeti ijayo barabara hizo zikumbukwe. Kwenye jimbo langu kuna barabara ambayo imefanyiwa tathmini kwa mfano barabara ya Arusha – Mirongoine – Tera kwenda Kongwa. Naomba hii barabara katika bajeti hii isisahaulike.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ambayo tumeahidiwa pia na Mheshimiwa Rais, Barabara ya Mianzini – Timbolo kutokea Sambasha kwenda Ngaramtoni, hiyo ni

barabara ya kilometa 18, Mheshimiwa Rais aliahidi kwa kiwango cha lami. Naomba Wizara husika isisahau kwenye bajeti hii; vile vile barabara ya kwenda Hospitali ya Oturumet, Hospitali ya Wilaya, kilometa tatu; na barabara ya kwenda Hospitali ya Seliani, kilometa tatu. Hayo ni maeneo ya huduma ambayo wananchi hawa wanahitaji kwa ajili ya kupata huduma bora. Pamoja na hayo tunaendelea kuipongeza Serikali kwa sababu, kwa kweli inajitahidi kwa kadiri ilivyoweza kuwafikia wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye suala la ajira; vijana wetu wengi wanakosa ajira, lakini Serikali imejitahidi kuimarisha sekta binafsi na hata ndani ya Serikali katika kuajiri vijana wetu. Ushauri wangu kuna Mfuko ule wa Akinamama na Vijana na watu Wenye Ulemavu; naishauri Serikali iangalie hiyo Sera ya Mfuko huo kwa sababu, utakuta vijana kuanzia miaka 18 mpaka 35 ndio wanaostahili kupata huo mkopo kwenye halmashauri zetu, lakini ukienda mbali zaidi ukiangalia watu wanaoweza kufanya biashara vizuri ni kuanzia miaka 18 mpaka angalau 40 mpaka 45.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali iangalie hiyo sera, ili kwa sababu ya ukosefu wa ajira kuanzia 18 mpaka 45 waweze kuingizwa kwenye sera ili waweze kupata hiyo mikopo. Hata hivyo, tunaendelea kuishukuru Serikali kwa sababu, imeondoa riba kwenye Mfuko huo na sasa wengi wananufaika isipokuwa upande wa vijana kuna changamoto kidogo kwa sababu ya hayo mambo magumu. Naomba pia, kuishauri Serikali kuangalia uanzishwaji wa vokundi kuanzia watu watano mpaka na kuendelea. Kwa sasa hivi ni watu 10, wananchi bado wanaona kidogo inawawia vigumu kuanzisha hivyo vikundi kuanzia watu 10 na kuendelea, lakini wakati ule ilikuwa watu watano angalau wananchi wanapata kujiunga vizuri na kuanzisha vikundi kwa ajili ya ujasiriamali. Nina uhakika eneo hili likiboreshwa suala la upungufu wa ajira ambalo kila siku sisi Wabunge na hasa mimi ninavyozungumzia kwenye jimbo langu, kila siku wananchi wananchi wanasema tutafutie ajira. Eneo hili tukiliboresha vizuri nadhani kwamba, wananchi wetu watapata ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la *NIDA;* Mheshimiwa Rais katika hotuba yake alisema ataboresha vitambulisho vya Wamachinga na baadae viwe kama vya *NIDA,* lakini naomba watu wanaohusika na *NIDA* hasa Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa kweli, wananchi wanateseka sana katika maeneo mbalimbali kupata huduma kwa sababu ya ukosefu wa vitambulisho hivyo vya Taifa. Hebu iangaliwe kwamba, kuna nini hasa kinachopelekea mpaka wananchi hawawezi kupata vitambulisho kwa wakati, ili waweze kupata huduma. Hasa ukizingatia kwamba, kitambulisho cha Taifa kwa sasa wananchi walio wengi wanahitajika kuwa nacho kwa ajili ya kupata huduma katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala la maji; kwanza niishukuru Serikali kwa kutupatia mradi mkubwa wa maji wa bilioni 500 katika Jiji la Arusha ambao unahudumia hasa katika jimbo langu na maji hayo yametoka kwenye jimbo langu. Mheshimiwa Rais alikuja kuzindua mradi huo mkubwa kwa kweli, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ameonesha ni kiongozi ambaye watu. Ninachoweza tu kusema hapa naomba sasa niikumbushe Wizara iangalie yale maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ameahidi, ili maji yaweze kuwafikia waweze kupata. Kwa mfano maeneo yale ya Floraid, Lemong'o, Lemanda, kule Ngutukoit, Losinoni Juu, Losinoni Kati mpaka huku chini kuja Oldonyosambu. Naamini Wizara itajitahidi kwa jinsi ambavyo inamuunga Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, suala la ulinzi na usalama wa wananchi wetu. Kama tunavyojua Serikali yoyote duniani ni Serikali ambayo inahakikisha wananchi wake wanaishi kwa salama na amani. Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli imefanya kazi kubwa sana ukizingatia katika kipindi hiki chote cha miaka mitano uhalifu umepungua kwa kiwango kikubwa mno.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo kidogo la kushirikiana. Nimwombe Waziri anayehusika wa Ulinzi, kuna mgogoro mkubwa sana na Waziri wa Maliasili, kuna mgogoro ambao

haujakaa vizuri kwenye jimbo langu. Ningemwomba Waziri angefika kule kwenye Msitu wa Meru. Wananchi kule...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Noah Lembris. Sasa ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai nikaweza kuwepo Bungeni leo. Naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Same Mashariki kwa unyenyekevu mkubwa kwa jinsi ambavyo walifanya uchaguzi mzuri sana na kuhakikisha wananirejeshea Jimbo langu la Same Mashariki. Nilishinda kwa kishindo tena kwa haki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais kwa mara ya kwanza amesimama imara akahakikisha nchi yetu inafanya uchaguzi kwa pesa zake za ndani. Nafikiri wote tunaoelewa uchaguzi tumekaa kwenye uchaguzi muda mrefu, siku zote tumekuwa tunabebwa na mataifa makubwa, lakini Mheshimiwa Rais kipindi hiki alisimama imara sana akaiheshimisha nchi yetu tukafanya uchaguzi kwa pesa zetu wenyewe. Waheshimiwa Wabunge naomba hili tulichukue kwa uzito sana na tuone kwamba, Rais ametukomboa kwa kitu kikubwa sana. Vile vile nimpongeze pia Rais alifanya kampeni za kutosha. Alizunguka nchi na aliomba kura na akashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nirudi sasa kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Rais ametoa hotuba siku ya kwanza hapa Bungeni, ilikuwa ni hotuba nzito sana. Namuunga mkono katika *area* tatu ambazo nimeona nizichague; kwanza katika viwanda, pili katika barabara na tatu nitakuja kwenye afya.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote inakua vizuri zaidi inapokuwa na viwanda vya nguvu. Mimi naomba nirudi kwenye Jimbo la Same Mashariki, Jimbo la Same Mashariki sisi tunalima tangawizi kwa muda mrefu. Kwa muda mrefu sana tunalima tangawizi na tumejenga kiwanda cha tangawizi, mnaokumbuka tangu nimeanza kuingia bungeni hapa nazungumzia tangawizi nikasimama na wale wananchi imara tukajenga kiwanda cha tangawizi.

Mheshimiwa Spika, nikiri kile kiwanda kilikuwa ni dhaifu, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Mhagama amekuja ziara kwenye jimbo langu akaja mlimani Mamba Miamba kukiona kiwanda kile. Amekuja nikajua ni Serikali imekuja kuona kile kiwanda. Kiwanda kile yeye mwenyewe amesimama imara pamoja na taasisi yake ya *PSSSF,* ambao wameingia ubia na sisi wananchi tunaolima tangawizi sasa pale Mamba Miamba, sasa pale Mamba Miamba tunakuwa na kiwanda kikubwa cha tangawizi katika Tanzania kwa sababu *PSSSF* wameamua kuingiza fedha nyingi sana kuwaunga wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wao wamechukua asilimia 60 sisi tumechukua asilimia 40, lakini ndugu zangu Wabunge hicho ni kitu kikubwa sana. Ina maana kiwanda kile ambacho kitakuwa kikubwa wananchi wangu wataondoka katika umaskini. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, namshukuru mama Jenista Mhagama mno mno, alikuja jimboni kwangu, nilipata furaha sana ambavyo aliwafanya wananchi wangu wakafurahi. Naipongeza sana Serikali kujali viwanda kwa wananchi. Nimeanza tu kusema kidogo, nitakavyokuwa niko hapa ndani nitaongea sana kuhusu hiki kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono suala la ujenzi wa barabara kwenye nchi yetu. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuangalieni tulitoka wapi tuko wapi sasa hivi. Tulikuwa kwenye barabara kwenye miji mikuu, ukiangalia Dar es Salaam, ukienda Arusha, ukija Moshi, ukija Dodoma, barabara zilikuwa za kawaida mno, lakini mimi nikienda Dar es Salaam na dereva wangu kwa sababu, mimi niseme ukweli mimi naishi Dodoma, kama sipo Dodoma niko Same

Mashariki, Dar es Salaam mimi ni mgeni; tukienda na dereva wangu Dar es Salaam sasa hivi inabidi tupate dereva wa kuingia na sisi mjini. Dar es Salaam Rais amesimama imara mno, ameisimamia nchi yetu imara sana. Sasa hivi Tanzania katika Afrika Mashariki, sio kwamba tujisifu tuseme ukweli, tunaongoza upande wa barabara.

Mheshimiwa Spika, tunaongoza upande wa barabara, lakini naomba nizungumze kama mama. Mama sisi tunapokuwa na watoto unawaangalia Watoto wako sana, unamwangalia mtoto wako wa kwanza, unaangalia wa pili, unaangalia wa tatu, sisi tuliozaa zaidi unaangalia wa nne. Kila mtu anapozaliwa, anapoumbwa na Mwenyezi Mungu akija duniani ana kitu amepewa, ana kitu Mungu amempa cha kwake kwamba, huyu nampa kitu fulani. Tumshukuru Mungu amempa Rais wetu silika ya kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais Magufuli pamoja na usomi wake, amesoma *mathematics* na kadhalika lakini nadni ya damu yake ni mjenzi, anajenga barabara. Mimi tangu nimekuwa bungeni hapa nimekuwa nae, hiki ni kipindi changu cha tano, yeye ni Waziri wa ujenzi, Waziri wa Ujenzi, sasa ni Rais anaijenga nchi mpaka mimi na Mheshimiwa Mama Sitta tumekaa tukafikiria hivi akiondoka tutafanya nini, lakini Mungu atatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi imejengwa barabara. Mimi najivuna sasa hivi nikiona hata Dodoma yangu inavyofanana. Dodoma inajengwa na Rais Magufuli mno na nampongeza kwa sababu, mume wangu siku moja alisema aah, hivi kumbe kweli hata nikifa kesho Dodoma imekuwa Makao Makuu, alimshukuru Mungu, lakini Malecela anasifu sana, anamsifu Rais mno, naomba umfikishie *message,* jinsi anavyojenga barabara za Dodoma.

Mheshimiwa Spika, sasa narudi nikwambie hivi *TARURA.* Sisi Wabunge wengi wa majimbo tunaitegemea *TARURA* na mimi niko Kamati ya Miundombinu, kuna mgawo wa fedha za kujenga barabara upo 70 kwa 30. *TANROADS*

anapewa 70; *TARURA* anapewa 30, mimi naona *TARURA* aongezewe pesa. Waheshimiwa Wabunge wa majimbo simameni imara sana *TARURA* aongezewe pesa ili wananchi wetu nao wapate barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshukuru Serikalini. Serikali imeona majiji makubwa, sasa tunaomba Serikali mrudi mtuangalie na sisi ambao tuko vijijini. Vijijini barabara zina hali mbaya sana. Sisi ambao majimbo yetu yako kwenye milima tuna shida kubwa ya barabara, tuna tabu sana ya barabara. Nasema ukweli lazima Wabunge bajeti inayokuja tusimame imara *TARURA* apewe pesa. Ule mgawo tunaoambiwa ni mgawo wa kisayansi wa 70 kwa 30 *TARURA* anapata pesa kidogo, Serikali itafute chanzo kingine cha kumpa *TARURA* pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye afya sasa; namuunga Mheshimiwa Rais sana mkono kwa jinsi alivyosimama imara kujenga vituo vya afya. Amesimama imara kujenga vituo vya afya. Sasa ahakikishe vituo vya afya vinatoa huduma kikamilifu, Madaktari watoshe na vyombo.

Mheshimiwa Spika, sasa hapo lazima nirudi kwenye Jimbo langu, mimi nina tarafa tatu. Tarafa ya Ndungu ina kituo cha afya kimoja, nimetoka kuongea na Waziri wa Afya pale. Tarafa zangu mbili za milimani zote hazina vituo vya afya. Rais alipokuja Same nilimlilia nikamwambia wananchi wanakufa. Tarafa ya Gonja kuna kituo cha afya lakini ni cha KKKT ni biashara, wananchi hawana uwezo wa kulipia zile gharama pale. Tarafa ya Mamba Vunta kuna kituo cha afya cha Katoliki ni biashara. Nimekwenda kumlilia Mheshimiwa Waziri sasa hivi pale, nimempigia magoti aje aone jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii ya hotuba za Mheshimiwa Rais, naipongeza sana Serikali inafanya kazi nzuri lakini naomba mtuangalie na sisi tunaotoka vijijini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, huyu ndiye Anne Kilango Malecela. Tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Neema Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mezani ya hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Napenda kujielekeza katika sekta ya kilimo na hivyo nitaendelea kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake na naomba nifanye rejea kwenye ukurasa wa 25 alisema kwamba: "*kwenye miaka mitano iliyopita tumefuta tozo 168 ambapo 114 zilihusu kilimo, mifugo na uvuvi na 54 za biashara. Tutaendelea na hatua hizo.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kufanikisha hili ambapo lengo kuu naamini ni kuimarisha uwekezaji na hivyo hivyo punguzo hizi zinaweza kuimarisha na kunufaisha wakulima wadogo. Hivyo napenda kuishauri Serikali kuwa ni muhimu sasa kufanya tathmini ili tuweze kujiridhisha punguzo za tozo hizi zote kama zinanufaisha wakulima wadogo kama ambavyo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali iagize wadau wote kufanya *impact assessment* ya tozo zote ambazo tumetoa, maana kwa uzoefu wangu inaonekana kwamba saa nyingine tozo hizi kunakuwa hakuna *trickle-down effect* ya kufika kwa wakulima wadogo ipasavyo. Mimi naamini kwamba uimarishaji wa mazingira ya ufanyaji biashara unatakiwa uende sambamba na unufaikaji wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake kwenye ukurasa 26 naomba kunukuu, alisema: "*Kwa msingi huo kwenye kilimo mathalani tunakusudia kuongeza tija na kufanya kilimo chetu kuwa cha*

*kibiashara. Lengo ni kujihakikishia usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwandani na pia kupata ziada ya kuuza nje. Ili kufanikisha hayo, tutahakikisha pembejeo na zana bora za kilimo ikiwemo mbegu, mbolea, viuatilifu/ dawa na matrekta vinapatikana kwa uhakika na gharama nafuu.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya kwa miaka mitano iliyopita. Hotuba ya Mheshimiwa Rais imesisitiza yale ambayo yameandikwa kwenye Ilani ya chama tawala, Chama cha Mapinduzi kwenye kifungu 35 – 46. Hivyo ili tuweze kufanikisha haya kwa kasi ambayo inatakiwa ningependa kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa tujikite katika uzalishaji wa aina mbalimbali za mbegu maana hivi sasa ukienda kwenye duka la mbegu utakuta 80% ya mbegu hizo zimetoka nje ya nchi na hivyo Tanzania tunakosa soko kubwa la uzalishaji wa mbegu. Aidha, naishauri Serikali iweke kipaumbele cha kujengea uwezo taasisi zetu za ndani na za binafsi za ithibati (*Local Certification Boardies*). Kwa kufanya hivi, tutaweza kufanikisha mbegu ambazo tunazizalisha ndani ya Tanzania nazo ziweze pia kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo jambo langu la tatu, nakubaliana na mapendekezo yaliyo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuhusu Wizara ya Kilimo kuwa na bodi za mazao na taasisi ambazo zinahitaji kupitiwa upya kimuundo ili ikiwezekana kuwe na taasisi chache zitakazoongeza ufanisi na kuimarisha usimamizi wa sekta hii. Nimesema hivi kwa sababu kwa jinsi ilivyo sasa wingi wa hizi bodi za mazao na taasisi unaleta mkanganyiko mkubwa kwenye sekta hivyo unakinzana na dhana nzima ya kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwisho niapenda kutoa wito kwa wadau wa sekta ya kilimo kuwa mstari wa mbele kuhamasisha uzalishaji na ulaji wa vyakula vyenye viini lishe vingi ili kuungana na jitihada za Serikali za kutokomeza

udumavu na utapiamlo kwa ujumla. Kama ambavyo tunafahamu Waheshimiwa Wabunge Tanzania 32% ya watoto chini ya umri wa miaka mitano wamedumaa, kwa maana hiyo katika kila watoto 100 watoto 32 wamedumaa. Cha kushangaza zaidi mikoa inayoongoza kwa udumavu ni mikoa ambavyo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula (*food basket*). Ndiyo maana nimesema tutoe wito kwa wadau hawa pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kibiashara pia wahamasishe uzalishaji na ulaji wa mazao yenye viini lishe vingi ambayo imo kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru tena kwa fursa hii ya kuchangia hoja iliyo mezani na naunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Neema Lugangira kwa matumizi mazuri sana ya muda. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninashukuru sasa umetaja vizuri jina langu ni jepesi tu Saashisha Elinikyo Mafuwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ndiyo nimepata nafasi ya kuchangia na kupata fursa ya kuweza kusema neno la shukrani kwa ajili ya wananchi wa Hai walionipa heshima kubwa sana ya kunichagua kuwa Mbunge wa Hai. Pia wametupa heshima kubwa sana kumchagua Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu kwa kura nyingi za kutosha 92%, lakini wametuchagulia madiwani wa kutosha sana. Nawashukuru sana wananchi wa Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa kwenye Bunge lako Tukufu. Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais inatoa mwanga na mwelekeo wa Serikali kwa kipindi cha miaka mitano. Ukisoma kitabu hiki kinajibu matarajio ya wananchi wa Jimbo la Hai na wananchi wa Tanzania. Hii ni ishara kwamba

Mheshimiwa Rais ni zawadi ya Watanzania, mambo anayoyafanya kwa nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mambo ambayo katika historia ya nchi hii hayatasahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo sababu ya kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetuletea zawadi ya Dkt. John Pombe Magufuli. Miradi mikubwa inayotekelezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyopita na hii ambayo tunaandaliwa tena ya miaka mingine mitano inaonyesha kwa kweli Mwenyezi Mungu ametupa zawadi ya Rais mwema. Nichukue nafasi hii kuendelea kumwombea Mungu ampe afya njema ili haya yote yaliyoandikwa na yaliyosomwa kwenye hotuba yake yaweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo limenigusa sana ni habari ya kilimo. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais amesema sasa tutaenda kupandisha thamani ya mazao kwenye kilimo ambacho tunafanya. Kwetu kule Hai 78% tunategemea shughuli za kilimo. Nashukuru sana hotuba hii miongoni mwa mazao ya kimkakati yaliyotajwa, zao la kahawa limetajwa kama zao la taifa la mkakati.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kidogo, kule kwetu Hai zao la kahawa limepunguza tija kidogo kwa sababu ya utitiri wa vyama vingi vilivyopo kabla ya zao hili kufika sokoni. Pia zao hili limepunguza uzalishaji kwa sababu ya kukosekana kwa maji ya kumwagilia.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuunga mkono hoja hii na kuiomba Serikali ihakikishe tunapata maji ya kumwagilia ili tuweze kufufua zao hili la kahawa. Ikumbukwe kwamba mbegu za kahawa au chanzo na utafiti wa kahawa unafanyika ndani ya Jimbo la Hai. Taasisi ya Uchunguzi wa Zao la Kahawa (TaCRI) iko ndani ya Jimbo la Hai. Nashangaa utaona maeneo mengine zao hili linapandwa lakini pale Hai limefifia. Niombe sana Serikali yangu sikivu, tumeomba na nimepeleka ombi maalum la kupatiwa mito ya umwagiliaji mitano inayopatikana ndani

ya Jimbo la Hai. Tukipata mifereji hii mitano itatusaidia sana kufufua zao hili la kahawa.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hilo tu, Jimbo la Hai Mungu ametujalia tunavyo vyanzo vikubwa sana vya maji lakini tatizo ni namna ya kuvifikisha kwa wananchi. Tunayo ardhi nzuri ya kilimo lakini tatizo ni namna gani tuitumie.

Mheshimiwa Spika, nilianza kwa kuomba wenzetu wa TARI Mlingano wafanye utafiti wa udongo, kazi ambayo imekwisha kukamilika. Kwa hiyo, kazi iliyobaki ni kuiomba Serikali iweze kutuletea maji kwa ajili ya kumwagilia maeneo haya mazuri.

Mheshimiwa Spika, niseme kilimo cha mazao ya mbogamboga katika Jimbo la Hai ni biashara ambayo Serikali tukiwekeza tutakusanya kodi nyingi sana, tunaweza tukafanana na wanaochimba madini. Sasa hivi ukiangalia mazao mengi yanaenda nchi nyingine sisi Hai tunazalisha lakini wanapeleka nchi nyingine kwa ajili ya kwenda kuongezewa thamani na thamani yanayoongezewa ni kufanyiwa *packing* tu. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa kule Hai tumekubaliana kuwa na ari mpya ya kilimo na viwanda, tupatiwe msaada wa *packing,* baada ya wananchi kulima tuweze kuyaongezea thamani kwa kufanya *packing.* Bahati nzuri tunao uwanja wa ndege tutaweza kusafirisha nje ya nchi ambapo kuna mahitaji makubwa ya chakula cha ziada kinachozalishwa katika Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imezungumza pia habari ya kuendelea kujenga miradi ya maji. Nashukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu kwa kutuletea Naibu Waziri wa Maji pale Hai. Tulikuwa na tatizo kubwa sana la maji; moja katika Jimbo letu la Hai huduma ya maji inasimamiwa na Bodi za Maji kulikuwa na shida kubwa sana. Nashukuru Naibu Spika alifika pale dada yangu akafanya kazi kubwa na nzuri ya kurekebisha matatizo yaliyokuwepo kule. Kwenye bodi hizi kulikuwa na shida amezinyoosha vizuri mno.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nasimama hapa kushukuru kwamba tulikuwa na mradi wetu wa Kikafu ambao ulishathaminiwa siku nyingi wa shilingi bilioni 3.6. Nimepewa taarifa tayari Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli imetupelekea shilingi milioni 500 kwa ajili ya mradi huo, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kule Lundugai tumepata shilingi milioni 200, hii ndiyo raha ya kuchagua CCM. Nataka niwaambie wananchi wa Hai walifanya maamuzi sahihi kabisa ya kuchagua Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kule Romu tumepata shilingi milioni 200. Naomba sana Serikali mradi huu wa Kikafu Chini utatusaidia kuondoa tatizo la maji. Pale Hai tunashida kubwa ya maji ya kunywa ukanda huu wa tambarare. Boma Ng'ombe, Mnadani, Weruweru, *KIA* hawana maji. Naomba sana Serikali fedha hizi shilingi bilioni 3.6 zikija kwa wingi zitatusaidia kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nashukuru sana Serikali kulikuwa na mradi wa visima 18 vilikuwa vinapeleka maji Arusha imesema sasa kwa kuheshimu Sera ya Maji ni vizuri pia Hai baadhi ya maji yakabaki pale. Nashukuru sana kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mchangiaji mwenzangu mama Anna Kilango Malecela, kwa kweli tunatakiwa kuongezea *TARURA* fedha ili waweze kufanya kazi. Miundombinu imeelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais lakini bado tunayo changamoto na mimi kule kwenye Jimbo la Hai hali si njema kwa habari ya barabara. Bado hatujafikia kiwango cha kukidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hapa niombe Mheshimiwa Waziri anayehusika, tunayo barabara moja ambayo inalalamikiwa sana sana na wakati Mheshimiwa Rais ananiombea kura pale aliwaambia nileteeni Saashisha hii barabara nitaitengeneza, ni kilometa 13. Barabara hii iliitwa barabara ya ng'ombe,

jambo hili linawachukiza sana wananchi kwamba ile barabara tuliambiwa ni ya ng'ombe. Sasa hii barabara ni ya watu, tunaomba barabara ile iweze kuwekwa lami, ni kilometa 13 tu kuanzia mferejini kupita *TaCRI*, Lyamungo kwenda kutokea Makoa.

Mheshimiwa Spika, lakini tunayo barabara nyingine ambayo hata ninyi mkishuka kwenye ndege pale KIA mkiwa mnaenda Moshi ni rahisi, inakuwa ni barabara mchepuko inaweza kutumika kilometa 25 tu inaanzia Boma ya Ng'ombe kwenda *TPC*. Ziko barabara nyingi ambazo kwa kweli kama *TARURA* itaongezewa uwezo wataweza kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumepeleka maombi maalum ya kupandisha hadhi barabara tano zilizoko ndani ya Jimbo la Hai kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS.* Nashukuru sana kikao cha *RCC* kilipitisha barabara hii. Naiomba Serikali iongeze spidi kwenye mchakato huo ili barabara hizi ziweze kuhudumiwa chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ni kuhusu umwagiliaji. Naomba sana, kwa kuwa nimeeleza hapo awali Jimbo la Hai linaweza kutumika kukusanya kodi nyingi kwenye mazao haya miradi hii ya umwagiliaji iweze kufanyiwa kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini iko changamoto, niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na TAMISEMI tunayo miradi iliyoko kwenye kata yetu ya Weruweru na pale Kikafu Chini, ni Jumapili tu nimetoka kwenda kutembelea miradi hii, iko shida. Serikali imeleta fedha pale shilingi milioni 91 lakini ule mradi umetulia, hakuna kinachoendelea. Tayari Serikali imeshaweka fedha ziko shilingi milioni 700 kwenye Kata yetu ya Weruweru kule Mijengweni, Serikali imeweka mashine zimefungiwa kule, naomba sana Serikali itoe pesa ili miradi hii iweze kukamilika wananchi waweze kunufaika. Hii ni miradi ya muda mrefu, Kikafu Chini ni miaka nane lakini huu mwingine wa Mijengweni ni miaka 15 mashine zimefungiwa

kule na bado zina uwezo wa kufanya kazi. Naomba sana Serikali itusaidie ili kuweza kukidhi matarajio na shauku kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kuweza kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa kwenye hotuba hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kupata umeme kwenye vijiji vyote. Wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kwamba maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme wa *REA* yaweze kufikiwa. Niombe sana kwa kuwa Serikali imeshafanya kwa kiwango cha 84% hii asilimia iliyobaki Mheshimiwa Waziri ni ndogo sana. Wewe unafahamu na asubuhi nimezungumza na wewe kwamba yule mkandarasi pale Hai anatupa shida. Mimi naomba sasa Serikali mfanye maamuzi ili ile ahadi ya Mheshimiwa Rais iweze kutokea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza?

**SPIKA:** Tayari muda wako umeisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, haya naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na utafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi siku hii ya leo nina afya tele. Pia nishukuru chama changu cha CCM kwa kunipa fursa ya kugombea kwenye Jimbo lile la Vunjo ambapo wananchi wake walitupa kura kwa wingi na CCM ikashinda kwa kishindo, kwa hiyo, CCM oyee.

**WABUNGE FULANI:** Oyee.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, niseme hivi, mimi niliyesoma hivi vitabu vitatu nasema ni kitabu kimoja ambacho bado kinaandikwa bado hakijaisha na naamini kwamba itakapofika mwezi Juni, 2025 tutaona *chapter* ya nne na pengine ikimpendeza Mheshimiwa Rais tutaona na *chapter* ya tano itakayokuwa inatuonesha kwamba dira ya 2025 kwenda 2050 itakuwaje lakini ni kitabu kitamu na utamu wake ni kwa sababu una *happy ending,* unaishia pazuri.

Mheshimiwa Spika, niliposoma nimeona kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa Novemba 2015 anaanza na mambo magumu sana ya kuunda utawala bora na kutafuta uongozi ambao ungeweza ukapigana na mmomonyoko wa maadili ndani ya Serikali, kurudisha nidhamu na kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali yanakusanywa vizuri na yanatumiwa vizuri. Naamini kwamba kwa kile alichokifanya kuunda uongozi ambao aliweza kufanya nao kazi lakini pia akawa anatumbuatumbua mpaka tukaona mambo yamesimama vizuri ndiyo sababu tunasema kwamba kusema kweli ni fundisho kubwa linalosema kwamba maendeleo ya Afrika, maendeleo ya Tanzania yanatokana na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini uongozi bora siyo viongozi bora ni kiongozi mmoja ambaye anajitokeza, *the leader,* ana *make a big difference* katika mambo yote yanayofanyika kwenye nchi au kwenye kampuni inakuwa hivyo hivyo, kama ukiwa na kiongozi bora utaona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru na nasema kwamba kusema kweli ukisoma kitabu hiki ambacho kinaandikwa hakijaisha natumaini utaona wazi kwamba tumempata kiongozi ambaye anastahili sifa kwa kila Mtanzania. Hata mtiririko wa namna anavyoelezea dira na mkakati wake na malengo yake na *milestone* za kufikia na namna ya kutathmini utaona wazi kwamba ni kitu ambacho kinaeleweka kwa kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaona kitu kama hicho hata ukimuuliza bibi yangu pale mgombani kule Moshi wewe ni

nani? Anakwambia mimi ni Mtanzania naenda kwenye uchumi wa kati, kipato cha kati na baadaye tutafika kwenye kipato cha juu. Kwa hiyo, kila mtu anaelewa ni kitu gani. Lengo kuu la nchi ni kuinua kipato cha Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake aliyotupa kwenye ufunguzi anasema wazi kwamba sasa amejua kutakuwa na miundombinu lakini hailiwi, lazima sasa tuweze kuwezesha wananchi wetu na wale tunaowaongoza kuongeza kipato chao, wajasiriamali kwa kuwawezesha kupata mikopo na kadhalika ili waweze kuinua kipato chao. Kwa hiyo, nasema kwamba kwa *logic* ya hiki kitabu kiko vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimsifu kwa kitu kimoja, katika nchi ambayo inaenda kwa kasi tunayoona, kasi ya ukuaji wa pato la Taifa kwa asilimia saba kwa wastani, lakini miradi mikubwa inatekelezwa. Utakuta kwamba mataifa mengi yanashangaa kwamba bado tumeweza kuendelea na utulivu wa uchumi mkubwa. Utulivu huo umetokana na umakini wa Mheshimiwa Rais, lakini pia tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wetu wa Fedha na Mipango pamoja na Gavana wa Benki Kuu kwa ushauri mzuri waliotoa. Kwa sababu wangeweza wakachukua njia rahisi ya kufanya *inflation finance* maana ku-*print* pesa na kukuza mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wao hawakufanya hivyo, wametumia njia ngumu ya kukusanya mapato kutoka kwa Watanzania, hiyo njia ngumu kuliko ku-*print* pesa au kukopa tu na ni kweli kwamba hii miradi mikubwa ungekuta kwamba inashawishi watu sana kuchukua mikopo ya ziada, lakini nashukuru kwamba hawakufanya vile wamefanya kitu ambacho ni kigumu, lakini tunaona matunda yake ni mazuri na ndio hapa unasema hapa tunaona kuna *happy early*.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme hivi tumeona kuna utulivu wa uchumi wa ujumla ndio, *exchange rate* imekuwa *stable*, mfumuko wa bei uko chini, riba zimetulia lakini hazijatulia mahali pake kwa sababu ziko juu bado watu wanalalamika riba asilimia 15 *inflation* asilimia tatu, *really*

*interest rate* ni kubwa sana. Kwa hiyo, kinachohitajika sasa ni pengine tuhakikishe kwamba tunaendeleza sera hizo za kuhakikisha kwamba riba nazo zinashuka kwenye mabenki yetu. Utaona mabenki yanarekodi faida kubwa sana, mwaka huu kwa mfano, faida za mabenki ni kubwa sana kwa sababu wanatoza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoke hapo niseme hivi, kwa kuona kwamba miundombinu inaboreshwa vizuri, sasa njia ya peke ni kuongeza uwekezaji na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba ameunda Wizara ndani ya ofisi yake ambayo inashughulika na uwekezaji. Niseme hivi kwamba *private* sekta haitaweza kunufaika sana kama *blue print* aliyoizungumza Mheshimiwa Mwijage haitatekelezwa kwa umakini na kwa haraka zaidi. Inatekelezwa kwa *speed* tofauti tofauti kwenye kila Wizara, lakini ingetekelezwa kwa *speed* ile wanayotekeleza kwa mfano Wizara ya Viwanda naamini ungekuta vitu vinabadilika na pengine *private sector* ingeweza ikaanza kushika hatamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba tatizo kubwa katika sekta binafsi ni kusema kwamba uwekezaji lazima uwe mkubwa sana, kumbe sasa hivi uwekezaji hata kwenye nyumba yako unaweza kwa sababu kuna umeme. Ukishakuwa na umeme unaweza ukawa na kiwanda kidogo cha kuchakata hata ndizi na hiyo ndio njia peke kusema kweli ya kuinua kipato kule kwetu mashambani kwa kuunda viwanda vidogo kwa vikundi au kwa mtu mmoja mmoja ambaye ataweza kuchakata mazao akayaongezea thamani na yale mazao yakauzwa sehemu nyingine ambapo hayapatikani au ambapo yanahitajika kwa wakati ule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba pengine tuangalie namna gani ya kuwawezesha vijana wetu au wajasiriamali wanawake na wengine na hata akinababa kwa kuwapa *exposure.* Nikasema *exposure* haiwezi kutolewa kwa kumpeleka mtu China kuangalia maonesho China hapana, *exposure* ni kwamba pengine Shirika letu la *SIDO* lingekuwa karibu zaidi kule kwenye vijiji sasa linashughulika kwa kuona kwamba kweli linaonesha watu kwamba kuna

kiwanda kidogo cha shilingi milioni moja au laki tano na hiki kiwanda unaweza ukakitumia mkiwa vijana watano, mkakitumia mkaongeza thamani mkapeleka mkauza. Naamini kwamba hicho lazima kifanyike na naamini kwamba Wizara inayohusika itafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunazungumza mambo ya mikopo, kupeleka watu vyuo vikuu, hii nataka kusema katika uchumi tunaojenga sasa hivi uchumi wa kati, tatizo kubwa ni *skills study* zile za watu kufanya vitu kwa mkono sio kuwa na *degree* sio kuwa na ma-*Ph.D* hayatasaidia sana. Utakuta kwamba *unemployment* kati ya watu waliomaliza chuo kikuu ni kubwa sana lakini mtu anayetengeneza simu, simu hizi tunazotembea nazo hizi mfukoni ukimtafuta mtaani humpati na wana kazi, *mechanic* wote wana kazi lakini tatizo moja tunasema tu kwamba elimu yetu inalenga chuo kikuu, hapana! Huko ni kwa zamani, elimu ilenge daraja…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** …baada ya kumaliza *form six* watu wengi waende kujifunza kazi za mikono, *study* za mikono. Kwa hiyo, vyuo vya ufundi viongezeke…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Lakini na vyenyewe vibadilishe mwelekeo sio kuangalia zile *study* zilizokuwa zinahitajika zamani tuangalie *study* za kisasa, *electronic base* na ambazo…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei pokea taarifa, jitambulishe Mheshimiwa nani.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naitwa Mheshimiwa Musukuma, ningependa kumpa taarifa tu Mheshimiwa Dkt. Kimei kwamba anavyochangia anasema tuache kuamini ma-*degree* na ma-*PhD*. Nampa taarifa tu kwamba duniani kote matajiri wengi hawana *degree*. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa!

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Dkt. Kimei hujapokea taarifa hiyo, nisisitize tu Waheshimiwa Wabunge mumsikilize Mheshimiwa Dkt. Kimei hoja yake, ni hoja ya msingi sana. Hii habari kila mwanafunzi anaenda chuo kikuu anasoma vitu vya ajabu ambavyo tumezoea *traditionally,* sitaki kuyataja masomo, yako masomo yaani ni kama kumpotezea mtoto tu *direction*. Yalikuwa na maana enzi hizo, lakini leo hii dunia ya sasa, dunia ya uchumi wa kati, ndio hii anayopendekeza Mheshimiwa Dkt. Kimei. *Skills* na kwa hiyo hata mfuko wa mikopo uelekeze zaidi mikopo yake huko. Mheshimiwa Dkt. Kimei hebu rudia hiyo hoja yako bwana, nakupa dakika tatu. Katibu hebu iweke vizuri. *(Makofi)*

Waziri wa Elimu amekaa vizuri anakusikiliza sasa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ndio nasema hivyo kwamba, kusema kweli mahitaji ya uchumi wetu wa sasa hivi ni watu wanaoweza kutenda na mahitaji ni kwamba watu wana magari lakini hawawezi kutengeneza, ukitafuta fundi hakuna kwa sababu hakuna mtu anayefundisha vitu hivyo na siyo tena kutengeneza magari ambayo ni ya ajabu, sasa hivi tengenezeni magari ambayo lazima zile shule zetu za ufundi na zenyewe zi-*adopt* mahitaji ya sasa hivi. Ukienda uka-*register* wanafunzi utapata wanafunzi utapata wengi sana ukitafuta kwenye *electronic base industry* na nini utapata, lakini ukienda kwa ile ya zamani kwamba sijui unataka mtu wa kuranda. Tuna chuo cha ufundi pale kwetu Mamba pale lakini hakuna mtu anaenda kwa sababu wana mashine za kuranda wanafundisha kuranda

au cherehani za kushona lakini ni zile za zamani sasa hivi kuna cherehani za kisasa.

Mheshimiwa Spika, niendelee kwa kusema hivi kwa kule kwetu kama anavyosema Mheshimiwa Saashisha, kusema kweli zao la kahawa limedorola sana na nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais aliweka hilo pia katika zao la kimkakati. Hata hivyo, niseme hivi kule Kilimanjaro ile ardhi imeshadididimia haifai tena hata kulima kahawa, utatumia madawa mengi na watu hawajui kutengeneza *composite,* kwa hiyo unakuta kwamba ile kahawa ukiipeleka kuuza nje tena hupati hata wanunuzi. Halafu bahati mbaya pia vile vihamba vyetu, yale mashamba yetu yamekuwa *tragmented* mtu mmoja ana robo heka, atalima wapi.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi, sisi Wachaga wengine tunataka tuhamie mahali ambapo kuna ardhi, tukalime huko, mambo ya kusongamana kule haifai na wameniomba wananchi wangu wa Vunjo kwamba jamani ukienda tafuta mahali utakakoweza kutupeleka tukalime tupate eneo tulime na sisi tuwe na tija, tuwe na mabilionea na sisi, lakini kusema kweli kule Uchagani huwezi kuwa bilionea kwa sababu hakuna ardhi. Watu wa kule Vunjo tuna shida hiyo na nitakuja kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, atusaidie.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme hivi katika rasilimali tuliyonayo sisi kule Kilimanjaro, ni mlima Kilimanjaro na ni kweli wana Vunjo na wengine wote wanaozunguka ule mlima wanapata shida sana. Shida kubwa ni kwamba ajira haipatikani, vijana wengine wanaokuja kupata ajira kule ni kutoka maeneo mengine, lakini hata wale wanavijiji wanaozunguka ule mlima, ile nusu maili hawaruhusiwi kutumia, siku hizi wanapigwa, walikuwa wanasema ni wanawake tu waende huko, sasa wanawake wakaenda wenyewe, baadaye na wenyewe wakanyimwa kwenda huko kutafuta kuni, kutafuta majani ya ng'ombe na mbuzi na kadhalika. Sasa tunamwomba Waziri wa hifadhi naye atuangalizie hilo na ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Spika, mambo ya barabara yameshazungumza sana. Naunga mkono hoja ya kuongeza Mfuko wa *TARURA,* kusema kweli barabara zetu zina matatizo japokuwa hata zile ambazo zinatakiwa ziwekwe lami zimeahidiwa lami tunazo hizo kama tatu hivi ambazo Mheshimiwa Rais naye alituruhusu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Naona kengele imelia.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kimei, tunakushuru sana…

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa moyo moja na sisi tutatekeleza kila jambo ambalo liko kwenye hotuba hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu hotuba mbili za Mheshimiwa Rais. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri za kuendelea kulitumikia Taifa letu, lakini pia mipango yake mizuri ambayo wananchi ilikuwa ni tarajio lao.

Mheshimiwa Spika, hotuba hizi mbili zimeligusa Taifa, lakini limegusa jimbo langu katika kila nyanja. Mheshimiwa Rais alizungumzia uboreshaji upande wa sekta ya elimu. Kwa kweli elimu inaendelea kuboreshwa na kuendelea kupunguzwa changamoto ambazo ziko katika maeneo mbalimbali kwenye shule zetu ikiwa ni pamoja na kuwaondosha watoto wetu kukalia matofali pamoja na mawe. Ametoa agizo Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunaendelea kutekeleza kuhusu masuala ya wanafunzi wetu kukamilisha madawati pamoja na madarasa.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinakabili sekta hiyo hususan upande wa Nyang'hwale Waziri wa Elimu alichukue hili kwamba tuna upungufu mkubwa wa walimu hasa wa sayansi. Pia bado tuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu pamoja na vitendea kazi. Mheshimiwa Rais alizungumzia suala la kupunguza kero ya akinamama kufuata maji mbali, kupunguza kero hiyo vijijini pamoja na mjini. Nashukuru kwamba sekta ya maji imepiga hatua kubwa ikiwemo Jimbo la Nyang'hwale, tuna mradi mkubwa ambao tulitengewa fedha zaidi ya bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, mradi huu Waziri wa Maji atakuwa yupo, ajue kabisa kwamba mradi huu unakwenda kwa kusuasua, umechukua muda mrefu na tarajio kubwa la wananchi wa Nyang'hwale kupate maji kutoka Ziwa Victoria ni kiu chao kikubwa sana. Leo tumekuwa tukiahidiwa kwamba mradi huu utakamilika ndani ya miezi mitatu, ndani ya miezi miwili, lakini mradi huu haufikii mwisho. Wananchi wetu wanaenda wanapoteza imani kubwa na Wizara hii Maji kwa sababu ahadi hiyo inakuwa haikamiliki.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu wamezungumzia mtoto huyu *TARURA*, *TARURA* fedha zake inabidi ziongezwe tumekuwa na changamoto kubwa sana ya barabara kwenye halmashauri zetu, lakini *TARURA* amekuwa hawezi kukidhi kurekebisha barabara hizo kutokana na uchache wa fedha. Kwa hiyo, naungana na wenzangu kwamba hoja hii ya kumwongezea mtoto huyu wa *TANROADS*, *TARURA* aweze kupata fedha kuweza kukidhi shida mbalimbali zilizoko kwenye maeneo hususani kwenye halmashauri zetu ikiwemo Nyang'hwale; barabara nyingi zimeharibika *TARURA* hawezi kutokana na kiwango kidogo cha fedha ambacho anapewa.

Mheshimiwa Spika, hotuba hizi zimegusa maeneo mbalimbali imegusa upande wa umeme, kuboresha umeme kuongeza uzalishaji wa umeme ili sasa tuweze kuwa na viwanda na umeme wa uhakika. Nampongeza sana Waziri wa Nishati, juhudi kubwa zinafanywa huko vijijini lakini bado

kuna changamaoto. Nitazungumzia upande wa Jimbo langu, ni vijiji 62 lakini mpaka sasa hivi vijiji ambavyo vimeshawashwa havijazidi hata nusu. Yeye amesema hapa nilivyomsikia kwamba bado miezi michache vijiji vyote vya Tanzania vitakuwa vimekamilishwa umeme, sasa sijui na Nyang'hwale vitakuwa vimekamilika? Kwa hiyo, changamoto ya umeme Jimboni kwangu bado ni kubwa kuna maeneo mbalimbali nguzo zimesimikwa na mashimo yamechimbwa lakini waya ndiyo tatizo kubwa. Mkandarasi wetu kila unapoongea naye anasema tatizo kubwa ni la nyaya. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Nishati awasiliane na huyo mkandarasi aelewe tatizo ni nini. Si changamoto tu ya umeme kwa wilaya ya Nyang'hwale, ni maeneo mengi kwa hiyo, Waziri wa Nishati ajaribu sana kuangalia wakandarasi wake ili waweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kwa kipindi cha miaka mitano ikiwemo kuimarisha usafiri wa anga, leo Tanzania tunajivunia usafiri wa anga, tuna ndege zetu ambazo zimeshakuja na zingine zinakuja na kwa kweli zimeleta faida kubwa, zimeleta sifa kubwa kwa nchi yetu, lakini pia Rais wetu kafanya kazi kubwa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, muda wa hutoshi nataka nizungumzie suala la upande wa kilimo; wakulima wetu wamekuwa na changamoto nyingi ikiwemo pembejeo ambazo zinakuja mbovu, hazifai lakini changamoto nyingine kubwa ni soko la uhakika. Waziri wa Kilimo yupo, wananchi wetu mazao yao sasa hivi yapo hayana thamani, tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ajaribu kuliangalia sana suala hili la kuzuia upelekaji wa vyakula nje, wananchi wetu leo hii wanahangaika kupata fedha kwa sababu ya zuio hilo la kuzuia kupeleka chakula nje.

Mheshimiwa Spika, najaribu kuangalia leo hii jimboni kwangu debe la mahindi mpaka sasa hivi linauzwa shilingi 7,000, mkulima huyu atatoka vipi hapo alipo debe la mahindi shilingi 7,000 lakini kama kungekuwa soko la nje naamini kabisa asingeweza kuuza debe la mahindi shilingi 7,000. Kwa

hiyo, Waziri wa Kilimo ajaribu kuliangalia hilo zuio, sawa lina wakati wake hilo zuio, kama hali ya hewa ya chakula si nzuri, waweke hilo zuio, lakini kwa sasa hivi hali ya hewa ni nzuri na wakulima wetu wanapata vyakula kwa wingi ili waweze kutoka hapo, basi tunaomba soko hilo liweze kufunguliwa kuweza kupeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Mheshimiwa Rais alivyokaa na wachimbaji wa madini mbalimbali, kwa kweli hamasa imekuwa ni kubwa na pato la nchi limeongezeka, lakini bado kuna changamoto ziko kwa wachimbaji wetu wadogo wadogo. Nitazungumzia wachimbaji wadogo wadogo walioko Wilaya ya Nyang'hwale, wana maeneo ambao wameyavumbua lakini inakuwa ni tatizo kubwa la kuweza kuwapatia leseni. Kuna maombi mbalimbali ambayo yameombwa kwa wachimbaji wetu wadogo ili waweze kupatiwa maeneo ya uchimbaji lakini leseni zenyewe kutoka inakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Madini kwa sababu yupo hapa namwomba sasa, wachimbaji wadogo wa Wilaya ya Nyang'hwale wamekuwa na changamoto ya kupata huduma za Ofisi ya Madini kwa sababu Ofisi ya Madini inakuwa iko mbali, zaidi ya kilomita 90. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Madini aweze kuangalia namna gani ya kufungua Ofisi ya Madini pale Makao Mkuu ya Wilaya ya Nyang'hwale Kharumwa ili hawa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini waweze kupata huduma hiyo karibu hapo na kuweza kusababisha kuzuia mianya saa nyingine ya kuweza kutorosha madini haya. Mtu anapotoka eneo moja kwenda eneo lingine inawezekana kuna jambo liko pale katikati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Madini naomba ulichukuwe hili ili uweze kuwasaidia wachimbaji wa Nyangh'wale kwa kuwasogezea huduma. Nimeshalizungumza sana suala hilo.

Mheshimiwa Spika, bila kukuficha Mheshimiwa Waziri wa Madini, Nyangwale wamemuunga mkono sana

Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, sasa hivi utoroshaji wa madini asilimia 98 nakuhakikishia haupo tena. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Madini hakikisha basi unaifungua hiyo ofisi ili kuweza kukamilisha zile asilimia 2 za wasiwasi unaweza kutorosha madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya ardhi, Mheshimiwa Waziri wa ardhi yupo, wananchi wangu hususani wa Wilaya ya Nyang'wale wamekuwa wakienda kuomba kupimiwa ardhi zao pamekuwa na usumbufu mkubwa, njoo kesho, njoo kesho kutwa. Waziri wa Ardhi ajaribu kuwasiliana na Maafisa Ardhi wa Wilaya ya Nyang'wale ajue kwa nini wamekuwa wakiwasumbua wananchi kuhusu suala la kupima ardhi zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'wale. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais na wananchi wa Madaba kwa kupata fursa ya kutumikia jimbo la Madaba kwa awamu ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja katika mambo makubwa ambayo yamejitokeza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ni hoja na haja ya kuwa na uwekezaji jumuishi katika kilimo. Hili Mheshimiwa Rais alilipa kipaumbele kwenye hotuba yake kwa sababu kubwa tatu.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza sekta hii imeajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania, lakini sababu ya pili ni kwamba asilimia kumi au zaidi ya Watanzania ambao hawajishughulishi moja kwa moja na kilimo wamejiajiri kupitia sehemu ya mnyonyoro wa thamani wa shughuli za kilimo. Wapo waliojiajiri kwenye biashara ya mazao ya kilimo, wapo

waliojiajiri kwenye usindikaji kwa maana ya *agro-process*, wapo ambao wamejiajiri kwenye kutoa huduma za kifedha yakiwemo mabenki, *SACCOS,* wapo waliojiajiri kwenye usambazaji wa pembejeo, lakini pia wapo wengi waliojiajiri kwenye huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu ni kwamba sekta hii ndiyo inayochangia asilimia mia moja ya chakula cha Watanzania wote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alitoa kipaumbele kikubwa sana katika kueleza namna gani sekta hii ipewe kipaumbele na ipewe msukumo katika safari hii ya miaka mitano sehemu ya pili ya kipindi chake cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, leo naomba nitoe ushauri wa namna nzuri sasa ya kutekeleza maelekezo haya, ndoto na matamanio ya Mheshimiwa Rais kwenye sekta hii ya kilimo. Vitu ambavyo au jambo pekee ambalo linamfanya Mtanzania, mkulima aende shambani akawekeze kwenye kilimo, kivutio au *incentive* ya mtu kwenda kulima ni upatikanaji wa soko la uhakika na tija kwenye kilimo. Mambo makubwa yanayomfanya Mwanamadaba, Mwanasongwe na Mtanzania mwingine aache shughuli zingine akalime ni soko na tija kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa kipaumbele miaka mitano iliyopita na kumekuwa na mafanikio, mipaka ilifunguliwa, masoko walau yalikuwa na unafuu. Hata hivyo, bado changamoto ni kubwa kwenye sekta hii upande wa tija kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili ya kushauri na kabla sijashauri nimpongeze Profesa Mkenda na Naibu Waziri Mheshimiwa Bashe wameanza vizuri sana katika kukabiliana na changamoto za sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo napenda Serikali iendelee kuweka msisitizo ni kuwa na mkakati madhubuti wa masoko ya kilimo, bado hatujafaulu. Wakulima wa Madaba na maeneo mengine hata msimu huu wamepata shida ya soko la mahindi. Kwa hiyo ipo kazi kubwa

ya kufanya. Namshauri Mheshimiwa Waziri aangalie sana mkakati endelevu wa kuimarisha vyama vya ushirika ili vitumike kama sehemu ya kupambana na changamoto ya soko lakini mkakati wa uwekezaji kwenye usindikaji wa mazao, sekta hii ni sekta mama ambayo itatutoa.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili ambalo nitatumia muda mrefu kulifafanua ni hili la kuwekeza kwenye kupunguza gharama za kilimo. Jitihada zilizofanyika miaka hii mitano zimeonekana za kuhakikisha kwamba wakulima wanapata masoko ya mazao lakini hata pamoja na masoko kupatikana faida ambayo mkulima anaipata kutokana na shughuli zake bado ni ndogo kwa sababu gharama za uwekezaji kwenye kilimo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo mengi yanayochangia mambo matatu nataka niyaseme. Jambo la kwanza linalochangia gharama ya uzalishaji ni upatikanaji wa pembejeo kwa gharama nafuu. Jambo la pili ni gharama za usafirishaji wa mazao maeneo ya vijijini na jambo la tatu ni upotevu na uharibifu wa mazao baada ya mavuno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mkulima yupo Madaba na maeneo mengine ya vijijini, huko ndiko alikojaa Watanzania, huko ndiko wanakokaa asilimia 80 ya Watanzania na wanajishughulisha na kilimo. Moja ya vikwazo ambavyo nimevisema ni upatikanaji wa pembejeo kwa gharama nafuu. Hili la upatikanaji wa pembejeo lina mawanda mapanda, lakini moja katika maeneo ambayo nataka nisaidie na kuishauri Serikali ni uwekezaji kwenye maduka madogo madogo ya kusambaza pembejeo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pembejeo nyingi zinapatikana mijini na huko vijijini ambapo wakulima wapo hakuna maduka ya kusambaza pembejeo. Mkulima ili azalishe anasafiri kilometa nyingi kufuata pembejeo mijini. Suala hili nililisema katika Bunge lililopita. Sasa kinachokwaza upatikanaji wa maduka ya pembejeo vijijini ni gharama za uanzishaji wa maduka. Hapa ningeweza kwenda kwa *details*, lakini *TPRI,*

*TFRA* na *TOSCI* peke yao ili upate kibali cha kuwekeza kwenye duka la usambazaji pembejeo kijijini lazima uwe na laki nane ambayo haihusishi kununua mali ghafi. Sasa hatuwezi kupata mapinduzi ya kilimo kama hatutaki kutoa hizi tozo. Hatuwezi kumsaidia mwananchi wa kijijini kupata pembejeo kwa gharama nafuu kama hatutaki kupunguza hizi tozo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tutaenda nalo lakini naomba tulizingatie. Tuondoe hizi tozo ili tusaidie wajasiliamali wawekeze kwenye maduka madogo madogo ya pembejeo vijijini ili mkulima apunguziwe gharama za uzalishaji kilimo ili hata kama atakosa soko nzuri bado atauza kwa faida kwa sababu atakuwa amezalisha kwa gharama ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili ni gharama za usafirishaji wa mazao vijijini. Nashukuru Mheshimiwa mama Kilango amesema Watanzania wengi wamejaa vijijini, huko ndiko kwenye changamoto kubwa za miundombinu ya barabara na madaraja. Bajeti ya *TARURA* ni ndogo sana kuweza kukidhi mahitaji yaliyoko vijijini. Leo mkulima amelima mazao yake ili kusafirisha sehemu ambayo angesafirisha kwa shilingi laki moja anasafirisha kwa laki tano, hiyo inaongeza gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mama Kilango amesema ipo haya ya kuangalia uwezekano wa kuongeza bajeti *TARURA* ili barabara za vijijini zijengwe katika ubora, zipunguze gharama za uzalishaji kwa mkulima mdogo. Ndiyo maana nasema ni mkakati jumuishi wa sekta ya kilimo, sekta ya kilimo haiwezi kukua kama barabara za vijijini hazijaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu nililotaka kuliongelea na kuishauri Serikali ni kwamba Serikali iangalie namna gani itapunguza upotevu na uharibifu wa mazao baada ya mavuno. Tafiti zinaonyesha asilimia 30 ya mazao ya mkulima yanaharibika baada ya mavuno. Sasa hii asilimia 30 kama ingeweza kufika sokoni ingempa faida huyu mkulima mdogo. Leo mkulima mdogo pamoja na gharama kubwa za uzalishaji

zinazotokana na kutopatikana pembejeo kwa wakati na karibu pamoja na gharama kubwa za usafirishaji bado...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja yako ni ya msingi sana lakini muda hauko upande wako.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mchangiaji wetu wa mwisho mchana wa leo basi awe ni Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii lakini kwenye karatasi yangu niliandika niliomba nichangie kesho, ahsante.

**SPIKA:** Sasa hawa Wabunge wa Songwe maana alikuwa ni Mheshimiwa Mulugo akaweka kando, akaja Mheshimiwa Condester na yeye, haya inaelekea Songwe huko. Kwa wale ambao hawako tayari kuchangia leo wasilete karatasi yoyote mtaomba siku hiyo hiyo. Tuendelee na Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa fursa ya kuzungumza katika Bunge lako hili tukufu. Kama ulivyotamka majina yangu naitwa Husna Juma Sekiboko, ni Mbunge wa Viti Maalumu kutoka Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, nina na mambo machache ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais zilizowasilishwa katika Bunge la 2015 na hotuba yake mwezi wa kumi na moja 2020 kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda napenda nitumie kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa namna ambavyo Serikali ya

Awamu ya Tano katika kipindi chake hiki cha pili inakwenda kutekeleza masuala mbalimbali ya kimaendeleo katika nchi yetu. Vilevile nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo umeonesha uhodari mkubwa katika kuongoza shughuli za Bunge hasa kwa sisi ambao ni wapya tunaendelea kujifunza na kuimarika kwa haraka, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza imezungumzwa sana na Waheshimiwa Bunge waliokwishatangulia kuchangia kuhusiana na uchumi wa nchi yetu. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ameeleza namna ambavyo Serikali anayoiongoza angependa ipige hatua kubwa zaidi katika masuala mazima ya uchumi. Katika kuelezea hilo Mheshimiwa Rais amekazia katika sekta ya kilimo na ameeleza kabisa kwamba Wizara atakayoiunda ambayo tayari ameshaiunda sasa atatamani ishughulike moja kwa moja na ile mifuko ambayo inasaidia ukuaji wa sekta ya kilimo hasa kwa wananchi wa hali ya chini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuseme kweli kabisa sekta ya kilimo ambayo ndiyo inaajiri Watanzania walio wengi katika nchi yetu bado haijafanya vizuri kabisa. Namna nzuri zaidi ya kuweza kufanya vizuri ni kuhakikisha kwamba tunaweka mkazo kwenye yale mazao ya kimkakati kama mkonge, mahindi, mazao ya matunda ambayo yanazalishwa kwa wingi sana katika Mkoa wa Tanga, lakini vilevile mazao ya alizeti na korosho ikiwa hayo ndiyo mazao makubwa ya biashara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna ya kutekeleza haya nilidhani niishauri Serikali kwamba kwa miaka mingi sasa tumekuwa tunazungumzia namna ya kuboresha kilimo katika nchi yetu lakini yawezekana hatujaona tija kubwa siyo kwa sababu pengine bajeti inayotengwa haikidhi mipango ambayo inapangwa juu utekelezaji wa shughuli za kilimo lakini bado wananchi wetu hawajajuwa kilimo ni fursa na ni ajira ya uhakika. Namna ya kufanya kilimo kuwa ajira ya uhakika ni kutengeneza mipango mikakati ya kuidhinisha maeneo ya

mapori ya yaliyojaa kwenye nchi yetu na kupanga mazao ambayo yanaweza yakalimika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kule Handeni wakazi wengi wa Wilaya ya Lushoto kutokana na Lushoto kule ni milima mitupu wanaenda Handeni kulima mahindi lakini wanapata shida sana namna ya kupata ardhi ya kilimo pale Handeni kwa sababu siyo wenyeji pale na ukifika pale bado kuna tozo mbalimbali kwenye vijiji na Serikali za Mitaa ambayo bado inamrudisha nyuma, inamkatisha tamaa huyu mwananchi mdogo ambaye anahemea kule kwenda kufanya kilimo katika wilaya ambayo siyo ya nyumbani kwake. Pangekuwa na mkakati wa Serikali wa moja kwa moja kuwasaidia wale wote ambao wana nia ya dhati ya kufanya kilimo hata kwenye wilaya ambazo si za nyumbani kwao, wakaenda wakafanya kilimo chenye *support* kubwa ya Serikali kwa maana ya pembejeo na vifaa vingine vya kilimo pengine tungetoka kwenye hali ya sasa ambayo inaonyesha dhahiri kwamba bado hatujafanikiwa sana kuajiri vijana wengi kwenye kilimo kutokana na mikakati ambayo ipo sasa.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kufanya tathimini, ukiangalia matokeo ya kidato cha nne mwaka 2020, kuna wanafunzi zaidi ya 280,000 walipata *division four* na *zero*. Takwimu hiyo ya wanafunzi takribani laki tatu wanaotengenezwa kila mwaka na kutupwa na mfumo kuwa nje ya *system* nzima ya ajira rasmi baada ya miaka kumi unaweza kuwa na watu wengi sana ambao ni walalamishi kwenye nchi, hawana shughuli maalumu ya kufanya. Kama wangetengenezewa utaratibu maalumu wakawa wanawekwa kwenye sekta za ujasiliamali, sekta za kilimo na wakawa wanapewa mafunzo pengine ingewasaidia vizuri zaidi kupata ajira na kuacha kuilalamikia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia limeuliziwa katika swali asubuhi na Mheshimiwa Hawa Chakoma Mchafu kuhusiana na vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 64 ameelezea namna gani Serikali imefanikiwa kujenga vituo vingi vya afya na zahanati katika nchi yetu

ndani ya miaka mitano. Tumejengewa zahanati 1,998 lakini vituo vya afya 487. Hii ni hatua kubwa mno ambayo nchi yetu ndani ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna shida kubwa katika utoaji wa huduma katika vituo hivi. Baba mtu mzima ambaye anaenda kuhemea huduma kwenye kituo cha afya kilichopo pembezoni takribani pengine kilometa 90 mpaka 100 kwenda kwenye hospitali ya wilaya anashindwa kabisa kupata huduma za msingi kama vile dawa za presha na vipimo vingine ya kawaida ambavyo viwengeweza kufanyika kwenye ngazi ya kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna pekee ya kuweza kuondoa tatizo hili ni sasa Wizara ya Afya kuamua kubadilisha mfumo wa utekelezaji wa majukumu kutoka kwenye kuyagawa kwa hospitali na baadaye wayagawe kwa kada za watumishi au madaktari ambao wanapatikana kwenye hivyo vituo. Kwa sababu wapo madaktari wazuri na wasomi kwenye vituo vya afya, kwa nini wasipewe jukumu la kuweza kumpima mtu presha na kumpatia dawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mtu ambaye amepata shida labda ya kuvunjika mkono au mguu, tunavyoenda sasa, kama Serikali itapeleka vifaa tiba kwenye vituo vyetu kama ambavyo mwongozo wa afya unazungumza maana yake utakuwa na *X-Ray mashines* na vifaa vingi kwenye ngazi za vituo vya afya. Sasa akishapima hapo atakwenda wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Husna.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyo ni Mheshimiwa Husna Sekiboko kutoka Tanga, tunakushukuru sana.

Tunashukuru kwamba mjadala sasa unaendelea tu vizuri na wale wote ambao mmeleta majina jioni mtapata nafasi. Tutaanza na Mheshimiwa Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa na wengine wote tutapata nafasi kadri hali itakavyokuwa, tuendelee kujiandaa tunaendelea vizuri.

Nilitaka kuwaambia Wajumbe wa Kamati mbalimbali yale mambo ambayo mtajiwekea tangu mapema, maana kuna kazi mtaletewa na Spika kwenye Kamati lakini kuna kazi ambazo zinatokana na ninyi wenyewe kama Kamati namna mnavyoona mambo na mnavyojipanga na mkihitaji msaada wa ofisi tuko tayari kufanya hivyo. Niwahakikishieni yapo baadhi ya malengo msipojipanga vizuri yanaweza yasifikiwe miaka mitano. *(Makofi)*

Tunazungumza hapa Bima ya Afya kwa Wote, Kamati ya Huduma za Jamii mkichekacheka miaka mitano itaisha hapa hiyo sheria haijafika. Kwa hiyo, maana yake lazima muanze nayo tangu mwanzo *consistently,* kila *session* inayofuata bima ya afya imefika *level* gani, *we want it,* tunataka hivi na hivi, siyo tu mnataka na ninyi muendelee ku-*brainstorm* namna gani mnadhani iwe maana hili jambo ni gumu siyo yepesi, namna gani kitu kama hicho kinaweza kuwa katika nchi yetu. Jambo hili ni msaada mkubwa sana wa uhai watu wetu walio wengi na sisi ni watu tunaotengemea kura za wapiga kura.

Kamati za Huduma za Jamii masuala ya mabadiliko ya mtazamo katika elimu, mtaona kuna haya kubwa sana, si lazima tusubiri mjadala wa kitaifa au sijui kitu gani, sisi wenyewe kama Kamati tuna maono gani na tunashauri nini Serikali katika eneo hilo. Ni ukweli kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Dkt. Kimei watoto wanasoma masomo akirudi huna pa kumpeleka naye hana cha kufanya. Kwa nini tusielekeze nguvu zetu nyingi zaidi katika maeneo haya ambayo anaweza kujiajiri na yanasaidia nchi sana katika uchumi wa kati kuweza kwenda mbele na halali njaa hata siku moja badala na kuwa na *degree* ambayo haina *utility* kabisa na kadhalika.

Hatusemi kwamba zifutwe lakini ni vizuri kuwaelekeza vijana katika maeneo hayo. Hivi kwa nini mwalimu wetu wa sekondari awe na masomo mawili tu ya kufundisha, kwani ni lazima na ndiyo hivyo dunia nzima kwamba ana masomo mawili tu? Kwa nini yasiwe matatu? Kwani ni lazima twende na mfumo huo? Unakuwa na mwalimu mmoja anafundisha *Physics, Chemistry, Mathematics* kuna shida gani? Mwalimu wa *Chemistry* na *Mathematics* anashindwa kufundisha *Physics?* Hawa wa masomo mawili mawili tutafika, hata walimu wa shule ya msingi nao wana masomo mawili mawili au matatu sasa utaajiri walimu wangapi? Kwa nini mwalimu wa shule ya msingi asiwe na masomo matano anayofundisha au hata zaidi ya hayo kwani kuna shida gani na kadhalika. Lazima tubadilike yaani hatuwezi kwenda tu Mwingereza alivyotuacha na sisi tunaenda tu hivyo kila siku, haiwezekani, kwa hiyo, tuwashauri sana. *(Makofi)*

Niliwahi kutoa mfano wakati fulani wa wenzetu mfano Wachina, nilikuwa nimetembelea China mwaka jana au mwaka juzi, nikaenda kwa Balozi wetu pale, akaniambia alipofika pale akahitaji marekebisho kidogo kwenye nyumba yake, kwa hiyo, akawaambia nitafutieni kijana wa kurekebisha makochi haya, akatafutwa kijana akaja pale kurudi jioni akakuta ameshaRekebisha vizuri kabisa.

Akamwambia sasa nitafutie mwenzako atakayenisaidia kurekebisha mabomba, kuna mabomba humu ndani yanahitaji kurekebishwa. Akamwambia haina shida unaweza ukanionyesha, akamuonyesha akamwandikia vifaa, akamwambia una shilingi hizi, hiyo hela ya China, akamwambia hizi ninazo akampa, akiamini anaenda kumtafuta kijana mweziye aje afanye kurudi jioni kashamtengenezea mabomba yule yule.

Akamwambia tena sasa kuna shida ya umeme chumba hiki na hiki, twende nionyeshe, kurudi jioni kashatengeneza umeme. Mwisho wa siku simu yake ilikuwa inasumbua kitu fulani akamwambia hebu nipe, akaweka kitambaa kwenye miguu yake mara moja tu akamwambia simu tayari hii, *do you see*?

Hao ndiyo vijana tunaotaka. Hatutaki *VETA* ambayo ni seremala tu mpaka asubiri kazi ya seremala, mwingine kasoma bomba kama hakuna kazi ya bomba yeye anazunguka na spana yake. *VETA* imfundishe kijana awe *dynamic* akipata kazi hii anafanya, akipata kazi hii anafanya, akipata ile anafanya. Kwa hiyo, halali njaa yaani haangahiki na tunaweza mambo hayo kuliko hii ya kukariri kitu kimoja tu, alivyotuacha Mwingereza kitu kimoja tu, hatuwezi kufika lazima kuwe na vitu vingi. Sasa Kamati zetu hizi tuna mambo mengi sana ya kufanya na tuanze na Mawaziri wetu hawa tuanze nao tangu mwanzo *consistently* na vile vitu ambavyo tunataka na sisi tu-*achieve in five years.* Mkiamini kuna *time* huko mbele *there is no time*. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

*(Saa 07.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilikwishamtaja Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Adamson Mwakasaka na atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa.

Mheshimiwa Mwakasaka tafadhali.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii ambayo nimeweza kuipata kwa ajili ya kuchangia hii hoja iliyopo mbele yetu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nami kama wengine walivyoanza naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo imejenga na ina dira ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nina hoja chache sana kwa sababu nyingi zimeshazungumzwa na waliotangulia,

nitachangia kidogo kwenye kilimo kwa sababu naona wengi wameongelea kilimo; upotevu wa baadhi ya mazao ya kutoka kwenye kilimo yameongelewa zaidi, sehemu za kuhifadhia kwamba ni moja ya sehemu inayofanya kuwe na hiyo *harvest loss* ya *30 percent to 40 percent* ambayo imetajwa kwenye ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pia nadhani mbegu zinachangia sana katika upotevu wa mazao. Kwa mfano kwenye mahindi kuna mbegu ambayo ipo sasa hivi ambayo hata kama imekomaa yule mkulima akichelewa kidogo tu kuivuna anakuta kwamba tayari yale mahindi anavuna yakiwa yameoza, lakini ile ni ubora wa ile mbegu. Wizara hii ya Kilimo inafanya kazi nzuri sana lakini kwenye suala la mbegu bado kuna changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la reli; ni kweli sasa hivi reli inajengwa kwa kasi kubwa na hasa *SGR,* lakini pia tunahitaji ile reli ya zamani kuendelea kuwepo kwa sababu nafahamu kwamba hii reli ambayo sasa hivi ni ya kisasa hata kama itakuwa imekamilika, bado kuna shughuli za usafirishaji zitaendelea kuwepo kwa kutumia reli ya zamani. Kwa hiyo kuna umuhimu sana wa kuimarisha reli ile ya zamani na hasa maeneo ambayo tumekuwa kila siku tukiyasikia miaka na miaka, maeneo ya Kilosa yale nadhani ni Gulwe na maeneo mengine ya Godegode, kila mara reli inachukuliwa na maji na inaigharimu Serikali hela nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani wakati umefika Serikali ibuni namna gani itafanya hata kama itatumia fedha nyingi sana kuinua matuta makubwa kwenye hii reli ya zamani ambayo ile treni itapita juu kabisa isikutane na yale maji, kitu ambacho kitakuwa *sustainable,* sio hii ya kila siku zinapelekwa *billions* za fedha pale, lakini kila mwaka mvua ikija eneo lile reli inachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la miradi ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiisimamia ambayo kwa kweli hata Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi ufanyaji

kazi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli na miradi ambayo imeibuliwa na inaendelea imetubeba sana hata kwenye uchaguzi uliopita.

Mheshimiwa Spika, hii miradi ni endelevu, sina uhakika kama miradi yote hii kwa mfano ya nishati ile ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kule lakini nimetoka kuzungumzia *SGR* na miradi mingine mikubwa; miradi hii sijui kama inaweza ikaisha yote kabla Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hajamaliza kipindi chake. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais anaiheshimu sana Katiba na ameshazungumza kwamba yeye hatoongeza kipindi, ataondoka, sasa yeye yuko *very strong* lakini ile miradi iko *protected* namna gani, ile miradi mikubwa aliyoianzisha itaendelezwa kinamna gani?

Mheshimiwa Spika, hapa hoja yangu ni kwamba tunatakiwa tujifunze kutokana pia na matukio ya wenzetu. Hivi karibuni baada ya uchaguzi wa Marekani, siku ya kwanza tu Joe Biden alisaini *executive orders* za ku-*revise* vitu alivyovifanya Trump, *the same day* ambayo aliapa alisani. Kwa hiyo ina maana yeye katika kipindi chote kuna vitu ambavyo alikuwa hakubaliani navyo, alikuwa anasubiri tu akiingia avibadilishe.

Mheshimiwa Spika, sasa naongelea hili kwenye miradi mikubwa ambayo Mheshimiwa Rais ametuanzishia na inakwenda vizuri na ni muhimu sana kwenye kujenga uchumi wa nchi yetu; iko *protected* namna gani? Ili asije akaingia mtu, maana yake kwa sasa Mheshimiwa Rais yuko madarakani kila mmoja anam-*support,* lakini mioyo yetu tunaifahamu wanadamu, kubadilika ni wakati wowote. Hatujui, je, miradi hii itaendelezwa akiondoka? Sasa mimi pendekezo langu hapa ni kwamba ikiwezekana ziimarishwe *institutions* ambazo zitalinda hii miradi ili isije ikaguswaguswa na wengine watakaokuja mpaka iishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukizungumza hivyo unaigusa kidogo Katiba, lakini nimewahi kusema hapa kwamba Katiba sio Msahafu au Biblia, hata Mheshimiwa Rais wakati anaingia nakumbuka kwenye hotuba yake ya kwanza alipokuja hapa

aligusia Katiba na hakuna mahali aliposema kwamba labda Katiba ile haifai. Labda ninukuu kidogo kwenye ukurasa wa 12 wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2015; naomba ninukuu, anasema; *"Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mchakato wa Katiba Serikali yangu imepokea kiporo cha mchakato wa Katiba ambao haukuweza kukamilika katika Awamu iliyopita kutokana na kutokamilika kwa wakati kwa zoezi la uandikishaji wapiga kura.*

Anaendelea, anasema; *napenda kuwahakikishia kuwa tunatambua na kuthamini kazi kubwa ya kizalendo iliyofanywa na wananchi walioshiriki hatua ya awali ya ukusanyaji wa maoni kuhusu Katiba mpya. Pia tunatambua kazi nzuri ya Tume ya Marekebisho ya Katiba na Bunge la Katiba lililopita lililotupatia Katiba inayopendekezwa. Tutatekeleza wajibu wetu kama ulivyoainishwa katika Sheria ya Marekebisho ya Katiba; napenda mtuamini hivyo."*

Mheshimiwa Spika, naomba ili miradi hii asije akaichezea atakayekuja tuangalie utaratibu, hata kama utakuwa ni wa Azimio la Bunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, naam!

**SPIKA:** Hii ajenda ya sijui nani ataondoka, nani atakuja siipendi sana kwa sababu tunaishia kuwatia hofu wananchi; tuamini Mungu ni mwema na tupo na Rais yupo. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, mimi hoja yangu hapo ni kwenye namna gani tutailinda hii miradi ili isije ikaishia njiani. Ndiyo maana nilitoa mfano huu wa Marekani, kwamba kwa mfano Trump angekuwa amepewa wigo mpana wa kugusa vitu vingine, maana yake aligusa vidogovidogo tu, zile *executive*

*orders,* Biden akaweza kuzibadilisha, lakini Trump hakuwa mtu wa kawaida, lakini kuna vitu alizuiliwa kwenye Katiba asiviguse. Kwa hiyo, maana yangu hapa ni kuzi-*strengthen institutions* kwa mfano Mahakama na Bunge.

Mheshimiwa Spika, leo kwa mfano Bunge tukiazimia hapa kwamba miradi fulani ambayo ni ya kimkakati hata likija Bunge lingine isibadilishwe au isisimamishwe na kama itakuwa iko kwenye Katiba yule mtu hatogusa hii ndiyo *concern* yangu. Kwa sababu hii ni *legacy* kubwa Mheshimiwa Rais atakapoondoka ataiacha, miradi hii aliyoianzisha ni *very productive* kwenye *economy* lakini...

**SPIKA:** Yaani hoja yako naielewa, tunaielewa vizuri sana.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Kwa mfano Makao Makuu ni Dodoma, hatutarajii tena aje mtu mwingine aseme ana Makao yake Makuu Sumbawanga au mahali pengine.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, iko *protected* wapi? Akija mtu akisema anataka kurudisha Dar es Salaam?

**SPIKA:** Ahsante sana, bahati mbaya sasa na muda nao umekuwa...

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana wakati huu wa mjadala huu muhimu sana wenye shida kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu au Mawaziri kwa ujumla wake, ni vizuri mkaandika na ni vizuri zaidi ukiandika kwenye... au siyo, maana simu tumeziruhusu wala hazina shida humu, ni vizuri

zaidi; mnanisoma? Kule Zanzibar wanasema mnanifahamu? *(Kicheko)*

Mmeshanifahamu? Ndiyo, mkienda watu 20, 30 hapo kwa Waziri Mkuu sijui kama kesho hataanza kukohoa na nini kwa hiyo *please* tuchukulie hilo jambo *seriously.*

Niliyemtaja anayefuata aendelee; Mheshimiwa Abdul-Hafar.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutupa kibali cha kuwa hai na kutunusuru na mambo mbalimbali tunayoyaona na tusiyoyaona.

Mheshimiwa Spika, la pili, nikushukuru wewe, nami kwa mara ya kwanza leo nasimama katika Bunge lako Tukufu kwa ridhaa yako, nakushukuru sana. Kwa namna ya kipekee nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kilichonipa fursa ya kukiwakilisha katika nafasi ya kugombea Ubunge katika Jimbo la Mtoni; na hapohapo niunganishe kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtoni Zanzibar kwa kunichagua mimi leo hii nikawa Mbunge katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza nikisimama leo hii nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mtoni. Imani waliyoiwekeza kwangu sina mashaka yoyote kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitailipa kwa kuwatumikia wao na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja na kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hapohapo naendelea kumpongeza kwa kuendelea kuwa Mwenyekiti mwema wa chama ambacho kinaiongoza Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Mtoni, tulifarijika sana pale ambapo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania aliposema wazi ndani ya Bunge hili Tukufu akituhutubia sisi na akilihutubia Taifa hili kwamba katika awamu yake hii anaendelea kuahidi kuulinda Muungano wa Tanzania kwa gharama yoyote; tulifarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sisi kule Zanzibar Mapinduzi kwetu ni jambo la mbele yawezekana kuliko uhai wa mtu mmoja mmoja kwa maslahi ya Taifa hili, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusema tena wazi kwamba Mapinduzi ya Zanzibar yataendelea kulindwa na kuheshimiwa katika utawala wake; tunampongeza sana katika hotuba yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze kwa uchache sana lile ambalo pia nimedhamiria kulichangia kwa maslahi hasa ya wananchi walionituma katika Bunge hili, wananchi wa Jimbo letu la Mtoni. Jimbo letu nasi linapakana na bahari, moja ya mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameyasema atayasimamia na Serikali hii ya Awamu ya Tano katika kipindi cha pili tutayaona ni kuimarika uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi wa Bahari Kuu ni moja kati ya Sekta za Muungano. Ni kweli bado kwa nguvu zetu za ndani hatujafanya vizuri sana katika uvuvi wa Bahari Kuu, lakini pia Bunge lako tukufu hili katika mwaka 2018 moja ya ripoti za Kamati zilisema wazi kwamba kama tukiwekeza vya kutosha katika Bahari Kuu, Taifa letu linao uwezo wa kupata takribani bilioni 350 kila mwaka kutokana na uvuvi wa Bahari Kuu. Sina mashaka yoyote kwa haya yaliyosemwa 2018 yalitoa dira kwa Chama Cha Mapinduzi kuweka katika Ilani yetu, lakini yalitoa dira kwa Rais wetu kuja kuyazungumza mbele ya Bunge hili Tukufu na hivyo kuwahakikishia Watanzania kwamba meli nane za uvuvi katika Bahari Kuu zitakuja katika awamu yake hii ya pili.

Mheshimiwa Spika, sisi kule Zanzibar, hasa wananchi wa Mtoni, tumefarijika sana kwa sababu meli nne katika hizo, bila kuficha maneno Rais amesema hizi zitakwenda kufanya uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar na sina mashaka yoyote

itachochea uchumi wa Zanzibar na wananchi wenzetu katika majimbo yetu kwa kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar sisi bahari ni kitu muhimu sana na eneo la bahari ni kubwa kuliko eneo la ardhi ambalo Mungu ametutunuku. Kwa hiyo kivyovyote Bahari Kuu ni kubwa kuliko bahari ndogo ambayo kwa sasa inatumika na inaleta maslahi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa kule Mtoni wameniagiza niseme katika Bunge hili na nichangie hotuba hii kwamba ujio wa meli ile ama meli hizo zitakapofika hawaoni tu mabadiliko ya uchumi wa mtu mmoja mmoja lakini wanaona mabadiliko ya kifikra kwa wawekezaji wetu na wao sasa kuanza kuwekeza kwa kuleta meli zenye uwezo wa kuvua Bahari Kuu na hivyo kuongeza ajira kwa wananchi wetu wa ndani lakini kuongeza pato la fedha za kigeni kupitia kuuza samaki hawa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo imejipambanua wazi kupambana na masuala ya kifisadi katika awamu hii ya pili. Ni kweli vijana wengi ama fursa nyingi za ajira zimejitokeza katika awamu iliyopita na tunatumai yale tuliyoahidi na yaliyoahidiwa na Ilani ya Chama chetu, Serikali yetu kupitia Rais wetu aliyo madarakani itayatizmiza kwa kuendelea kupambana na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, tukipambana na ufisadi zile ajira milioni nane tulizowaahidi Watanzania katika ilani yetu, na chini ya usimamizi wa Dkt. John Magufuli, tuna uhakika zitatimia. Viongozi wenzetu katika Serikali mkimsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia mianya ya upotevu wa fedha, hali za wananchi wetu zitaendelea kuimarika, fursa za Taifa hili kwa vijana zitaendelea kuimarika na sisi viongozi tuko tayari kuendelea kushirikiana na Serikali; na wananchi wa Jimbo la Mtoni wamenielekeza nimalizie kwa kusema wataendelea kuiunga mkono Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iyatende yale ya Muungano kwa maslahi ya Wazanzibari na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa kwa mchango wako.

Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Paulo Mbogo; Mheshimiwa Nyamoga tafadhali.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, pia nami nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ananiwezesha kwa mara ya kwanza kusimama hapa Bungeni na kuchangia. Nikushukuru wewe, lakini pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilolo ambao waliniamini na kunituma niwawakilishe.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza kwenye suala zima la kilimo na mnyororo wa thamani, lakini kabla sijaenda huko, napenda kupongeza na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo ilijaa hekima, busara, mwongozo na maono ambayo naamini katika miaka mitano ijayo tutakuwa na *story* au hadhithi ya kusimulia ya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Tume ya Uchaguzi, kwenye hotuba ilionesha wazi kwamba walifanya matumizi mazuri ya hela hadi kuwa na albaki ya karibu bilioni 69, kiwango cha uadilifu mkubwa ambacho walikionesha.

Mheshimiwa Spika, tukielekeza macho yetu kwenye suala zima la kilimo hasa kwenye suala la uwekezaji, napongeza hotuba hiyo kwa sababu ukurasa wa 29 unataja chai pamoja na mazao mengine kuwa mazao ya kipaumbele. Naomba nijikite kwenye hili suala la chai hasa mawazo na maoni ya wananchi wa Kilolo.

Mheshimiwa Spika, pale Kilolo kuna jumla ya hekta 3,600 ambazo zina rutuba kwa ajili ya kilimo cha chai. Siyo hivyo tu, kuna zaidi ya hekta 184 zimepandwa chai tangu miaka ya 1990 na kuwekewa kiwanda feki. Ile michai hivi

tunavyozungumza, ile miti imekuwa inatosha hata kujinyongea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu miaka ya 1990 imekuwa ni kutafuta mwekezaji. Sasa najiuliza, pamoja na nia na dhamira ya Mheshimiwa Rais, ikiwa tutachukua zaidi ya miaka 30 kutafuta mwekezaji kwa ajili ya shamba na kiwanda cha chai kimoja, tutafika ndani ya miaka mitano?

Mheshimiwa Spika, lazima kuna mahali tunakwama. Nami napenda sana kumwomba kaka yangu, Waziri anayehusika na uwekezaji pamoja na viwanda na biashara ambao wanalijua jambo hili walitilie mkazo kwa sababu uzalishaji wa chai katika Wilaya ya Kilolo ambapo ardhi yake inafanana na Wilaya ya Mufindi yenye zaidi ya viwanda saba, hiyo ingeweza kukuza uchumi kwa kiwango kikubwa na wananchi wale waliopanda ile michai wanataka kuanza kung'oa kubadilisha mazao.

Mheshimiwa Spika, napenda kulizungumzia hili kwa mkazo kwa sababu watu ni lazima wajue kwamba moja ya sababu ya kupanda ile chai ilikuwa ni zao linaloweza kulinda vyanzo vya maji ambayo ndiyo yanayoenda Mtera na hata Kidatu. Kwa hiyo, tutakapobadilisha na kulima zao lingine pia tutavuruga vile vyanzo vya maji ambavyo vinalindwa kutokana na kulima lile zao la chai.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nizungumzie zaidi kuhusu tafiti zinazofanywa na uelekezaji wa mazao. Hivi karibuni nilimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa kule Kigoma akihimiza sana utafiti wa mbegu na uzalishaji wa zao la mchikichi ambalo linalimwa katika mkoa ule.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba watu wa Kilolo wanalima maparachichi; na siyo Kilolo tu, ni Mkoa mzima wa Iringa na sehemu ya Mkoa wa Njombe. Changamoto yake ni aina ya miche wanayopanda, hiyo mbegu wanayolima; je, ni ile ambayo itapata soko wakati watakapoanza kuvuna?

Mheshimiwa Spika, hapa napenda kutoa ushauri kwamba ipo hii Taasisi ya Utafiti inayoitwa TARI, napenda waelekeze nguvu kwenye utafiti wa mazao ya matunda na mbogamboga kwa kuweka kituo kabisa katika Mkoa wa Iringa au Njombe kwa ajili ya kuhakikisha haya mazao kama parachichi yanapolimwa, wakulima wanalima mazao sahihi ambayo yatapata soko wakati wa kuvuna utakapofika.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kila mtu anakuza miche, anaokota mbegu huko, wakulima wanauziwa, wakati mwingine wanaambiwa ndani ya miaka mitatu wataanza kuvuna, ikifika miaka mitatu mti unarefuka tu na hakuna mazao kwa sababu hawakujua kama hiyo mbegu wanayotaka kuilima ni bora ama siyo bora. Udhibiti wa mbegu hasa miche, ni changamoto kwenye uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia umuhimu wa mnyonyoro wa thamani katika mazao yanayolimwa kwenye maeneo yetu. Kwa sababu tuna nia ya kuwa na nchi ya viwanda, ni lazima kuangalia ni jinsi gani tunaboresha mnyororo wa thamani. Nitatoa mfano wa zao la nyanya ambalo linalimwa sana katika baadhi ya maeneo kwenye Jimbo langu pia. Maeneo hayo ni Ilula na Ruaha Mbuyuni yote ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa huwa wanapita na kununua nyanya.

Mheshimiwa Spika, wakati unapita mara ya kwanza unaweza ukanunua tenga moja kwa shilingi 10,000/= lakini upo wakati utakaonunua kwa shilingi 90,000/=. Sababu ni kwamba hakuna namna nzuri ya uongezaji wa thamani kwa mazao yetu. Kwa hiyo, wakati fulani wananchi wanalima kwa gharama kubwa na wanashindwa kuvuna na kuuza kwa bei kubwa kwa sababu thamani yake haijaongezwa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri haujafanyika utafiti wa kutosha wa masoko kwa sababu nafahamu ziko nchi ambazo hazilimi nyanya lakini zinauza nje. Wakati mwingine tumesikia baadhi ya mazao yanasafirishwa kwenda nchi nyingine na kule yanapofika ndipo yanapouzwa. Mfano mmojawapo ni

parachichi; ukifanya utafiti utakuta bandari zetu bado hazi-*pack* na kupeleka nje, wala viwanja vyetu vya ndege; lakini zipo nchi ambazo tayari zinafanya hivyo kwa kuchukua mazao hayo kutoka kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hili tusipolifanyia kazi maana yake ni kwamba tunazinufaisha hizo nchi jirani. Pamoja na ujirani mwema, lakini siyo kwa kufikia kiwango cha sisi kulima parachichi, miti ya mbao, zikauzwe kupitia nchi jirani. Napendekeza suala hili lifanyiwe utafiti wa kutosha na Wizara zinazohusika ili mazao yanayolimwa na wakulima kwenye maeneo yetu yaweze kuongezewa thamani na wananchi wale waendelee kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 33 unaoelezea kuhusu ubora wa mifugo na vitu vingine mbalimbali. Tukizungumzia mifugo, tunazungumzia uboreshaji wa thamani. Katika hili napenda kupongeza maana ndani ya hotuba hii imetaja baadhi ya machinjio yanayoboreshwa. Katika Mkoa wa Iringa iko machinjio moja ambayo naamini ni mojawapo itakayoboreshwa.

Kwa kuwa machinjio hizi baadhi yake zimechukua muda mrefu; na kwa kuwa baadhi ya watu wanaoishi katika maeneo yetu ya Jimbo la Kilolo na maeneo mengine ya Mkoa wa Iringa ni wafugaji, napendekeza kasi ya uboreshaji wa machinjio hizi iweze kuwa ya kwenda mbele ili wananchi hao waweze kufaidika mapema.

Mheshimiwa Spika, wakati huu ninapozungumzia hili, napenda pia nizungumzie kuhusu vyanzo vya utalii hasa katika Mkoa wa Iringa na hususan Jimbo la Kilolo ambalo natoka. Moja kati ya utalii unaohimizwa ni utalii wa kihistoria. Pale kwenye Jimbo langu la Kilolo, Kihesa Mgagao pale waliishi wapigania uhuru wa maeneo mbalimbali, hata Rais Mstaafu wa Afrika Kusini, Marehemu Nelson Mandela alishafika pale. Pia pana kumbukumbu nyingi za wapigania uhuru hao, kumbukumbu ambazo kwa sasa lile eneo limegeuzwa kuwa gereza.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Kilolo hatusemi kwamba hatufanyi makosa; tunafanya, lakini gereza lile idadi ya wafungwa wake hawafiki 20. Pia pale ni sehemu ya kumbukumbu za kihistoria. Wanafunzi wa Kilolo na maeneo mengine ya Mkoa wa Iringa hawawezi kwenda kujifunza pale kwa sababu ya ulinzi uliowekwa mahali pale.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sanasana Mheshimiwa Nyamoga. Nilishamtaja Mheshimiwa Vincent Paulo Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha Wabunge wote, tumepata ushindi wa kishindo na Mwenyezi Mungu ametuwezesha kuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja Hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo imegusa nyanja zote; ametupa uelekeo wa nchi nzima na baada ya miaka mitano kama haya tutayasimamia kama Wabunge kwa nia njema ya maono na kumsaidia Mheshimiwa Rais, nadhani nchi ya Tanzania tutapiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa ni tajiri kama maono ya Mheshimiwa Rais anaposema anataka mabilionea. Mkoa wa Rukwa ni matajiri kwa sababu hali ya hewa ni nzuri, ni wazalishaji wazuri, tatizo ni miundombinu. Naomba Wizara inayohusiana na miundombinu hasa upande wa barabara, baadhi ya barabara, mfano kwenye Jimbo langu la Nkasi Kusini, mimi

sina mjini; ni vijijini, porini, ni wazalishaji tu, lakini hakuna barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija Jimbo la Nkasi Kusini upande wa Ziwa Tanganyika, bado hatujalitumia. Ziwa Tanganyika bado linatumika ndivyo sivyo. Namshukuru Mheshimiwa Rais amesema ataweka meli ya mizigo, sasa meli ya mizigo ikija na miundombinu hamna, itakuwa bado ni shida.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hizi ziangalie maeneo ambayo ni *economic zone* kila jimbo. Kuna barabara ambazo ni *economic zone*, ndiyo mhimili, ndiyo mgongo wa Jimbo. Mfano ni barabara ya Wampembe, Ninde, Kala na Mpasa. Zile ndiyo mwambao mwa Ziwa Tanganyika ambazo wale watu wamejikarantini kiuchumi. Tunaongea masuala ya kujikarantini, lakini kwenye Jimbo langu baadhi ya kata kama nne zimejikarantini, masika hakuendeki, labda utumie pikipiki; kwingine pikipiki haifiki inabidi utembee kwa mguu.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Jafo anapafahamu Wampembe. Naomba sana hizi barabara za Ninde, Kala na Wampembe ziingizwe *TANROADS*, hakuna namna, *TARURA* wamezidiwa, naungana na mama yangu Mheshimiwa Malecela. *TARURA* wamezidiwa, tuwapunguzie mzigo; baadhi ya barabara ziingie *TANROADS* na nyingine zibaki *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika mikoa inayozalisha ni pamoja na Rukwa; na katika Rukwa, Jimbo la Nkasi Kusini. Tukija upande wa pembejeo ni gharama mno kwa mkuma mdogo *(peasant).* Kwa nini isifike mahali kupata maeneo vijengwe hata viwanda vya mbolea? Wizara ikae, i-*sort* maeneo, kuwe na zone za kujenga viwanda hasa mikoa ile inayozalisha sana mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Maji, katika Jimbo langu kuna watu bado wanaishi maisha ya ujima. Kipindi cha ujima tulisoma kwenye historia, lakini katika Jimbo langu watu wapo wana-*depend on nature*. Naomba

Wizara hii; nilipita na watendaji wengi ambapo najua ni kilio cha nchi nzima; Wizara ya Maji inabidi ikae pembeni ifanye kama *special operation*, kwa sababu kilio cha wafanyakazi kule ni wachache, wataalam wa maji hakuna. Ingefanywa tathmini angalau hata robo kwenye baadhi ya miradi, Mheshimiwa Rais anahangaika anatuma fedha na fedha zipo nyingi sana lakini watendaji hakuna. Kuna mradi kama wa Wampembe, Mradi wa Kala, Mpasa na Mradi wa Chala, maeneo yote hayo fedha zipo ila wataalam wako wachache, wanazidiwa. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Maji ikae chini iwe na *special operation* upande wa maji katika majimbo yetu, ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana kumshukuru Mungu, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais, sisi sote humu Mzee amesema alikuwa ana hofu sijui ni *successor* au nini, sisi ndiyo walinzi wa nchi hii. Maono ya Mheshimiwa Rais, ametukabidhi sisi Wabunge ambao ndiyo wanasiasa, ndiyo wa kusimamia kile kilichoanzishwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sanasana Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo. Nilishakutaja Mheshimiwa Christina Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama na mimi kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia nami kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Mbili. Vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai wa kutuwezesha Wabunge sote kwa pamoja kuja katika Bunge hili na kuwatumikia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia katika suala la afya. Tumeona ni jinsi gani Mheshimiwa Rais ameweza kutupa dira ambayo itatufanya tufikie katika malengo ambayo tumeyakusudia. Kwa mfano, kwa mwaka 2015 tumeona kwamba mpaka kufikia 2020 Zahanati zimekukwa 1,198, Vituo vya Afya 487 na Hospitali 99.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwani alipokuwa kwenye ziara Mkoa wa Shinyanga, Wilaya ya Kahama, aliipandisha hadhi kuwa Manispaa na Hospitali yetu ya Wilaya ya Kahama inatarajiwa kupanda daraja. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anazidi kujidhatiti katika kuboresha huduma za afya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipengele hiki cha sekta ya afya, nakumbuka kulikuwa na mpango wa MMAM. Mpango huu ulikuwa umekusudia kila Kata kuwa na Kituo cha Afya na kila kijiji au mtaa kuwa na Zahanati. Katika Mkoa wa Shinyanga kuna zahanati nyingi ambazo zimeshafika kwenye maboma. Hivyo, nadhani ni wakati muafaka sasa, ili kutimiza azma na matamanio ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba huduma za afya zinawafikia Watanzania wengi, yale maboma yaweze kumaliziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la afya, tumeona jinsi ambavyo vifo vya wamama wajawazito vilivyopungua kutoka vifo 11,000 mpaka vifo 3,000. Hili tuna sababu kubwa sana kumpongeza Mheshimiwa Rais na watendaji wote wa Wizara ya Afya na wafanyakazi wote wa sekta mtambuka ambao wanahakikisha kwamba huduma ya afya inaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la maji, lakini tumeona dira ambayo Mheshimiwa Rais ameionyesha katika hotuba yake na vilevile kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, nawapongeza sana Wizara ya Maji, hasa Mheshimiwa Aweso kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo ya Maji kuhakikisha kwamba mwanamke anatuliwa ndoo hasa katika Mkoa wa

Shinyanga, Tabora na hata Dodoma kwa kweli sasa hivi shida ya maji siyo kama ile. Tunatarajia kwamba mradi wa Ziwa Victoria utafika na Dodoma na sehemu nyingine. Kwa hiyo, ni suala la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi ambazo kwa kweli anazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, tumeona katika suala zima la uchumi. Ukiangalia katika hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais mwaka 2015 ukalinganisha na hotuba ambayo ameitoa mwaka 2020, tunaona kuna ongezeko la pato la Taifa kutoka 7% kwa mwaka. Pia tumeona makusanyo ya mapato yameongezeka toka shilingi trilioni 94.3 kwa mwaka 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 139. Hivyo tuna sababu kabisa ya kuweka mipango yetu vizuri kwa sababu tunakwenda kwenye bajeti. Katika bajeti ni lazima tuzingatie dira ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa ili tuweze kutekeleza yale ambayo Chama cha Mapinduzi na sisi Wabunge kwa ujumla tuliyaahidi wakati tunaomba kura.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia kuhusu barabara. Barabara ni changamoto sana hasa vijijini. Hata hivyo, kwa mpango madhubuti ambao upo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, naamini kwamba kuja kufikia 2025 barabara nyingi zitakuwa zinapitika na zinafunguka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema kwamba kwa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais, sisi kama Wabunge tuna sababu ya kumpongeza na kuzidi kumwombea kwa sababu vita ya kiuchumi ni kubwa sana. Mheshimiwa Rais naamini halali akiwaza maendeleo ya Tanzania, anatamani kuacha nchi ya Tanzania katika *level* fulani na anatama yale anayoyafikiria yanatimia. Hivyo, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunamwombea.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, niseme kwamba tunapaswa kuendelea kumwomba Mungu hasa katika janga ambalo lipo lakini tunapaswa kuendelea kujikinga kwa sababu Mungu wetu ni mwaminifu, kama ambavyo aliweza kutushindia kipindi kile tukaweza kuepukana na janga hili, ataendelea kutushindia. Nchi za wenzetu wanatamani kuwa

na Rais kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Wanasema laiti tungekuwa tunaweza kubadilishana, basi tungeweza kubadilishana mkatupa Rais Dkt. John Pombe Magufuli hata kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, tuna sababu sanasana sana ya kumshukuru Mungu kwa sababu ya kumpata Rais huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Moshi Kakoso.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu la Kumi na Mbili, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwanza kwa kutuwezesha kufika hapa salama na kutuwezesha sisi kushinda uchaguzi mgumu uliopita.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mbozi Mkoa wa Songwe na Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunichagua mimi kuwa Mbunge. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais sio tu ni dira kwetu sisi Wabunge, nafikiri ni mwelekeo kwa miaka mitano ijayo kwa Taifa letu. Kuna jambo moja ambalo ningependa nijikite ambalo nikuhusu kilimo. Chama chetu Cha Mapinduzi kwa nia njema kabisa kilileta hii sera ya ushirika kwa nia ya kumsaidia mkulima mmoja mmoja ili awe na uhakika wa masoko na bei yake.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi vyama hivi vya ushirika nahisi sijui vina mapepo au vimevamiwa na majambazi, sielewi! Sijaona mahali ambako vyama vya ushirika vimefanya vizuri. Ukienda Kagera, ukija Mbozi, ukienda Mbinga kote ni malalamiko hayo hayo yanayofanana. Kwangu mimi kwenye Jimbo langu la Mbozi vyama hivi vya ushirika sisi kule tunaita *AMCOS,* huwa wakulima wanapeleka

kahawa. Kule kwetu Mbozi, sisi kahawa ndiyo kama dhahabu, sisi hatuna zao lingine tunalotegemea zaidi ya kahawa. Sasa wakulima wakishapima kahawa yao, hawa viongozi wa *AMCOS* wanachofanya, wanakwenda benki kuchukua mkopo bila wale wakulima wengine kwenye vyama vile vya msingi kujua kwamba wale viongozi wamechukua mkopo. Matokeo yake sasa benki inapokuja kufanya malipo inafyeka yale malipo na kuwafanya wakulima waishi katika hali ya umaskini. Hii hali imeendelea kwa kipindi kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda nishukuru juhudi ambazo zimeanza kuchukuliwa sasahivi naOfisi ya TAKUKURU ya Mkoa, ingawa zimekuja kwa kuchelewa lakini bado hatua zaidi, ningependa tunapozidi kufikiria hili suala liingie kisheria. Hawa watu sio tu wafilisiwe nyumba zao, wafikishwe mahakamani na kufungwa. Nafikiri tukiamua kuwa wakali katika hili suala la ushirika na hawa viongozi ambao wanataka kuua ushirika, nafikiri tutakuwa tumemsaidia sana mkulima, kwa sababu kwa muda mrefu sana hawa viongozi wamekuwa wanaishia TAKUKURU tu, wanapewa ratiba ya kurudisha fedha zao, wengine wanahama miji, lakini bado hatujapata *solution* ya kudumu ya kuokoa maisha ya hawa wakulima ambao bado wanaishi katika hali ya umaskini. Kwa hiyo, napenda kuunga hoja hii ya hotuba ya Rais, lakini hili suala la viongozi wa*AMCOS* ni lazima tuje na *solution* ya kudumu ili kuhakikisha kwamba wakulima wa chini wanalindwa kutokana na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, kingine napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais, wakati wakampeni alikuja kwenye Jimbo langu la Mbozi na mimi binafsi pamoja na watu wengine tulimweleza shida ya wafanyabiashara pale Mlowo, Vwawa na Tunduma wanavyopata shida na *TRA.* Rais alikuja tarehe Mosi Oktoba, siku ya Alhamisi. Siku ya Jumatatu yake tarehe 4 alimtuma Kamishna wa*TRA* aje pale Mbozi. Kinachotokea, *TRA* badala ya kuwa rafiki wanachofanya wakikutana na mfanyabiashara wanamkadiria makadirio ya juu kwa mapato yake, kodi ya juu sana kuliko uwezo wake ili tu akae nao mezani waweze kupata kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni kwamba *TRA* imekuwa kama ni fimbo kwa wafanyabiashara na hili ni suala ambalo limekuwa kinyume na maono ya Mheshimiwa Rais. Rais wakati anazindua hili Bunge alisema kwamba angependa *TRA* na wafanyabiashara wawe marafiki, lakini mahali popote unapokutana na mfanyabiashara, adui yake mkubwa ni *TRA.* Kwa kweli hili ni suala ambalo kama kweli unataka kumsaidia mfanyabiashara na kuinua mapato ni lazima hawa maafisa wasio waaminifu wa *TRA,* washughulikiwe.

Mheshimiwa Spika,kwa hiyo kwa kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa George. Nilishakutaja Mheshimiwa Suleiman Moshi Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mwanga Mheshimiwa Tadayo Joseph Tadayo. Mheshimiwa Kakoso, hayupo eeh? Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa sehemu ya Bunge lako hili la Kumi na Mbili kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, nikishukuru sana chama changu Cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini niweze kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi uliopita. Niwashukuru sana wananchi wa Mwanga kwa ushindi mkubwa walionipa wa kura za kishindo.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mwenyezi Mungu anijaalie mimi lakini atujalize sisi sote tuweze kuwatumikia wananchi ipasavyo kwa kuwa utendaji wa Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha miaka mitano ya kwanza pamoja na ushindi huu wa kishindo umeamsha shauku kubwa sana ya wananchi na matarajio makubwa ambayo wanayo. Kwa hiyo Mungu atujaalie tuweze kuyatimiza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya hotuba ya Mheshimiwa Rais na sababu kubwa ni kwamba hotuba hii ni mwendelezo wa hotuba ya 2015 ambayo ilitekelezwa ikatutoa na kutupeleka kwenye uchumi wa kati. Ni dhahiri kwamba tukitekeleza hotuba hii mafanikio yatakayopatikana ni makubwa mno na yatatupeleka mbele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeitazama hotuba hii nikaona pamoja na mambo mengine lakini kwakweli inatusababishia kwenye kushusha chini yale mafanikio makubwa ambayo yalipatikana kwenye miradi mikubwa ya kitaifa yaende yawaguse wananchi na kugusa uchumi wa mtu mmoja mmoja, jambo ambalo ndilo hasa wananchi wanalolitamani na kulitarajia. Naipongeza sana Serikali kwa sababu imeshaanza kutekeleza. Kwenye Jimbo langu la Mwanga tulikuwa na tatizo sugu la maji ambalo matumaini ya kuliondoa yalikuwa yanafifishwa na utendaji ambao ulikuwa hauridhishi wa mkandarasi ambaye kimsingi alikimbia *site* kwenye ule mradi mkubwa wa maji. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa maana alisikia kilio chetu akachukua hatua za haraka za kuweza kusaidia na ule mradi sasahivi unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba iwajali wale wafanyakazi waliokuwa chini ya mradi ule kwa sababu baada ya mkandarasi yule kuususa au ku-*repudiate*ule mkataba na kuondoka wako wafanyakazi ambao stahiki zao hazijalipwa. Naamini kabisa kwamba kwa sababu mkandarasi amekimbia basi endapo kuna chochote anachodai Serikali inayo mamlaka ya kumkata na kuwalipa wale wafanyakazi nahata kama hakuna anachodai bado Serikali inaweza ikawalipa wafanyakazi pamoja na watu wengine waliokuwa wana mikataba na mkandarasi yule na ziko taratibu za kisheria za Serikali ku-*recover* fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwamba kwa kasi hiyo hiyo ambayo imeonekana kwenye miradi hii, basi miradi mingine ambayo iliahidiwa wakati wa kampeni ambayo wananchi wa Mwanga wameiomba sana itekelezwe. Kwa mfano, liko suala la mradi wa hospitali ya wilaya ambayo

Mheshimiwa Rais alituahidi, kiwanja kipo tayari hekari 54, kwa hiyo tunaiomba Wizara husika basi iweze kulitekeleza jambo hilo kwa sababu litakidhi kiu na matamanio makubwa sana ya wananchi wa Mwanga. Pili, iko miradi ya umaliziaji wa vituo vya afya hasa Kituo cha Afya cha Kigonigoni ambacho kwa kweli kiko kwenye mkwamo. Tunaomba Wizara husika ilitazame suala hili.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Wizara ya Ujenzi kwa niaba ya Serikali kwamba kasi ya ujenzi wa barabara katika Jimbo la Mwanga inaendelea vizuri lakini bado ziko barabara, iko barabara ya Lembeni – Kilomeni mpaka Lomwe kilometa 31 ambayo tayari iko chini ya *TANROADS* tunaomba sasa barabara hiyo nayo itazamwe. Iko barabara ya Kisangara – Ngujini – Shingatini kilometa 25.9 na barabara ya Mgagao – Pangaro – Toroha kilometa 35 ambazo katika ngazi ya *road board* na *RCC* zimeshaombewa kuingia *TANROADS.* Tunamwomba Mheshimiwa Waziri husika basi atusaidie barabara hizi ziingie *TANROADS* ili pia ziweze kupata matengenezo kama barabara zingine.

Mheshimiwa Spika, ukienda ukurasa wa 15 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais amezungumzia mkazo juu ya uwekezaji katika sekta ya nyama. Jimbo la Mwanga ni wadau wakubwa pia wa sekta hii ya nyama kwa sababu tunayo mifugo mingi na pia eneo letu *location* yetu iko mahali pazuri kwa ajili ya viwanda vya nyama kwa sababu kuna Bandari ya Tanga iko karibu, kuna Uwanja wa Ndege wa *KIA* na pia tuko mpakani. Nafahamu kabisa kwamba nyama ya Tanzania hasa nyama ya mbuzi ina soko kubwa sana *middle east* huko na nafahamu kabisa kwamba ziko nchi za jirani ambazo huwa zinachukua mbuzi wetu na kuwachinjia kwao na kutoa *certificate of origin* wale mbuzi waonekane wanatoka kwao, lakini ukweli wa mambo wale mbuzi wanatoka Tanzania na wanapata soko zuri nje kwa sababu ya ladha yake. Kwa hiyo, tunaomba Waziri anayehusika kutukumbuka katika uwekezaji kwenye sekta hii ya nyama hasa katika eneo la Kata ya Mgagao ambapo tayari kuna mnada mkubwa unaovuta watu kutoka hata nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ombi hili, ningependa pia niseme kwamba wafugaji katika Jimbo langu kwa sababu wako wanapakana na Mbuga ya Mkomazi wanakabiliwa na changamoto zinazokabili wafugaji wengi wanaopakana na maeneo ya hifadhi. Ni vizuri Serikali ikahakikisha kwamba mipaka kati ya maeneo ya wafugaji na hizi mbuga inaeleweka na wafugaji wapewe elimu inayotosheleza na kwa kweli ni vizuri wakaongezewa maeneo ya kulisha mifugo yao. Ziko faini ambazo wanatozwa pale ambapo mifugo yao imekosea ikaingia kwenye maeneo ya hifadhi. Zile faini ni kubwa mno na kwa kweli zinakuwa ni kama zinawakomoa hawa wafugaji. Wafugaji wanaishi maisha ya mashaka sana katika mipaka na hifadhi ikiwa ni pamoja na wafugaji wa Jimbo langu la Mwanga.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa niaba ya Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kudhibiti suala la…

Mheshimiwa Spika, nasikia kengele imelia. Nakushukuru kwa nafasi hii.

**SPIKA:** Hapana ni kengele ya kwanza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:**Ni kengele ya kwanza, ahsante.

Mheshimiwa Spika, basi kwa haraka nizungumze tu kwamba suala la kudhibiti uwindaji haramu limefanikiwa katika kipindi cha miaka mitano. Hii imesaidia wanyamapori kuongezeka, lakini baraka hii ya wanyamapori kwa baadhi ya maeneo imesumbua sana.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa sana la tembo ambalo limefanya maeneo ya karibu kata tano za jimbo langu yawe magumu sana au yasifae kabisa kwa masuala ya kilimo. Nilimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu akizungumzia juu ya kuweka kambi za hawa Askari wa Wanyamapori katika maeneo ya changamoto kama hizo. Naomba hilo liharakishwe kwa sababu ziko kata tano za jimbo langu

ambazo kwa sasa hivi maisha ni magumu na wako watu kadhaa ambao wameshapoteza maisha kwa ajili ya wanyama hawa tembo.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia kwamba naunga mkono hoja kwa dhati kabisa na tuko pamoja katika kutekeleza haya yaliyomo humuna kuisukuma mbele nchi yetu kwenda kwenye uchumi wa kati wa juu sasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tadayo Joseph, Mbunge wa Mwanga. Mtaona toka tulivyoanza asubuhi katika wachangiaji asilimia 95 au zaidi ni wanaume na wanawake ni chini ya asilimia tano. Sasa una-*tend* kujiuliza Wabunge wanawake tatizo ni nini? Halafu ninyi ndiyo mnasema eti muwe asilimia 50 ya Bunge, litakuwaje?Hebu oneni aibu, niwaseme hadharani kidogo.Haiwezekani hivyo yaani mmekuja kukaa hapa?Hamkuja kukaa hapa. Ulipokuwa unagombea si ulikuwa na*mission* fulani! Mechi imeanza.*(Kicheko/Makofi)*

Sasa kama kweli mmekuja na *mission* nataka mlete vikaratasi hapa ili muokoe angalau akiongea mwanaume, awe na mwanamke. Kama hamleti vikaratasi basi nitakapomaliza *session* hii niwaambie Watanzania, wale watu mliowaleta huku, sio.

Anafuata Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

**MHE. SELEMANI M. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amefanya ndani ya nchi hii. Katika hotuba aliyoitoa yapo mambo ya msingi ambayo aliyasisitiza ambayo na sisi tunahitaji yafanyiwe kazi hasa kwenye maeneo ya watendaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya vitu vingi na vikubwa katika nchi hii, lakini bado kuna eneo moja la kilimo halijawekewa msukumo mkubwa sana. Hili ni eneo ambalo

linawashika Watanzania walio wengi na karibu asilimia kubwa ya ajira za wananchi ziko kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameelezea zaidi kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji. Miradi mingi ya umwagiliaji haijatendewa haki katika nchi hii na ili tuweze kuwa na uzalishaji mkubwa lazima tuwekeze uwekezaji mkubwa kwenye eneo hili. Nchi hii ina mabonde mengi ambayo hayafanyiwi kazi. Tunaweza tukawa wazalishaji wakubwa na tuchukulie mfano tu Mkoa huu wa Dodoma. Mkoa wa Dodoma ndiyo mkoa ambao una ardhi nzuri yenye rutuba sana, kwa bahati mbaya sana mkoa huu mvua zake ni za shida. Sasa kama tungekuwa tumewekeza kwenye eneo la umwagiliaji karibu kila sehemu ya mkoa wa nchi hii ungekuwa na uzalishaji mkubwa sana. Tunaishauri Serikali…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, watu wengi hawafahamu hilo kwamba Mkoa wa Dodoma *of course that means and Singida and a little bit of Shinyanga* ni mkoa wenye ardhi yenye rutuba sana, ni mvua tu! Mvua ikinyesha ukiona hayo mahindi yalivyokaa vizuri utafikiri yamewekewa mbolea ya aina gani.Endelea tu Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. SELEMANI M. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaishauri Serikali iwekeze fedha nyingi za kutosha kwenye eneo la Sekta ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, la pili, hata kama wananchi wengi watawekeza kwenye kilimo na kikawa kinalipa, kama hakuna masoko ya msingi, Serikali haijajikita kutafuta masoko ni kazi bure. Mkulima anapozalisha hawezi kusukumwa, kinachomsukuma ni soko, ndiyo maana mnaona mwaka huu watajikita kwenye kilimo cha mpunga, baadaye watahama wataenda kwenye kilimo cha mahindi, ni kubahatisha kutafuta soko.

Tunaiomba Serikali iwekeze kwenye kitengo cha masoko ilikile kinachozalishwa na wakulima kiweze kuwa na uhakika wa kupata masoko yaliyo mazuri.

Mheshimiwa Spika, tunayo mazao makubwa nchini yanayoingiza fedha nyingi za kigeni. Kwa bahati mbaya sana bado Serikali haijawekeza sana. Tukitaka uzalishaji wa tumbaku, mkonge, pamba ni lazima tuwe na uwekezaji mkubwa na ifike mahali Serikali iwekeze na kuweka ruzuku ya kutosha kwenye mazao haya. Naamini tukifanya hivi, Serikali itakuwa inanufaika kwa kiwango kikubwa, mzunguko wa fedha utakuwa mkubwa na wananchi watanufaika sana, ukata hautakuwepo kwa sababu ni eneo ambalo limeshika walio wengi.

Mheshimiwa Spika, nichangie kwenye eneo la miundombinu. Serikali imewekeza fedha nyingi sana kwenye eneo la miundombinu, lakini ushauri wangu naomba nijikite sana kwenye eneo la *TARURA.*

Mheshimiwa Spika, tulianzisha *TARURA* lakini haina bajeti. *TARURA* inategemea fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zinakusanywa asilimia 100. Kati ya asilimia 100, asilimia 30 ndizo zinazoenda kwenye eneo la *TARURA* na asilimia 70 zinaenda kwenye Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukawa kituko pale ambapo tulianzisha kitu ambacho hakiwi *supported.* Tunaomba Serikali kuu itenge fedha za kutosha, nchi yetu imekuwa kubwa, tuna maendeleo ya kila aina, kila sehemu panahitaji miundombinu ya barabara. Hata hayo mazao tunayozalisha yanategemea barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuna bajeti ya *TARURA.* Kama nilivyozungumza hapa naelewa mfuko ule unaotumika kwenye bajeti ya *TARURA* ni Mfuko wa Barabara tu ambao chanzo chake tumekiweka kwenye eneo la mafuta. Sasa niombe Serikali ifanye kama inavyofanya kwenye eneo la barabara kuu zinazohudumiwa na *TANROADS* ifikie mahali itenge fedha za kutosha ili ziweze kuhudumia barabara. Maeneo haya ni muhimu sana kwa hiyo Serikali iangalie ili tuweze kupata kile ambacho Mheshimiwa Rais anakitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mindombinu ya umeme. Serikali imejikita kupeleka umeme vijijini. Tuna mategemeo makubwa na Serikali kwamba itapeleka miundombinu hiyo.

Naomba Serikali ihakikishe kama Mheshimiwa Rais alivyosema tuhakikishe maeneo yote vijijini yanapata umeme. Tukifanya hivyo tutakuwa tunakuza uchumi kwa kiwango kikubwa ambacho kitawasaidia wananchi. Maeneo mengi bado kwenye vijiji hawajapata umeme ambapo malengo ni kusukuma na kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Tunaomba eneo hili liangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nichangie kwenye eneo la sekta ya afya. Hapa bado tuko nyuma sana kwenye bima ya afya. Niiombe sana Serikali katika kipindi hiki cha miaka mitano tuhakikishe Watanzania wote wanapata bima ili waweze kunufaika na Serikali ambayo imefanya mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali, tunampongeza Mheshimiwa Rais, nami naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana, tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala na utafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pili nikishukuru chama changu na wananchi wa Mbagala kwa ujumla. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri ambayo kwa kweli ukiifuatilia inaenda kujibu kero za wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikijiuliza sana wakati naisoma hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Katika kila neno kwenye hotuba hii ni dhahiri linahitaji fedha ili tuweze kuitekeleza hotuba hii sambamba na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nimekaa nikatafakari sana pamoja na matatizo mengi yaliyokuwepo katika jimbo langu, lakini nimeona mchango wangu nijielekeze sana ni kwa namna gani ambavyo naweza kuishauri Serikali namna ya kupata mapato ambayo mwisho wa siku naamini yanaenda kutekeleza hotuba hii ya Mheshimiwa Rais pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, katika kila eneo nililolisoma nimeona tuna nafasi ya kupata mapato ambayo naona Serikali tulikuwa tunayapoteza. Nianze na suala zima la miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hotuba yote imezungumza namna ambavyo tunaenda kutengeneza barabara na miundombinu mingine. Hata hivyo, nikija katika suala la utenengezaji wa miundombinu iliyopita na inayotaka kutengenezwa, ni dhahiri kuna baadhi ya maeneo ambayo miundombinu imepita yamelipwa fidia. Baadhi ya Wabunge hapa tumeona wakisisitiza ulipwaji wa fidia kwa baadhi ya maeneo ambayo yametwaliwa na Serikali. Pia nimemsikia Waziri wa Ardhi akisisitiza suala la ulipaji fidia maeneo ambayo yanatwaliwa na umma.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa nikaona kuna fedha za Serikali zinapotea. Tunapolipa fidia hatuangalii yule tunayemlipa fidia, hana deni la *land rent* au *property tax?* Kama jukumu la kulipa fidia ile ni la halmashauri basi linaishia kulipa fidia na badaye hamna mtu anayejali madeni haya ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi kabla sijaja hapa nilikuwa Diwani katika Manispaa ya Temeke. Tumelipa fidia ya zaidi ya shilingi bilioni 20 lakini baadaye nikafikiria, je, hawa tuliowalipa fidia hawakuwa na madeni ya *property tax* au *land rent?* Nikaja kugundua ni fedha nyingi sana ambazo tumezipoteza kwa kutokulipa hizi *property tax* na *land rent.* Kwa hiyo, naishauri Serikali washirikiane kati ya taasisi zinazolipa fidia na Wizara ambazo zina mapato yake katika ulipwaji ule wa fidia.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ni katika miundombinu ya ujenzi. Hotuba ya Bunge la Kumi na Moja na hili la Kumi na Mbili tumezungumzia sekta ya maji, barabara, lakini miradi hii tunaenda kuwapa wakandarasi mbalimbali. Nikawa najiuliza, je, wakandarasi hawa wanazilipa halmashauri zetu *city service levy?*

Mheshimiwa Spika, mimi nilijaribu pale Temeke, tulikuwa na mradi ule wa uboreshaji wa Jiji la Dar-Es-Salaam. Makampuni yote tuliowapa tenda za ujenzi zaidi ya shilingi bilioni 600 tulihakikisha zinalipa *city service levy.* Pato la *city service levy* ndiyo lilikuja kuleta maajabu ya kuweza kujenga madarasa 120 kwa mapato yetu ya ndani. Naomba niishauri Serikali maeneo yote ambayo kuna wakandarasi wanafanya kazi za ujenzi, basi tuone namna gani halmashauri zetu nazo wanaenda kuchukua *city service levy* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikaiangalia Wizara ya Ardhi. Wizara ya Ardhi kuna *property tax* ambayo inapatikana kutokana na majengo yanayojengwa kwenye ardhi zile lakini pia kuna *land rent.* Halmashauri na majiji mengi zimepima viwanja lakini vinakaa zaidi ya miaka 10 havijaendelezwa; sheria ipo kwa nini Wizara ya Ardhi viwanja vile wasiwauzie watu wengine ili majengo yale yajengwe na hatimaye tuweze kukusanya *property tax* katika majengo yale?

**SPIKA:** Sheikh Abdallah utaua hapo. Wako wengi humu hapo walishaugulia tayari, endelea Mheshimiwa. *(KIcheko)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, tukitaka tulete mabadiliko ya kweli basi na sisi tunatakiwa tuwe mfano katika kusababisha hayo mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye sekta ya afya, tumemsikia Waziri hapa asubuhi akisema kuna zahanati moja ilitumia shilingi milioni 40 kununua dawa na ilivyokuja kutoa huduma ikapata zaidi ya shilingi milioni 100, lakini wakaja kununua dawa za shilingi milioni 20. Ni wajibu wetu sasa Wabunge kwenda kufuatilia vitu kama hivi. Tunapofuatilia

maana yake malalamiko madogomadogo yanakuwa yanapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye elimu, Serikali yetu imejitahidi sana kuboresha miundombinu ya elimu, lakini yapo makampuni yanaendeleza maeneo kwa kujenga ma-*real estate.* Kwa mfano, *NSSF* pale Tuangoma wamejenga nyumba nyingi na wakatuletea wananchi wengi lakini hatuwaoni *NSSF* kusema hata tunajenga shule moja tukaiita hii ni *NSSF Primary School,* hawafanyi hivyo. Pia hata maeneo mengi ambayo wamekuwa wakiyamiliki hawayaendelezi kwa muda mrefu. Tukiwaomba maeneo yale basi mtupe maeneo fulani tujenge shule za msingi, sekondari na vituo vya afya, nayo imekuwa mgogoro.

Mheshimiwa Spika, niombe sana, pamoja na kuichangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais lakini vilevile tupate nafasi kubwa ya kuona ni sehemu gani mapato ya Serikali yanapotea na tuweze kuyadhibiti ili hotuba hii na utekelezaji wa Ilani uende kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie, nimeona halmashauri nyingi zikiandika miradi ya kimkakati lakini leo kwenye hotuba ya Rais nimeona kuna mazao ya kimkakati. Nikajiuliza, je, kwa nini katika ile miradi ya kimkakati halmashauri ambazo zina uwezo wa kulima zisiandike andiko la kuomba fedha ili wakalima mazao ya kimkakati ya kihalmashauri ikawa ni moja ya vyanzo vya mapato?

Mheshimiwa Spika, nitakutolea mfano mdogo tu, Halmashauri ya Lindi. Halmashauri ya Lindi imegawa maeneo kwa ajili ya wananchi kuwekeza. Katika semina ile ilikuwa inaeleza mtu ukiwa na ekari 200 ukaweza kupanda mikorosho baada ya miaka mitatu una uwezo wa kila mwaka kupata shilingi bilioni moja. Je, halmashauri ingefanya yenyewe ikatafuta mashamba yake ikachukua ekari 100, ekari 500, ikaomba fedha serikalini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chaurembo kwa kutugawia uzoefu huo mzuri sana. Nimeshamtaja Mheshimiwa Tabasam na atafuatiwa na Mheshimiwa Mpembenwe. Huu mpira unachezwa na wanaume tu. Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ni miongoni mwa hotuba tamu sana katika nchi hii. Hizi hotuba za kishujaa hazitakiwi kuachwa bila kujadiliwa wala kusifiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameonesha ushujaa mkubwa sana ndani ya miaka mitano. Nimeangalia hotuba ya miaka mitano, nikaangalia na hotuba hii aliyoitoa juzi anafungua Bunge la Kumi na Mbili, mimi binafsi naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusiana na suala la mifugo. Katika mifugo Mheshimiwa Rais amesema kwamba wafugaji katika nchi hii sasa wana nafasi kubwa ya kupewa maeneo ya kupata vitalu, lakini waandaliwe sera nzuri kwa ajili ya kuacha kwenda kuchunga mifugo kwa aina ya zamani sana. Leo wafugaji wanatembea kuchunga wakati tunayo ardhi kubwa ya kutosha tungeweza kuzalisha nyasi, tunayo mabua ya mahindi yanapatikana kila mkoa, kwa nini wasitengeneze sera nzuri kwa ajili ya mifugo yetu?

Mheshimiwa Spika, leo wafugaji wanahamishwa kama hawapo kwenye nchi yao. Kila siku kesi zinakuwa nyingi, ukiangalia taarifa ya habari ni migogoro mikubwa ya wafugaji. Katika hili kama utaandaliwa mfumo mzuri sisi pamoja na kuwa nchi ya pili kwa ufugaji katika Afrika, tutakuwa nchi ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwenye hili suala la nyama, wananchi wa Tanzania hawajahamasishwa kula nyama. Mwananchi mmoja anatakiwa kwa kiwango cha chini ale kilo, ana hali mbaya nusu kilo, lakini akila hata robo kilo tu soko la nyama peke yake halitoshi katika nchi hii. Sisi wenyewe tunakuwa ni soko kubwa sana la nyama, kwanza tuanze kula sisi nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la maeneo haya ya malisho. Ni kwamba wakikata vitalu na hawa wafugaji wakapewa maeneo ya kwenda kuchunga kwanza ni walipaji wazuri kwa wakati. Leo katika nchi hii mifugo imeenea nchi nzima na miongoni mwa wafugaji ambao wanapata tabu, lazima tuwe wakweli, ni Wasukuma na Wamasai. Tumekuwa tunakwenda kila kona unahamishwa unaondoka, sasa hii imekuwa ni hatari. Kwenye hotuba hii tunakwenda katika uchumi wa kati, nafikiri Waziri wa Mifugo na Waziri wa Sheria waliangalie jambo hili tuwe huru katika nchi yetu katika suala la mifugo.

Mheshimiwa Spika, sasa niende upande wa kilimo cha pamba. Nchi hii pamba inalimwa katika mikoa 11. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais ametembea nayo katika kampeni, anasema tunahitaji kuzalisha tani milioni moja, tuna uhakika wa kuzalisha zaidi ya tani milioni tatu lakini ni kama pamba itaokolewa na Serikali kwa dhamira ya kweli.

Mheshimiwa Spika, Kwa mfano, kama tumeweza kuokoa Shirika letu la Ndege leo liko hai kwa nini tusiokoe pamba yetu ya Tanzania kwa mambo matatu tu? Jambo la kwanza ni kwamba pamba hii ya nchi yetu itumike kwenye kuzalisha nyuzi na kutengeneza nguo katika nchi hii. Serikali inunue viwanda vya nyuzi na nguo halafu uone kama kilo moja ya pamba haitauzwa Sh.2,000 mpaka Sh.5,000 kwa kilo. Hii nguo niliyovaa mimi leo inauzwa Sh.170,000 au Sh.150,000 ukipata kwa gharama nafuu wakati haina robo kilo ya pamba. Sasa tunaonekana watu wa ajabu, ni lazima tumsaidie Mheshimiwa Rais na tuweke dhamira ya kweli, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kupiga marufuku kuuza pamba kwa robota, kwa sababu uuzaji huu wa pamba wa robota unaifanya nchi hii inakuwa mtumwa, wanatuchezea katika maeneo makuu. Wanatuchezea katika mbegu, tunazo nchi zinazolima pamba katika Afrika; Burkina Faso ukiangalia Mali, Sudan, Misri, Zimbabwe na ukiwaona wenzetu Waganda leo wanakwenda kuchukua pamba ya Msumbiji wanasema ni miongoni mwa pamba bora katika Bara la Afrika hii yote ni kutuchezea akili, lakini kama tutakuwa tuna viwanda vyetu hatuwezi kuulizwa hilo jambo kwasababu pamba ni kilimo cha mabepari.

Mheshimiwa Spika, mbegu katika nchi hii hivi viwanda vya pamba vilivyopo huwezi ukailinda mbegu, unaweza ukatoa maelekezo kwamba mbegu ya kupandwa katika nchi hii inalimwa Igunga...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Hii kengele na yenyewe tena, basi bwana.

**SPIKA:** Ya kwanza hiyo.

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Sawa. Hapa nipo mahali patamu sana basi tu.

Mheshimiwa Spika,suala la mbegu haliwezi kulindwa na wafanyabiashara, suala la mbegu litalindwa na Serikali, lakini suala la pembejeo, mbegu na dawa na pamba ina muda ina *timeframe,* mwisho wa kupanda mbegu ni tarehe 15 mwezi 12, lakini mbegu inafika Januari, hizi dawa baada ya kupulizia, roho inaniuma muda unakuwa ni mdogo, sijui nifanyeje kuhusiana na suala la pamba. Serikali imerudisha viwanda vyetu vya Nyanza, *SHIRECU,* halafu tunashindwa kuiokoa pamba, zaidi ya wananchi milioni 16 ndiyo roho yetu.Mheshimiwa Rais tutamsaidiaje katika hili maana yake roho inatuuma, tuokoleeni pamba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasamu. Unapaswa kuchangia ukitabasamu.

Kwenye eneo hili la mifugo na uchungaji sijui mimi huwa nawaza kwamba Serikali ikitoa kodi sijui au nini kwenye seng'enge, migogoro mingi sana hata ya mkulima kwa mkulima, mipaka au wafugaji na wakulima kwa maeneo mengi migogoro hii itapungua kwa asilimia kubwa sana. Kwasababu uchungaji wa kuzurura tu nchi nzima kwa vyovyote vile siyo mzuri kwa vyovyote vile, kwasababu sasa tuko milioni 60, miaka 20 ijayo watakaokuwepo itakuwa 90 au 100 yaani haiwezekani. Ndiyo maana hukuti matatizo haya ya wakulima na wafugaji na nani, huwezi kuyakuta Zambia hapo, Zimbabwe, Kenya hapo kwasababu wenzetu wana *fence,* ukishakuwa na ardhi yako *you fence it*. Kwahiyo migogoro ya kwamba huyu kaingia kwenye mpaka sijui ngombe, sijui nani kafanyaje, migogoro yote inaisha.

Sasa sisi hata Ranchi za Taifa haziko *fenced,* yaani pako wazi tu kwahiyo matokeo yake hata ukipata hicho kitalu unachosema, kesho yake unakuta ng'ombe wa watu wamejaa huko, keshokutwa unakuta mtu kaanzisha shamba katikati ya kitalu chako, unakuwa ni mtu wa migogoro tu, kazi yako kuwa kwenye mahakama za ardhi kila kukicha, lakini vi-*fence fence* hivi tukianza navyo kidogo kidogo, itasaidia sana ku-*secure,* kila mtu kwenye kaeneo kake, kama mko ushirika mna eneo lenu, basi mtafuga au mtalima kufuatana na eneo lenu mlilonalo, hii itapunguza sana migogoro. Najua watu hawaipendi *fence* lakini ndiyo yenyewe inayotatua matatizo kwa kiasi kikubwa.

Nilimtaja Mheshimiwa Seif Mpembenwe na atafuatwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuwa mchangiaji katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Naomba tu kidogo nifanye marekebisho hapo jina langu naitwa Twaha

Mpembenwe, Seif Mpembenwe alikuwa mzee wangu na tayari ameshatangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi, wapiga kura wa Jimbo la Kibiti kwa heshima kubwa sana waliyonipa mimi na familia yanguna leo hii niko hapa mjengoni nawashukuru sana. Sambamba na hilo, naomba vilevile nichukue fursa hii kuwashukuru watu muhimu sana katika maisha yangu hasa rafiki yangu mpenzi ambaye ni mke wangu mama Sabrina; wanangu Sabrina, Leyla, Naima na Najma. Nawashukuru sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoweza kutoa shukrani za dhati kwa aliyekuwa Mkuu wangu wa Wilaya lakini sasa hivi ndiye Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Joseph Joseph Mkirikiti pamoja na Katibu Tawala wangu wa Mkoa, mama yangu Rehema Madenge wakati nafanyakazi chini yao walikuwa viongozi wazuri na waliweza kuniongoza vizuri na mpaka leo nimekuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Pwani ni wakarimu sana, halafu tuna desturi ya kuweza kushukuru. Sasa kabla sijaanza kuichangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ningependa kuanza kumshukuru Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa mambo makubwa na mazuri aliyoweza kutufanyia watu wa Jimbo la Kibiti.

Mheshimiwa Spika, katika sekta nzima ya afya katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020 Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliweza kutupatia fedha takriban shilingi 4,021,493,500,fedha hizo ziliweza kutumika katika kuweza kujenga hospitali ya wilaya, vituo viwili vya afya, zahanati tisa na vilevile tumeweza kukarabati kituo chetu cha afya kikongwe cha pale Kibiti. Tunashukuru sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya elimu,Mheshimiwa Rais aliweza kutupa fedha takriban shilingi 4,243,607,588.99,

fedha hizi zimeweza kutumika katika kuweza kujenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za Walimu na kuweza kukarabati vilevile shule yetu kongwe ya Kibiti Sekondari ambayo ninauhakika kabisa baadhi ya Wabunge hapa wamepita na kuweza kusoma katika shule ile.

Mheshimiwa Spika,kama hivyo haitoshi Mheshimiwa Rais ametufanyia lingine kubwa ameweza vilevile kutupa fedha takriban shilingi bilioni 14.3 katika Kata ya Salale katika Wilaya ya Kibiti pale katika Kijiji cha Nyamisati limejengwa Gati zuri ambalo kwa namna moja ama nyingine limeweza kuturahisishia sisi watu wa Kibiti pamoja na ndugu zetu wa Mafia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili vilevile naomba ku-*declare specialinterest,* katika gati lile limeweza kuturahisishia sana sisi watu wa Kibiti kwasababu kule Mafia kuna akinamama kule wa kiarabu arabu na sisi watu wa Kibiti tunakwenda kule kwenda kuoa sasa kuweza kuchanganya mbegu zile. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rais ameweza kutupa fedha takriban shilingi 4,021,850,786.38 fedha hizi zimeweza kutumika katika kuweza majengo ya utawala majengo yale ni mazuri jengo kubwa la Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji, bado kuna fedha kama shilingi milioni 700 tumeweza kuziomba kwa Serikali Kuu ili tuweze kumalizia katika miundombinu masuala mazima ya umeme na maji ili wananchi wale sasa waweze ku-*enjoy* kuweza kumchagua Mheshimiwa Raisna kuweza kuwa na Mpembenwe kama Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, shukrani hizi bado zinaendelea katika Jimbo letu la Kibiti limegawanyika katika sehemu kubwa mbili kuna sehemu ya geta na sehemu ya juu huku. Katika sehemu ya geta kule Mheshimiwa Rais aliweza kutupa fedha takriban shilingi bilioni 2.5, fedha zile katika kujenga daraja, kuna mambo mambo yaliweza kutokea lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ndugu yangu Mheshimiwa Selemani Jafo aliweza kutia mguu, sasa

hivi ninavyoongea wakandarasi wako *site,* mkandarasi aliyekuwa amejenga gati la Nyamisati ndiyo yuko kule shughuli zinaendelea na vijana wetu pale vilevile wameweza kufunguliwa fursa za ajira, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kubwa kuliko yote tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuturudishia amani ambayo ilikuwa imepotea katika Jimbo la Kibiti. Jimbo la Kibiti amani ilikuwa ni bidhaa adimu sana. Nataka nieleweshe tu kwamba kuku walikuwa na uhuru mkubwa sana kuliko mwanadamu wa kawaida katika kipindi cha mwaka 2018/2019, lakini Mheshimiwa Rais aliweza kusimama katika nafasi yake kama Amiri Jeshi Mkuu na kuweza kuturudishia amani hiyo. Tunamshukuru sana katika hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo katika Bunge hili la Kumi na Mbili tumefarijika sana kwasababu tuna kiongozi vilevile wa Chama Cha Mapinduzi naye siyo mwingine ni komredi Humphrey Polepole. Nataka niombe vile vile nichukue nafasi hii dakika moja kuelezea utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika Jimbo la Kibiti katika kipindi cha uchaguzi mpaka hivi sasa. Hivi ninavyoongea baada ya kuweza kuwasiliana na wadau mbalimbali nimeweza kufanikiwa kupata fedha shilingi milioni 175 kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji kwa ajili ya kununua *ambulance*. Fedha hizi zipo sasa hivi katika akaunti ya Mkurugenzi Mtendaji, tukimaliza *session* hii tu nitamwona Waziri wa Fedha ili tuweze kuweka mustakabali mzima wa masuala ya *exemption* tuweze kuleta *ambulance* ile na wananchi wa Kibiti sana waweze kufurahia kuwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli lakini vilevile kuwa na Mbunge mbunifu ambaye ni Mpembenwe.

Mheshimiwa Spika, kama hivyo haitoshi wakati tukiwa vilevile katika suala zima la kampeni, nilipita huko vichochoroni, nimeweza kuhangaika kwa wadau wangu mbalimbali kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji ninavyoongea tumeweza kupata fedha shilingi milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa *dispensary* fedha hizo zipo kwa Mkurugenzi

Mtendaji wakati wowote kuanzia sasa hivi *dispensary* ile itajengwa kwa kupitia *force account*. Hilivilevile linafanyika.

Mheshimiwa Spika, kama hivyo haitoshi vile vile naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu pamoja na kiongozi wetu komredi Humphrey Polepole, madawati 100 tayari yalishasambazwa katika Jimbo la Kibiti na hivi ninavyoongea kuna madawati mengine 500 wiki tatu zijazo yatasambazwa katika shule za msingi vilevile pamoja na shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pia naomba tu niseme tutaanza ujenzi wa kituo cha Polisi haraka iwezekanavyo kwa kutumia nguvu zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais mimi sitaki kwenda mbali nasema machache tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha sasa hotuba ya Rais sasa. *(Kicheko)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sanakatika kuichangia hotuba ya Mheshimiwa Rais mimi nagusa sehemu tatu muhimu. Kwanza katika suala zima la kilimo, najua Wizara ya Kilimo inafanyakazi nzuri sana. Napenda vilevile kumshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Bashe kwa hotuba nzuri sana ambayo aliitoa siku alipofanya mkutano kule Tabora *you real*kneeled down,nilijaribu kumpigia simu lakini hakuweza kupatikana. Nampongeza sana kwa hotuba nzuri na mikakati mizuri ambayo Wizara ya Kilimo sasa hivi wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo kuna shida kubwa sana katika suala zima la bei ya korosho. Bei ya korosho na ufuta kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani hususan katika Jimbo la Kibiti imekuwa ni mtihani mkubwa. Sisi tuna watoto wetu wa asili Wamwera, Wamakonde na Wayao kule, wao wanauza kilo moja ya korosho gredi A shilingi 2,700 wakati mwingine, lakini inashangaza sana kuona kwamba baba zao sisi watu wa Kibiti, kilo hizo za korosho gredi A inauzwa shilingi

800. Kwa hiyo naomba niishauri Serikali sasa tuweze kuangalia mustakabali mzima katika kuweza kuangalia minada hiyo wakati inafanyika, ifanyike kwa pamoja kwasababu minada ikiwa inaanza kule kusini halafu baadaye inakuja huku katika Mkoa wa Pwani, inakuwa shida sana, ndiyo wale wanunuzi wanaanza kufanya *illegal price fixing,* wakati mwingine wanakuja kununua korosho kwa bei ya chini. Mpaka hivi ninavyoongea sasa hivi bado kuna korosho chungu nzima za wananchi wanahangaika nazo kule.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nichangie katika sekta nzima ya mambo ya elimu. Tuna wajukuu zetu hawa sasa hivi wana miaka sita elimu bila malipo imeweza kuonyesha kwamba watoto wengi sana wameweza kusajiliwa kuingia Shule ya Msingi, ikifika mwakani tayari watoto hawa watakuwa wamesha-*mature* miaka saba imetimia. Kwa tafsiri hiyo tusipokuwa makini elimu bila malipo inaweza ikageuka ikawa *timing bomb*.

Naomba sasa kuishauri Serikali, tuweze kwa namna moja ama nyingine kuwaongezea nguvu watu wa Halmashauri turudishe baadhi ya makusanyo, vyanzo vya mapato viende kwao, hivi sasa wawe na mpango mkakati wa kuweza kutengeneza vyumba vya madarasa. Tukifanya hivyo tafsiri yake pana ni kwamba tutakuwa na uwezo mkubwa sana wa kuweza kufanikisha watoto hawa kuingia Sekondari na bila ya *crisis* ya namna yoyote.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nilichangie ni katika sekta nzima ya masuala ya uvuvi, nashukuru kwa kengele lakini bado dakika zinaendelea. Katika sekta hii ya uvuvi ..

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Delta.

**SPIKA:** Ooh,muda hauko upande wako Mheshimiwa twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:**Mheshimiwa Spika, nashukuru nanaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Twaha Mpembenwe kwa mchango wako. Pia suti yako ni ya kiwango hongera sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Hassan Omar King kutoka kule Zanzibar.

**MHE. ALI J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kuniona. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake mbalimbali anazotujaalia, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumuumba mja wake Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na akamjaalia kuwa Rais wa nchi hii na yeye akaitendea haki nchi hii kwa kufanya mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ndiyo mara yangu ya kwanza pia kusimama katika Bunge lako hili,nikishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuniteua na kunifanya kuwa Mbunge. Pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kondoa Mjini kwa kuniamini na kunipa kura nyingi za kishindo na mimi kuwa mwakilishi wao.Ahadi yangu kwao ni kwamba tutafanyakazi kwa bidii kubwa kuhakikisha tunaleta maendeleo kwa wananchi. Vile vile niishukuru familia yangu mama Hashim na watoto wangu wawili kwa kuendelea kunipa nguvu katika kufanyakazi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba zote mbili za Mheshimiwa Rais ile ya 2015 na hii kwa kweli hotuba zote mbili hizi zimejaa kila aina ya miongozo kwa ajili ya kulilete a neema Taifa hili. Ukweli ni kwamba pamoja na michango yetu yote tutakayochangia bado haitoi maana ya kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano, imefanya mambo makubwa sana katika Taifa hili. Hivyo basi, katika kuchangia mimi nitakwenda ukurasa wa 10, Wizara ya Afya. Serikali ya Awamu ya Tano imepunguza kwa kiwango kikubwa sana vifo vya

mama wajawazito na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano. Kama tutamsaidia Mheshimiwa Rais kikamilifu basi tutaendelea kupunguza vifo hivi, lakini kama tutazembea, hatutaweza kumsaidia Mheshimiwa Rais, bado vifo hivi vitaendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, kwenye hiki kifungu cha akinamama wajawazito kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wananchi kwamba sera za afya na Ilani ya CCM, utekelezaji wa sera unakinzana na Ilani ya CCM, Ilani ya CCM inaelezea kwamba tutaendelea kutoa huduma bure kwa akinamama wajawazito na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano,lakini uhalisia haupo hivyo. Akinamama wamekuwa wakitozwa gharama katika kujifungua na akinamama wengi katika ziara zangu wamekuwa wakizungumza wengine wameamua kusimamisha kujifungua kwasababu ya gharama kubwa za afya.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali za kupunguza vifo zinaweza zikawa zinamikwamo kwasababu wapo akinamama ambao wameamua kujifungulia majumbani kwasababu wanaogopa kwenda kujifungua hospitali wakiogopa gharama. Sasa kama hili litaendelea na wakahamasishana akinamama basi juhudi za Serikali za kupunguza vifo hivi zitakuwa zimekwama.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kondoa Mjini linaeneo ambalo limetengwa naMto Bubu. Miezi miwili iliyopita tumepata kesi za vifo, mama mjamzito akisubiria maji yapungue aende hospitali kujifungua maji hayakupungua akajifungulia upande wa pili wa barabara, mtoto akafariki,mama wakawa wanamkimbiza wampeleke Hanang, yule mama pia akafariki.

Kwa hiyo kutokana na hali hii iko haja ya Serikali kuona namna gani wanaweza wakasaidia ng'ambo ile ya Kata ya Serya ambayo haina kituo cha afya wala zahanati na wakati huo huo hawana uwezo wa kipindi cha masika kuja mjini kwaajili ya kutafuta huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kero kubwa sana katika maeneo hayo ambayo yanazungukwa na huo Mto Bubu. Kwahiyo ombi letu watu wa Kondoa tunaomba aidha yafanyike mambo mawili katika moja; kulijenga lile daraja ili watu waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi pamoja na kupata huduma za afya au kujenga kituo cha afya katika maeneo yale ya Serya.

Mheshimiwa Spika, eneo la kilimo wako wananchi ambao mashamba yao yaliharibiwa na tembo na wakaahidiwa muda mrefu sana watalipwa kifuta jasho. Mpaka leo watu wale wanadai, hawakulipwa fedha zao, lakini wananchi wa Kondoa wanalalamikia suala la kulipwa kifuta jasho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Makoa, tembo walifika Kondoa Mjini?

**MHE. ALI J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, jimbo langu lina maeneo ya mjini na vijijini. Ipo Kata ya Kingale na Kata ya Serya ipo pembezoni mwa Hifadhi ya Swagaswaga. Kwa hiyo, tembo wale waliharibu mashamba ya watu lakini vifuta jasho wanavyopewa haviendani na thamani ya mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kupata mabilionea kupitia wakulima basi Wizara ione haja sasa ya kuangalia uwezekano wa kudhibiti tembo wale na kuwalipa wananchi fidia ya maeneo yao na siyo vifuta jasho. Kwa sababu kifuta jasho analipwa pesa ndogo sana ni bora alipwe fidia ili ile dhana ya kuwa na mabilionea kutokana na kilimo basi ipatikane.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni ajira kwa vijana. Serikali yetu imefanya vizuri sana kutenga asilimia 10 kwa ajili ya vijana. Hata hivyo, katika sera ya mfuko ule nashauri kwamba akaunti ya mikopo ya vijana ingetofautishwa na akaunti zingine za halmashauri ili wakati wa kupanga bajeti ya kuviwezesha vikundi asilimia 10 ya bajeti ya mwaka huu iwe inaendana na zile asilimia 10 zilizopita ambazo

zimerejeshwa. Tofauti na ilivyo sasa asilimia 10 inayofanyiwa hesabu ya *current year* lakini yale marejesho yanaingia kwenye akaunti ya maendeleo. Kwa hiyo, tunashindwa kujua uhalisia hasa marejesho yamekuwa ni kiasi gani na asilimia kumi ya safari hii ni kiasi gani ili kuwawezesha wale vijana, kinamama na walemavu kuweza kupata fedha ambazo zitawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaona vikundi vingi ambavyo vinapewa mikopo utakuta watu kumi wanapewa shilingi milioni 10, ukipiga hesabu ni shilingi milioni moja moja unashindwa hata kuwashauri wale vijana wafanye biashara gani. Mikopo hii maeneo mengi imekuwa siyo neema kwa vijana, wengi wamekimbia nyumba zao, wameshindwa kulipa madeni kwa sababu wanapewa mikopo kabla ya kupewa elimu ya kuifanyia kazi mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwa namna ambavyo imefanya juhudi kubwa ya kujenga miundombinu ya barabara. Hata hivyo, kilio kilekile cha wananchi ni kwamba kipindi hasa hiki cha masika barabara nyingi hazipitiki. Kwa jimbo langu eneo ambalo linashughulikiwa na *TANROADS* mpaka sasa ni kilomita kama 0.8. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwa miaka yote mitano *TANROADS* wanaweza wasitie mkono au mguu katika jimbo langu. Eneo kubwa linachukuliwa na *TARURA*, uwezo wa *TARURA* ni mdogo kwa maana hiyo, tunaomba *TARURA* waongezewe nguvu kwa sababu barabara nyingi sasa hivi zinashikwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini kwa mchango wako. Mheshimiwa Makoa alizungumzia habari ya huduma ya wamama wajawazito, inanikumbusha mara kadhaa ukikutana na vijana jimboni huko wanakuambia afadhali Mheshimiwa tumekutana daah! Unamuuliza nini tatizo, anakwambia mke wangu mjamzito yaani ndiyo wameshamuingiza huko wodini,

sasa kwa kuwa tumeonana hebu fanyafanya hapo kidogo tuokoe jahazi. Unamwambia aisee! Kwa hiyo, ni mjamzito yuko labor huko, anasema eeh kabisa. Kwa hiyo, sasa unamaanisha nini? Nina maana fanyafanya kidogo fedha kidogo, haya unamwambia mwenzangu una ngapi? Anasema hapa unaponiona hata shilingi sina. Sasa unawaza Mungu aliweka viashiria vyote wewe miezi tisa hata shilingi huna, huna maandalizi yoyote mpaka ukutane na Mbunge na kadhalika basi ubunge mgumu wakati mwingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ally Hassan King, huyu Mbunge ni maarufu sana kwa Wabunge wageni mtamfahamu tu atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu. Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kutusajili siku ya leo kuwa miongoni mwa viumbe ambao wana uhai na wana afya. Pili, nikushukuru kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya Rais ambayo ameitoa mwezi wa 11 wakati wa kufungua Bunge.

Mheshimiwa Spika, lingine nikishukuru chama changu na wananchi wa Jang'ombe kwa kunijalia kurudi tena hapa Bungeni kwani si kazi ndogo kufikia ukarudi. Kwa hiyo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea kuliongoza Taifa hili hali ya kuwa tuko katika uchumi mzuri na katika utulivu na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu mwanzo nitajikita katika ukuaji wa uchumi. Mheshimiwa Rais ametuongoza katika kukuza uchumi na ameeleza katika ukurasa wa 18 kwamba kila mwaka uchumi wetu ulikuwa ukikua kwa asilimia 7 kutoka 2015 hadi 2019 hata na hii 2020. Imeonyeshwa hapo kutoka shilingi trilioni 94.4 mpaka kufikia shilingi trilioni 140 maana yake ni kwamba katika miaka mitano hii tumeongeza

karibu ya *one third* katika *GDP* yetu ambayo imeanza tokea miaka ya nyuma. Kwa hiyo, katika kipindi cha miaka mitano tumefikia hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuko katika uchumi wa kipato cha kati lakini pia Mheshimiwa Rais amesisitiza kwamba tunataka kuendeleza ukuaji wa uchumi na ndipo katika eneo hilo ninapotaka mimi kuchangia. Katika eneo hilo nataka nijikite zaidi katika uvuvi wa bahari kuu. Kuna msemo wa wahenga wanasema mtemewa mate na wengi hulowa, kwamba lilishazungumzwa hili eneo la uchumi wa bahari kuu lakini na mimi nalirejea tena kulizungumza kwa umuhimu wake ili lipate kutiliwa mkazo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 35, 36 na 37 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ameelezea kwamba ana azma ya kukuza pato la Taifa kwa kuimarisha uvuvi wa bahari kuu lakini pia ameelezea mapato ambayo tunayapoteza ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 350, lakini pia ameelezea makusanyo ambayo sasa hivi tunapata kupitia uvuvi wa bahari kuu kwa sababu tunafanya katika ufinyu wake tunapata shilingi bilioni 3.3 kila mwaka. Kwa hiyo, tunapoteza shilingi bilioni 352 kila mwaka lakini tunachopata sasa hivi kutokana na ufinyu wa uchumi wa bahari kuu tunavyoutumia ni shilingi bilioni 3.3. Taarifa hizi ni rejea za ripoti ya Bunge la Kumi na Moja, tunakupongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kulisimamia hili na data hizi sasa hivi zinatumika huko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameeleza kuwa miaka hii mitano atasimamia vizuri uchumi huu. Pia katika shughuli hii ya uvuvi wa bahari kuu tayari sheria yake imeshapitishwa na Bunge lako Tukufu lakini pia Rais amepanga kununua meli nne Tanzania bara na meli nne Zanzibar. Pia kujenga bandari moja kubwa ya uvuvi itakayoajiri zaidi ya watu 30,000. Vilevile atahamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kuchakata samaki ambapo huko ajira zitazaliwa.

Mheshimiwa Spika, haya ni maelezo ambayo yako katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, sasa ushauri wangu. Ili

tufaidike kikamilifu katika fursa hii basi ni lazima tuwekeze katika ukamilifu wake, tusipowekeza katika ukamilifu wake zile faida tunazozifikiria kwamba tutazipata hatutoweza kuzipata. Soko la samaki linategemea mazingira ya samaki tokea anavyuliwa, bandari gani amepokelewa, *store* gani amehifadhiwa na mengine mengi ambayo yako katika *facilities* katika uvuvi huu wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kiufupi *facilities* zote zipatikane ndiyo tutafikia katika haya maono ambayo Mheshimiwa Rais ameyaona na ndipo tutafikia katika ripoti ambayo imetolewa na Bunge hili kwamba tukiwekeza katika bahari kuu tutafaidika na hayo. Sasa ili tufaidike na uvuvi huu tuangalia *resources* tutapata wapi? Serikali peke yake haitotosha kutoa *resources* zake kwa ajili ya kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu. Kwa hiyo, *inputs* ni lazima tuchanganye kutoka katika sekta ya umma, sekta binafsi, lakini pia katika mchanganyiko wa sekta ya umma na sekta binafsi yaani ubia (*PPP)*. Pia siyo makosa tukawaalika wenzetu wa nje wakaja wakatusaidia katika uwekezaji kwa sababu hii sekta inatakiwa kufanywa katika ukamilifu wake. Pia siyo vibaya kupata uzoefu kutoka katika mataifa mengine wanafanyaje wenzetu mpaka wanafaidika na mambo hayo?

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa kuwa Rais amesema na kwa kule Zanzibar atanunua meli nne, ina meli nne hazitoweza kufua dafu hizo meli zitavua lakini wapi tunaweza kupeleka itakuwa hakuna kwa kupeleka kwa sababu hakuna bandari na ikiwa hakuna bandari hiyo hata viwanda vya kuchakata havitakuwepo na hivyo kufanya *marketing* yake samaki hao itakuwa ni vigumu, kwa hiyo, hii fursa tunaweza tukaikosa. Sio vibaya na sisi tukawa na dhana au *aspect* hii ya uchumi wa *blue* tukiwa na huo uchumi wa *blue* nao pia unaweza ukatusaidia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, Mheshimiwa Rais katika ukurasa wa 62 na 63 ametambua shughuli nyingi sasa hivi zinafanywa kwa kutegemea TEHAMA. Kwa hiyo, TEHAMA ameipa kipaumbele na ameeleza katika kurasa hizo kwamba amepanga kuongeza wigo wa matumizi wa mawasiliano ya

kasi lakini pia kufikisha miundombinu ya mkongo wa Taifa ameeleza ili iwafikie wananchi wengi wa Tanzania na mambo mengine mengi ameeleza katika kurasa hizo ambayo yanahusiana na mambo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya ambayo Mheshimiwa Rais amesema, nampongeza sana ameweka Wizara inayoshughulikia masuala ya TEHAMA. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna dhana ya *digital economy*, hapo ndiyo kwenye hoja yangu mimi, pamoja na uwekezaji huu hivi sasa kutokana na *digital economy transactions* nyingi sana zinafanyika *online* kwa maana hiyo tunakosa kukusanya mapato kikamilifu kutokana na dhana hii. Sasa hivi hapa ukienda katika makampuni mengi unaweza ukaagiza unachotaka, ukalipa na ukaletewa lakini Serikali haipati kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia mfumo huu wa TEHAMA, naomba Serikali ijaribu kuangalia katika eneo la ulinzi na usalama kwanza lakini pia Serikali ikasomeshe vijana hapa tunakosa vitu vingi sana ambavyo vinatokana na *tax* zinazopatikana kutokana na hizo *transactions* zinazofanyika *off show*. Tusiseme watu wasifanye hiyo biashara ya *off show* lakini mpiganaji mzuri ni yule mtu anayemfuata mtu angani kuliko kusema umpopoe mawe aanguke chini um-*charge* huku chini. Kwa hiyo, Serikali itafute na isomeshe hao vijana ili tuweze kufaidika na hicho kitu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni la umuhimu sana katika uchumi wetu wa Tanzania ili uweze kukua tumeanzisha hii *standard gauge* reli na imeanza Dar es Salaam tumekusudia inakwenda mpaka kwenye mipaka yetu, lengo letu tuitumie vizuri bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, hoja yangu inaanza kujikita kutokana na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam na hili amelieza Mheshimiwa Rais na hoja yangu pia inajikita katika utoaji au upatikana wa fedha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, muda wangu umeishia hapo na nashukuru kupata nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, huyu ni mghani na mwimbaji wa nyimbo za taarabu, mtaalam sana katika eneo hilo. Ndiyo maana mwanzo nikasema mtamfahamu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Elibariki tafadhali chukua nafasi na Mheshimiwa Ndaisaba George ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na kimsingi naomba ninukuu maneno yafuatayo yaliyosemwa na Mheshimiwa Rais wakati analihutubia Bunge lako Tukufu. Alisema: "Nakwenda kuchangia kwenye maeneo mawili kwa kifupi sana. Nitumie fursa hii kuikaribisha sekta binafsi kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza bidhaa za mifugo, nyama, ngozi, maziwa, kwato na kadhalika. Katika hilo tunaahidi kutoa vivutio maalum kwa watakaowekeza katika viwanda hivyo ambavyo vitasaidia kuinua vipato vya wafugaji wetu na pia kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania. Hapa nataka niweke bayana kuwa watendaji watakaokwamisha ujenzi wa viwanda tutawashughulikia". Haya ni maneno ya Mheshimiwa Rais aliyatoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nataka nilipe taarifa Bunge lako Tukufu, *global practice* na najua hii ni *theory* kwa *international trade* mahali popote duniani, Tanzania, Uganda, Kenya, Ethiopia, Somalia na ukisoma katika *statistics* za dunia Tanzania tumetajwa kuwa nchi namba mbili kwa wingi wa mifugo barani Afrika. Katika hili namuomba sana Waziri wa Viwanda atulie anisikilize lakini pia namuomba Waziri wa Uwekezaji atulie na kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, nataka nilipe Bunge lako Tukufu hotuba ya Rais iliyokuwa imejikita katika kulisaidia Taifa kupiga hatua katika masuala mazima ya viwanda, nimeamua kuchagua eneo dogo na kulifanyia utafiti eneo la mifugo. Angalia hiki kinachofanyika katika nchi yetu ya Tanzania ili kama sisi Bunge tuweze kutoa mchango wa kulisaidia Taifa na kuwasaidia wakulima na wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, nakupa taarifa wewe na Bunge lako Tukufu gharama za uwekezaji na *export* ya nyama ambayo imeshasindikwa katika Taifa la Tanzania kwa kiwanda ambacho mtu amewekeza na ameajiri watu, kwa mfano, kiwanda cha Kenya, kilichowekeza na kuwa na uwezo wa kuzalisha kwa mfano nimechukulia mifugo, ng'ombe 1,000 kwa siku, Ethiopia nako ng'ombe 1,000 kwa siku Kenya na Uganda, angalia gharama hizi uone namna gani *we are the witch of our own development*. Nataka nikuambie wewe na Bunge lako Tukufu mipango ya Serikali na nia ya Rais najua asilimia mia moja ni nia thabiti ya kuhakikisha Taifa linapiga hatua lakini bado hatujafanya *harmonization* ya sheria, *regulation* zinakwamisha kupiga hatua kwa sekta nzima ya viwanda katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakupa mfano, kiwanda kinachochinja ng'ombe 1,000 kwa siku Tanzania kikafanya uzalishaji wa ng'ombe 1,000 kwa kipindi cha mwaka mzima Kenya ili uweze kuzalisha ng'ombe 1,000 kwa mwaka mzima, gharama unazozilipa zile za kawaida tu achana na mambo ya *tax*, kuna kuja kulipa *cooperate tax, PAYE* na mambo mengine kwa Kenya inagharimu 1,900,000 kiwanda kinapata kama tozo tozo kutoka Serikalini. Ethiopia kiwanda kinachozalisha nyama ya ng'ombe 1,000 kwa siku, kwa mwezi, kwa mwaka wanalipa 1,008,000.24. Uganda wanalipa 1,900,000. Njoo kwa Tanzania na hii nataka nikuambie na Waziri wetu Mkuu yupo hapa *state intervention* katika kulinda viwanda vinavyowekezwa na Watanzania au *investors* wanaotoka nje imekuwa changamoto kubwa kwa Taifa letu. Ndiyo maana tunajenga viwanda vinakaa mwaka mmoja vimekufa, *state intervention*.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania kuna bodi na matitiri mengi naomba niyasome uone picha na ninyi Mawaziri mliopo hapa mkasaidie kufikisha *vision* ya Mheshimiwa Rais katika sekta ya viwanda. Kwa Tanzania kuna kitu kinaitwa *livestock and fisheries,* ukizalisha nyama kila kilo wanaku-charge shilingi 150 wanasema gharama zao.

Mheshimiwa Spika, cha pili, kuna kitu kinaitwa Bodi ya Nyama, Mawaziri nyie mpo hapa kama nasema uwongo *prove me wrong,* nimefanya utafiti. Kuna kitu kinaitwa Bodi ya Nyama *they take one percent* ya *FoB* kwenye *production* ambayo imezalishwa na kiwanda. Kuna kitu kinaitwa *Chamber of Commerce* wanachukua shilingi 55,000 kila *certificate per consignment* ambayo inakuwa *exported*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukifanya *calculation* mwekezaji atakayekwenda kuwekeza kwenye kiwanda cha kuzalisha nyama kwa mwaka mmoja kwa Tanzania nje ya *cooperate tax* na mambo mengine analipa fedha zisizopungua 860,000,000 wakati Kenya mtu analipa 1,000,000 peke yake. *We cannot survival,* hatuwezi ku-*survival* Mawaziri wangu na ndiyo maana viwanda vingi vinafunguliwa tunapiga makofi tunafungua viwanda haviwezi kukabiliana na ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanafanya *state intervention* na maana ya *state intervention* ni kwamba wawekezaji wanapoingia na Rais hapa nimeisema *vision* ya Rais wa Nchi, *vision* ya Rais wa nchi anasema tutatoa *some sort of incentive* katika viwanda, lakini wito wangu ninaotoa kwa Serikali yangu sikivu, ndiyo maana mnalalamika hapa, amesema kaka yangu pale, mbuzi wanakwenda kuuzwa Kenya, kiwanda wanawezaje ku-*compete* na Wakenya, Mkenya mimi juzi nilikuwa Dubai niliamua tu kufanya *survey,*nimekwenda nyama zote Dubai zinaandikwa *imported from* Kenya wakati Kenya hawana mbuzi. Afrika nchi zenye mbuzi hata Ethiopia tunawasifu, lakini hawana mbuzi, Ethiopia wanakondoo, mbuzi wanatoka Tanzania na kiasi kidogo Somalia.

Mheshimiwa Spika, ninachokwambia nenda kwenye masoko ya nje,kama utakuta kuna nyama imeandikwa imetengenezwa kutoka Tanzania, hakuna nahii nawaambia Mawaziri wa Mifugo, wasisubiri Rais Magufuli aje atoe matamko wachukue hatua. Yaani *if I was the Minister, today* ingetoa *declaration* ya kuhakikisha tozo zote ya ovyo zinazokwamisha viwanda vya nchi hii na kufanya Watanzania wanakosa ajira, ni bora utumbuliwe umefanya maamuzi kwa maslahi ya Taifa. Wafanye kazi Mawaziri wangu, wasiogope Rais yupo nyumayao. Mheshimiwa Mwambe you are Minister kaka yangu tunakuamini, bado kijana mdogo tunajua uwezo wako, shirikiana na Wizara ya Mifugo saidieni Taifa hili kwa mustakabali wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, la pili, Rais jana alizungumza, nilisikiliza hotuba yake na hiyo pia iko katika *package*ya hotuba aliyotoa hapa Bungeni, suala la uwekezaji tuna changamoto kubwa sana, naomba nikwambie, kazi inayofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu hakika tunaweza tusiitambue kwa sababu kuna mambo mengine tunaweza tusiyaone Waziri Mkuu na Ofisi yake wanafanya kazi nzito sana katika kusaidia uwekezaji kwenye Taifa hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilipe Bunge lako Tukufu taarifa, Rais jana alipokuwa anatoa takwimu watu wanakwenda kwenye benki wanakopa hela kubwa sana za kuwekeza, wanakimbilia mahakamani. Natoa mfano mdogo sanasana, nenda kachukue takwimu za iliyokuwa *Bank* M *take statistics*angalia *list* ya watu waliokwenda kuchota bilioni za shilingi za Watanzania mle halafu uwekezaji fedha zimetoroshwa sijui Canada, sijui Kenya na mpaka leo ninavyokwambia *its true* Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya kazi kubwa sana angalau kuna bilioni 200 zimeokolewa kupitia *Bank* ya Azania.

Mheshimiwa Spika, hili nalisema kwa uchungu kwa sababu hapa Bungeni tunayo Kamati inayoshughulikia Uwekezaji na Mitaji, sina maana waanze kufukua makaburi kujua nani kakopa, lakini ukiangalia kwenye *list* ya waliokopa, mbaya zaidi hukuti mtu wa ngozi ya namna yangu,*I am very*

*sorry to say this,* tunaweza tukapigiana kelele na Wabunge hapa vimikopo tunachukua vidogo vidogo kwenye taasisi za fedha, nataka niseme *with confidence* na *with evidence,*Taifa hili bado linapigwa sana. Wizi wa rasilimali za nchi bado haujakoma kwenye nchi hii, lazima kama Bunge tudhamirie kwa dhati kusaidia *vision* ya nchi, Rais atiwe moyo na Bunge sisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Kingu. Huyo ni Mbunge wa Singida Magharibi kwa mchango wako mzuri sana na hasa kuhusu sekta ya mifugo na hiyo nyingine, ni kweli kabisa kwenye mifugo kuna jambo la kufanya.

Mheshimiwa Ndaisaba George, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Joseph Mkundi.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:**Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami nianze kuwashukuru wananchi waJimbo la Ngara kwa kunichagua kwa kishindo kikubwa na siku ya leo nipo hapa Bungeni kama Mbunge miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Mbili. Vilevile naomba nishukuru Chama changu Cha Mapinduzikwa kuniteua, bila Chama Cha Mapinduzi kuniteua leo hii nisingekuwepo hapa.

Nimesoma sana kwa umakini mkubwa hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukiondoa vitabu vya dini kwa maana ya Biblia, hii hotuba ya Mheshimiwa Rais ni Biblia yangu ya pili. Ukiangalia namna hotuba hii ilivyopangiliwa maudhui yaliyomo utagundua kabisa ndiyo maana Taifa letu linasonga mbele kwa sababu Jemedari wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yuko vizuri na mipango ipo vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya Rais kwenye maeneo matatu: Eneo la kwanza ni kuwezesha wananchi kiuchumi; eneo la pili, ni ufugaji; na eneo la tatu, ni upande wa sekta za maji, umeme pamoja na barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na sehemu ya kwanza ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa11 imeelezea kwamba kuna mifuko ya kukopesha wananchi zaidi ya 18 na mifuko hiyo inaonekana haileti tija kwa sababu ya gharama za kuendesha mifuko hiyo, suala la uratibu, lakini ukiangalia na namna ya kupima matokeo inaleta changamoto kunapokuwepo na mifuko mingi.

Mheshimiwa Spika, ukisoma hotuba hiyo ukurasa huo wa11 utaona kuna ombi ambalo linamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kuangalia uwezekano wa kuunganisha mifuko hii ili iweze kuleta tija kwa Watanzania. Mimi mwenyewe nilisikia baadhi ya mifuko kwa mara ya kwanza alipokuwa anaisoma Mheshimiwa Rais. Nataka nikueleze Watanzania hawajui hii mifuko tena ukiangalia, Mheshimiwa Rais amesema kwenye hotuba yake hapa kwamba mikopo hii ni ile isiyokuwa na riba na ile yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, hata sisi Wabunge tungependa kwenda kukopa kwenye mifuko hii tukaachana na kukopa hadi kwenye *gratuity* za kwetu, naomba niiombe Serikali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu iweke utaratibu mzuri kwanza wa utoaji taarifa kwa Watanzania juu yahii mifuko. Vile vile iweke utaratibu mzuri hii mifuko iweze kusaidia wananchi na wananchi wote nchi nzima waweze kupata taarifa sahihi za mifuko hii na utaratibu wa kuweza kupata fedha kutoka kwenye mifuko hii ya kuwezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye upande wa ufugaji na hapa najikita kwenye kitu kinaitwa uhimilishaji, huduma ya uhimilishaji ni huduma inayomfanya mfugaji ahamuwe muda na siku ambapo na siku ambapo mfuko wake utapata mimba, huduma ya uhimilishaji inamwezesha mwananchi kupanga akitaka ng'ombe wake apate mimba kesho yake anamwita Daktari wa Mifugo, anaweka homoni pale anaweka mbegu na ng'ombe wake anapata mimba.

Mheshimiwa Spika, huduma hii inaweza kumfanya mfugaji kuamua idadi ya mifugo anayoitaka kila mwaka na

hivyo tunaweza kuzalisha mifugo mingi na hivyo kukuza uchumi wa kaya moja moja na Taifa kwa ujumla. Naiomba Serikali kwenye eneo hili la uhimilishaji iweze kutenga fedha za kutosha kununua zana za uhimilishaji na kupeleka Madaktari wa Mifugo kwenye chuo kilichopo Arusha kinachofundisha masuala ya uhimilishaji ili kuweza kuleta tija kwenye eneo hili la ufugaji.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye upande wa miundombinu hasa *specifically* kwenye sekta za maji, umeme pamoja na barabara. Jimboni kwangu na maeneo mengine nimesikia Watanzania wengi sana wanalalamika hasa vibarua pamoja na kampuni za Kitanzania zinazofanya kandarasi kama *sub-contractors* na makampuni ya nje. Mimi mwenyewe nimewahi kuwa *sub* kwenye tenda ambayo walipewa Wajerumani. Nataka nieleze wazi kwamba tunapigwa sana kwenye eneo hili, mzungu anasaini mkataba wa dola milioni tatu anakupatia kazi kama *sub* tunafanya kazi yote asilimia 98, inapokuja kwenye malipo kipindi kingine anatuzungusha, kipindi kingine *bargaining power* inakuwa ni ndogo na hata kipindi kingine Watanzania tunadhulumiwa.

Mheshimiwa Spika, achilia mbali sisi ambao ni*Consultants,* njoo upande wa vibarua takribani maeneo mengi sana nchi nzima, wananchi vibarua wanalia. Hapa ninaombi kwa Serikali hasa kwenye idara zote hizi upande wa sekta ya maji, umeme na barabara, naomba Wizara ziweke utaratibu mzuri wa wananchi hawa wa Tanzania kulipwa moja kwa moja kutoka kwenye Wizara husika. Tukifanya hivyo, Watanzania watalipwa moja kwa moja na ile dhuluma ambayo tunadhulumiwa haitakuwepo, ni suala la Serikali kuweka utaratibu mzuri, mkandarasi mkubwa anatoa taarifa kwa aliyetoa kazi za vibarua ama aliyefanya naye *sub-contractors, then* Serikali inalipa moja kwa moja, tunadhulumiwa sana kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa,naomba nieleze changamoto iliyopo kwenye upande wa barabara. Barabara nyingi hasa za mjini ni chafu kwa maana ya kwamba zimejaa mchanga. Utaratibu uliopo wa kusafisha

barabara nimeshindwa kuelewa vizuri, nilikuwa najiuliza, barabara inajengwa nzuri ya lami lakini baada ya muda mfupi unakuta michanga imejaa na kaeneo ka kupita ni kadogo katikati ya barabara na ile michanga inamomonyoa barabara. Naomba Serikali iangalie utaratibu mzuri iuandae wa kusafisha hizo barabara kutoa michanga kwenye lami. Najiuliza jukumu la kusafisha barabara wakipewa TAMISEMI, akapewa Mheshimiwa Jafo, mtaa husika ukahusika kusafisha zile barabara ile michanga itaondoka maeneo yale na barabara zitakuwa safi.

Mheshimiwa Spika, zile barabara za mijini zilizotengenezwa kwa gharama kubwa hata ukipita wewe jaribu kuchungulia kwenye kioo cha gari yako utakuta michanga imesogea kabisa mpaka inataka kumaliza barabara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sanaMheshimiwa Ndaisaba George, Mbunge wa Ngara. Nilishamtaja Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga,*no, no, no* Mheshimiwa Joseph Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbongwe.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:**Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai mpaka leo, lakini nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba zake zote. Ni hotuba ambazo zimeonesha mwelekeo, zimeonesha dira, lakini zinatuonesha dhamira ya msingi aliyonayo Mheshimiwa Rais katika uongozi wakena kulipeleka Taifa hili mahali sahihi, tunakila sababu ya kumpongezea nakumtia moyo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwanza hotuba ya 2015,halafu ukija kusoma hotuba ya mwaka 2020 inaonesha namna gani mambo mengi makubwa yamefanyika kwenye Taifa hili chini ya uongozi wa

Mheshimiwa Rais katika Awamu hii ya Tano. Ukiangalia kwa mfano katika jitihada ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya na kusimamia, mapambano dhidi ya rushwa na ndiyo maana utaona kwa mujibu wa *Transparency International*, katika nchi 35 za Afrika Tanzania imekuwa ya kwanza, lakini hata katika dunia vile vile utaona imekuwa nchi ya 28 katika nchi 136 katika matumizi bora ya rasilimali. Ni jambo jema nakwahiyo tunakila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu mambo mengi yamefanyika kwenye miaka hii mitano.

Mheshimiwa Spika, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais inaonesha dira na kimsingi uelekeo ni mzuri, ndiyo maana ukiona kwa mfano uchumi wetu umekuwa mpaka kufikia kukua kwa asilimia saba ni jambo jema, pato ghafilimeongezeka kutoka trilioni 94 *point* kuelekea 139 ni jambo jema lakini mfumuko wa bei umeshuka, ni jambo jema vile vile katika maendeleo ya kiuchumi. Pia utaona hata mauzo ya nje vile vile yameongezeka kutoka dola bilioni 8.9 mpaka bilioni takribani 9.0,ni jambo jema. Kwa hiyo haishangazi hata mwezi Julai mwaka jana Tanzania ilivyotangwa kuingia sasa kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, jukumu tulilonalo sasa ni kuona namna gani kukua kwa uchumi huu tunakuoanisha na maendeleo ya wananchi wa kawaida ili kukua huku kwa uchumi kuwaguse kwenye maisha ya kawaida ya wananchi wetu. Mwananchi aliyepo pale Ukerewe anayeshughulika na uvuvi aone namna gani katika shughuli zake za kujipatia kipato zinaendana na uhalisia wa kukua kwa uchumi. Kwa mawazo yangu, tunasekta za kijumla na ambazo ni muhimu sana ambazo zinagusa sehemu kubwa ya wananchi wetu ambazo Serikali kama itawekeza kwa kiasi kikubwa zitasaidia sana ku-*link* kukua huku kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati njema sana kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais matarajio yake na ambayo ni matarajio yetu sote kwamba, sasa uchumi wetu uweze kukua kwa asilimia nane, ni jambo jema sana, lakini kama tutakuza sekta na kuzisimamia sekta kwa mfano sekta

ya kilimo, uvuvi, mifugo, lakini hata nishati ni maeneo ambayo yanaweza kusaidia sana ku-*link* kukua huku kwa uchumi na maisha ya kawaida ya mwananchi kuwa bora ili mwananchi huyu wa kawaida aweze ku-*feel* kukua kule kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwenye eneo la kilimo wamezungumza watu wengi hapa, kilimo kinaajiri sehemu kubwa sana wananchi wa Taifa zaidi ya asilimia 70 kwa mujibu wa takwimu, lakini uzalishaji huu wa kilimo bado unachangamoto nyingi, wamesema wachangajiaji waliotangulia kuna matatizo kwenye mbegu, kuna matatizo kwenye utaalam, lakini bado maeneo mengine ambapo uzalishaji umekuwa mkubwa kumekuwa na tatizo kupata masoko hasa masoko ya nje, bado tunachangamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa niishauri Serikali, lakini kwanza niishukuru Serikali angalau kwa taarifa nilizonazo kwa yale makubaliano ambao Serikali ya Tanzania imeingia na Serikali ya Israel ili angalau kila mwaka vijana takribani 100 wawe wanaenda Israel kupata mafunzo ya kilimo, ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, sasa niishauri Serikali, iweze kuwalea vijana hawa,iweze kuwawezesha iliwanapokuwa wamemaliza mafunzo yale wakirudi nchini watusaidie kufikia kwenye malengo yetu ya kufanya mapinduzi ya kilimo kwenye Taifa hili; kwa sababu kama kila mwaka vijana 100 wakienda wakarudi wakawezeshwa, wakaweza kutusaidia kitaalam ni kweli tutafikia mapinduzi haya tunayotarajia kwenye eneo la kilimo.

Mheshimiwa Spika, niipongenze Wizara ya Mambo ya Nje inafanya kazi kubwa sana kutafuta wawekezaji, lakini vile vile katika kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zetu tunazozalisha hapa nchini. Hata hivyo, bado naona kuna ombwe ambapo niishauri Serikali, iweze kuimarisha mahusiano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uwekezaji ili angalau wakulima wetu wanapolima mazao yao, basi yaweze kupata masoko ya uhakika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika,eneo lingine kama nilivyosema ni eneo la uvuvi; kama ilivyokwenye kilimo, uvuvi unaajiri sehemu kubwa sana ya wananchi wa Taifa hili. Kwa mfano kwenye eneo letu la Kanda ya Ziwa, mimi natoka Ukerewe, katika kilometa za mraba 6,400 za Ukerewe, asilimia 90 ni maji, kwa hiyo utaona wananchi wengi wa Ukerewe wanashughulika na uvuvi na hivyo uvuvi unaajiri vijana wengi Ukerewe, Kanda ya Ziwa lakini hata maeneo mengine. Hata hivyo, kama Serikali itawekeza katika uvuvi huu inaweza ikasaidia sana kuboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja. Bahati mbaya sana bado hatujaweza kufanya vizuri kwenye eneo hili la uvuvi.

Mheshimiwa Spika, alisema mchangiaji mmoja asubuhi hapa miaka miwili iliyopita kulikuwa na operesheni zile za kuzuia uvuvi haramu haisaidii sana, wavuvi wetu wadogowadogo hawa ambao tunahangaika kuwatafutia mikopo ili wajiimarishe kiuchumi hata kama kafanya kosa unakwenda unavunja mtumbwi wake, unachoma nyavu zake, haimsaidii sana. Nishauri Serikali iwekeze zaidi kwenye kutoa elimu. Bahati nzuri wananchi wetu ni wasikivu sana; kama wanashirikishwa, wanapata elimu, ni walinzi wazuri sana wa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali, kwenye eneo hili la uvuvi kwa mfano, ili tuweze kuufanya kwa tija na uweze kuwasaidia wananchi wetu kuweza kuimarisha uchumi wao kwa mwananchi mmoja mmoja na katika uchumi jumuishi, basi Serikali iwekeze kwenye kutoa elimu. Vilevile kama ambavyo tumekwishaanza tayari kwa ajili ya kuwasaidia kuwawezesha ili kuimarisha mitaji yao, jambo ambalo naamini litasaidia sana sehemu kubwa ya jamii yetu kuweza kuimarika kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa kumekuwa na changamoto vilevile kwenye sekta hii ya uvuvi; wavuvi wetu wanakabiliana na changamoto nyingi sana lakini ninahisi kunakosa kiunganishi kati ya wavuvi na Serikali; chombo ambacho kinaweza kikawatetea, kikawasemea na wakati mwingine kikashauri Serikali namna gani ya ku-*deal* na

masuala ya uvuvi ili sekta hii ya uvuvi iweze kuwa na manufaa kwenye taifa letu. Kwa hiyo, nishauri Serikali iweze kuliangalia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linaweza kusaidia sana kufanya uchumi wa mwananchi mmoja mmoja uweze kuimarika ni kwenye eneo la nishati. Nishukuru sana, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, mwaka 2015 wakati anahutubia Bunge, katika vijiji 12,000 ni vijiji karibu 2,000 tu ndiyo vilivyokuwa na umeme…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wale vijana uliozungumzia kwamba huwa wanakwenda kupata mafunzo ya kilimo Israel, ni kweli na huwa wanachukuliwa vijana waliomaliza *SUA* au vyuo vingine vya kati vya kilimo. Wanapokwenda kule huwa ni programu ambayo wanaporudi wanarudi na *seed money,* kapesa fulani ka kwenda kuazisha shughuli wao wenyewe na wanachanganyika na vijana kutoka nchi nyingine za Afrika. Kwa hiyo, kama wanarudi na kujifanya sijui hawana mtaji hawana nini, hicho nacho ni kisingizio kingine cha vijana wetu kama kawaida yetu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema wake kuweza kusimama mahali hapa na mimi niwe mmojawapo wa wachangiaji wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 13 Novemba, 2020.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais imegusia vitu vingi sana lakini kipo kitu kimoja ambacho wenzangu hawajakisema sana, mimi naomba niweke wazi. Nchi yetu kweli kila mmoja anatamani kwamba tuwe mabilionea lakini binafsi ninavyoangalia hatuwezi kuwa mabilionea kwa sababu ya tatizo la rushwa Rushwa imezidi, imepanda bei.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 2000 mimi nilikuwa dereva, tulikuwa tunatoa rushwa kwenye mabasi shilingi 2,000, lakini toka mwaka jana mpandishe faini rushwa imepanda sasa hivi kwenye mabasi wanatoa shilingi 10,000 na kuendelea. Nitoe ushauri tu kwa mhusika, kama yupo ama hayupo lakini ananisikia; sioni kama anafanya kazi kumsaidia Rais kwenye upande wa rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kwenye sekta ya afya hapa kuna tatizo kubwa sana kwenye upande wa afya. Mimi nazunguka sana kwenye mikoa hii ya Tanzania, kila ukipata tatizo ukaingia hospitali hizi dawa zinazosemwa tunazitoa bure hazionekani kiukweli. Naweza nikawa mlalamishi sana lakini ukweli uhalisia ndio huo.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kwa ajili ya wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe ambao wengi wao ni kweli ni watu ambao hawajasoma na Wabunge wengi humu tumepigiwa kura na hao watu ambao hawajasoma. Hivyo sasa naishauri Serikali ione jinsi gani hawa wenzetu ambao wameishia darasa la saba, hawana *CV,* tunashirikiana nao vipi ili kuepusha migongano. Maana nikiangalia kwa hali ya kawaida kama vile wasomi wengi siyo waaminifu. Tukiangalia kwenye halmashauri zetu Serikali inapata hasara nyingi sana. Ukiangalia upande wa watu hao wa rushwa hawashughulikii ipasavyo, utakuta tu watu wanauawa kwa kuiba kuku, wizi wa ng'ombe, wameuliwa na watu wasiojulikana, sijaona Mkurugenzi hata mmoja amefungwa kwa ajili ya kuhujumu miradi ya Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongea haya maneno nikiwa na *experience* kubwa sana. Leo ni miezi mitatu sasa mimi nikiwa Mbunge na nimejaribu kufanya operesheni kwenye jimbo

langu nikaona matatizo yanatokea jimboni. Hivyo sasa nitoe wito tu kwa wahusika; kuna Waziri wa TAMISEMI, hata jana nilimsema lakini na leo naomba tu nirudie ili nishereheshe ili aone kabisa kwamba ni jinsi gani Wabunge wengine tunapata hasira.

Mheshimiwa Spika, Rais anataka tusonge mbele lakini huku sisi tukijitahidi kusimamia kama wasimamizi wakuu wa halmashauri mapato yanayotumwa juu na mapato yale ya ndani hayaonekani yanaenda wapi. Nikiangalia Jimbo langu mimi la Mbogwe ni jimbo lililo na rasilimali nyingi sana, ukiangalia mauzo ya Geita, dhahabu inayotoka Mbogwe ni nyingi sana. Kuna mapato yanayoitwa ya *service levy,* halmashauri yangu inabaki kuwa maskini na mimi mpaka sasa hivi najiuliza na mwanasheria wangu wa halmashauri, nimemwambia aangalie kifungu, tufuatilie kabisa mapato yetu ili halmashauri yetu iweze kupiga hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huyo ni Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, mtani wangu. Yeye anatakiwa akimaliza miaka mitano aandikiwe kitabu kwa sababu ni mtu ambaye ameanzia mbali sana kimaisha; ametuambia hapa aliwahi kuendesha mabasi ya abiria hadi Mbunge. Mnaona jinsi nchi hii ilivyo na rasilimali kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maganga, endelea na mchango wako.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nilindie muda wangu usinikate, nina vitu vingi vya kuchangia hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwenye miundombinu, barabara mwanzoni zilikuwa zinashughulikiwa na Madiwani, mmekuja mkafanya mabadiliko mkazipeleka *TARURA* na mimi najitahidi sana kuwasiliana na watu wa *TARURA* naona jinsi gani hakuna kuwa *supported* wala kuambiwa kwamba kuna bajeti ya shilingi ngapi zilizopo kwenye akaunti.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ninavyoongea na wewe hapa ndani ya Bunge lako hili Tukufu barabara zangu zimekatika, Waziri Mkuu ni shahidi, waliwahi mpaka kunidharau sana mimi wakati wa kampeni maana barabara yangu moja ya Budoda ilikuwa haipitiki na mpaka sasa hivi haipitiki, kule kuna wananchi wengi sana na wanajifungua kila siku. Sasa ule mto wakitaka kuvuka waje Masumbwe wanasombwa na vifo vingi vimesababishwa na mto huu. Unaweza ukasema kwamba ni kitu cha kuchekesha lakini ni kweli na uhalisia wa vitu vilivyoko kule Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna barabara zangu za kutoka Mponda, tumepakana na Mheshimiwa Iddi, Mbunge wa Msalala, barabara zile ni mbaya sana. Kila ukiwafuata *TARURA* ni watu ambao hawaeleweki kwamba tunazirekebisha au tunafanya nini. Mwishowe nimekuwa kero kwenda kwenye ofisi za *TARURA* mpaka na mimi naiona hii kazi ya Ubunge ni ngumu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilindie muda wangu, bado naendelea. Kwa maana hiyo naliomba Bunge Tukufu hizi barabara bora zirudi tu halmashauri ili hawa Madiwani na wao wawe wanawajibika na kutoa *go ahead* kwamba turekebishe hapa na hapo, kuliko kumleta mtu mwenye *degree, engineer* ambaye amesoma *physically,* hajaona *practical* na hataki kujifunza na wala hayuko tayari kuwasikiliza wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu, alikuja akaniombea kura na nimeshinda kwa asilimia…

**SPIKA:** Katibu, muongezee dakika tatu. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Waziri Mkuu alikuja kuniombea kura na nimeshinda kwa asilimia mia moja. Japokuwa siku ile ukiwa kwenye mkutano wangu unaninadi baada ya kusoma yale maelezo nilipingana na wewe maana mimi huwa ninasali, huwa

ninajitahidi sana kutembelea kwenye neno la Mungu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nachotaka niliombe Bunge Tukufu, kwanza sisi Wabunge tuwe na hofu ya Mungu, unajua haya mamlaka tumeyapata kwa nguvu za Mungu. Wapo viongozi kabisa hata hii hotuba wanaipongeza tu na mimi nimekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa Rais wetu, watu wale wa karibu yake, ukitaka kumjua mtu angalia kwenye mawasiliano, anajua yule Waziri wa Mawasiliano ni nini huwa wanakifanya ili kumjua mtu mnafiki na mkweli. Wapo watu wakisimama majukwaani ni wazuri, wanampongeza kwa asilimia mia moja, huyu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kafanya mambo makubwa, moja, mbili, tatu, hivi na hivi Dkt. John Pombe Magufuli ni mtu mzuri lakini ukimfuatilia yule mtu unamkuta yuko kwenye *connection* za wizi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, watu wale kama wananifahamu wakitaka labda wanipeleke mahakamani mimi ushahidi ninao. Hata kama nikipoteza mwingine, Waziri wa Mawasiliano ni rafiki yangu, tutachomoa kwenye simu zao tutaangalia huwa wanaongea nini pale wanapoachana na Rais. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine naomba kwenye halmashauri zetu hizi tutengeneze sheria za kuwa-*limit* Madiwani. Kuna Madiwani ni wazee, ni baba zetu na sisi Wabunge tulioingia awamu hii ni wadogo, wao ni wazoefu wengine wana miaka 20 wamo kwenye *game.* Walishazoea kuiba, hawapo kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

Sasa sisi tulioisoma hii hotuba ya Mheshimiwa Rais, tunapokwenda na misimamo hii hii tunaonekana wabaya. Naliomba Bunge hili tukufu tutunge sheria ili tuweze kuwa-*monitor* wale Madiwani.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna kauli moja wanaitumia, nilindie muda wangu, bado kama dakika nne. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, namlinda Mheshimiwa, naomba tumpe nafasi. *(Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, kuna msemo mmoja hata hapa Bungeni nimeusikia, ukitaka kufuatilia ile miradi iliyotekelezwa na Chama cha Mapinduzi 2015 mpaka 2020 ukitaka kufuatilia kwamba hili jengo limejengwa kwa bei gani wanakwambia wewe usifukue makaburi, subiria zile fedha zinazokuja ili uanze kufuatilia hapo. Mimi naliomba hili Bunge pamoja na wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, najua kuna *CAG* pamoja na watu wengine na Mawaziri wahusika; tufukue makaburi *term* hii ili tuonekane tunamsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi namshukuru sana baba yangu mzazi ambaye anaishi kijijini, japokuwa napenda sana aishi na mimi lakini kwa uwezo wa Mungu na mapenzi ya watu wa Mbogwe niko hapa. Nakuomba tu endelea kuniongezea muda hivyo ili niweze kulisaidia taifa langu, hasa watu ambao hawajasoma wakapata vyeti lakini wana akili timamu na wana *experience* na wana uchungu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, namuomba Mheshimiwa Rais apime hata halmashauri 50 tu akiweka hata Wagogo na Wazaramo, sisi Wasukuma akituweka watasema kwamba kwa kuwa ni wa kwetu, aweke tu ninyi watani zetu ambao ni wa darasa la saba waende wakawe Wakurugenzi kwenye halmashauri muone zitakavyopanda hizo halmashauri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyo ni Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe. Ninyi mnacheka tu, Mheshimiwa Musukuma ametoka au bado yupo?

**WABUNGE FULANI:** Ametoka.

**SPIKA:** Ametoka kidogo eeh.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Alisema asubuhi kwamba mabilionea nchi hii ni watu wenye elimu ndogo, kwamba wenye ma-*degree* bilioni zenu ziko wapi? *(Kicheko)*

Sasa niwahakikishie Mheshimiwa Nicodemas Maganga ni mmoja wa watu wenye uchumi mzuri nchi hii. Kwa hiyo, mumcheke lakini muwe mnajua kwamba yuko vizuri. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Simon Songe, kama yupo na atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Pia nimshukuru Mungu sana kwa nafasi hii aliyotupatia ya kuwa mahali hapa leo. Kipekee nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi pamoja na wananchi wa Jimbo letu la Busega kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao mahali hapa.

Mheshimiwa Spika, 2015 nilibahatika kufuatilia hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015. Aliyoyasema nilianza kufikiri kwamba yanaenda kuwezekana vipi, lakini nirudishe shukrani nyingi sana kwa mapinduzi makubwa ya maendeleo aliyotupatia Mheshimiwa Rais kwa kipindi hiki cha miaka mitano iliyopita. Ni Imani yangu kubwa kwamba katika hii miaka mitano kupitia hotuba yake ya tarehe 13 Novemba, 2020 ambayo ilitoa mwelekeo wa nchi yetu yapo maeneo machache naomba nami nichangie.

Mheshimiwa Spika, kuna suala toka asubuhi linaendelea kujadiliwa; habari ya *TARURA*. *TARURA* ni pasua kichwa, *TARURA* ni shida mpaka sasa barabara nyingi vijijini zimekatika. Pia kutokuwepo kwa barabara hizi za vijijini kumesababisha sehemu ya uchumi wa wananchi wetu kushuka kwa sababu hawawezi sasa kupeleka hata mazao

yao kwenda kutafuta sehemu ambako kuna masoko, madalali wamekuwa wengi wa bei ya chini kwa sababu ya shida ya barabara ambazo ziko kwenye vijiji ambavyo sisi tunatoka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukiangalia kuna wakati hata hili zao la pamba kwetu kule Usukumani ambapo wananchi wengi wanalima, inafikia sehemu barabara ni ya shida watu wa pikipiki wanakwenda kununua pamba kwa bei ya chini sana, muda mwingine hata nusu ya bei ambayo ni halisia kwa sababu ya kutokuwepo barabara sehemu husika. Tunapotaka sasa kuendeleza uchumi wa wananchi wetu mmoja mmoja lazima tuwatengenezee mazingira mazuri ili wananchi hawa sasa waweze kusafirisha mazao yao ya biashara kwenda sehemu nyingine kwa ajili ya kupata bei iliyo salama.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nichangie kidogo eneo la kilimo. Mimi ni muumini sana wa uwekezaji katika sekta ambazo ni *productive* kwa nchi yetu. Tunapokuwa tunazungumza habari ya ajira milioni nane, ni lazima tufikiri kuelekeza baadhi ya ajira katika sehemu ambazo ni *productive* kwa nchi yetu ikiwemo na kilimo.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye halmashauri zetu, halmashauri zilizo nyingi zina shida ya watumishi, hasa Maafisa Ugani. Wananchi wetu wengi hawapati fursa ya kufundishwa na hawa Maafisa Ugani kwa sababu hawapo kila sehemu ni shida. Hii ni sekta ambayo tungeweza kuielekezea watumishi wengi wangeweza kuwasaidia wananchi wetu ambao wanalima kwa kutumia akili zao zilezile ambazo Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe alikuwa anajaribu kugusia.

Kwa hiyo, mimi niseme na niombe, tunapokuwa tunaangalia suala la ajira, lazima pia tuangalie eneo hili ili tuweze kuajiri watu wengi waende wakawasaidie wananchi wetu katika suala zima la kilimo na kilimo kiwe chenye tija na tutakapopata malighafi yetu basi itatumika kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni viwanda. Eneo hili tukitaka tufanye vizuri ni lazima tuhakikishe kwamba tunapata viwanda vyetu vya ndani ambavyo vinatengeneza bidhaa mpaka mwisho. Kama ni pamba basi tutengeneze bidhaa inayotokana na pamba mpaka mwisho tupate nguo ili tuweze ku-*export* nguo kwenda nje ya nchi, zao ambalo tayari limekamilika kwa kutumia bidhaa zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuongelea habari ya uvuvi, Mbunge wa Ukerewe amezungumza kidogo. Eneo hili bado lina shida, tozo ni nyingi sana kwa wananchi wetu ambao wanashughulika katika suala zima la uvuvi. Tozo ni nyingi, kuna leseni ya mtumbwi, *TASAC* Sh.70,000 wananchi wetu wanalipa lakini pia kuna leseni za halmashauri, kuna leseni ya mtumbwi na kuna shilingi 20,000 leseni ya mvuvi mmoja mmoja. Haya maeneo wananchi wetu wanayalalamikia sana kwa sababu tozo zimekuwa nyingi na wanashindwa kuzimudu kutokana na hali ya uchumi ambao wanao. Kwa hiyo, niombe Wizara husika waje na mpango kuona namna ya kupunguza baadhi ya tozo kwa hawa watu wetu ambao ni wavuvi ili waweze kunufaika na kazi ya uvuvi ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sekta ya afya. Eneo hili asubuhi limechangiwa katika hoja mbalimbali kupitia maswali. Huduma ya bila malipo kwa akina mama wajawazito, watoto na hata wazee; ni kweli kuna baadhi ya hospitali zinatoa lakini kuna shida kubwa sana ya upatikanaji wa dawa katika sehemu ambazo wananchi hawa wanatibiwa. Ama dawa *MSD* hazipatikani lakini hata kama zikipatikana basi mpango mzima wa kando unafanyika na kunakuwa na *shortage* kubwa sana ya dawa.

Mheshimiwa Spika, tumeona hata Mheshimiwa Waziri wa Afya amejaribu kwenda na hoja ya kutaka kuangalia *equation* tu iliyopo kati ya uwepo wa panadol na mwananchi kukosa dawa na akasema hii siyo *simultaneous.* Mimi nimpongeze kwa namna ya pekee sana kwa jinsi ambavyo ameamua kuja kwa kasi na kuhakikisha kwamba sehemu zetu

dawa zinaendelea kuwepo na wananchi wetu wanapata dawa.

Mheshimiwa Spika, niombe sasa, *MSD* bado kuna shida. Tunaweza kwenda na *order* kubwa ya dawa na fedha ambazo tayari ziko *MSD* lakini *MSD* inakosa dawa. Niombe sasa Serikali kupitia Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba tunaimarisha *MSD* ili iweze kuwa na sehemu kubwa ya kupata dawa ili wananchi wetu sasa waweze kupata dawa katika sehemu ambazo wanakuwepo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka kuchangia ni maliasili na utalii. Kuna shida kubwa sana ya tembo kusumbua na kuharibu mazao ya wananchi wetu. Nizungumzie kwa mfano kule kwangu Jimboni Busega kuna Kata za Lamadi, Mkula kwa maana ya Kijereshi, kuna shida kubwa ya tembo. Katika mwaka uliopita 2020, zaidi ya wananchi wanne wameuawa na tembo kwa sababu ya kukaa katika kata hizo ambazo nimeweza kuzitaja.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kubwa sana ya kuimarisha ulinzi wa wanyamapori kupitia maaskari wetu. Ninajua Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofika pale kwenye jimbo langu aliahidi kutupatia askari 26 ili waongeze kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na hii itatusaidia sana wananchi wetu kufanya kazi zao wakiwa na amani. Sasa kwa sababu mazao yao yanaharibiwa tunawapa tena wakati mgumu wa kupata mazao ili waweze kunufaika na mazao yao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, huyo ni Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Busega.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya hali ya muda tuishie hapo. Niwashukuru sana kwa *day one,* tumekwenda vizuri, tuendelee hivyohivyo kesho. Wale ambao hamjazipitia vizuri hotuba za Mheshimiwa Rais ziko kwenye *tablets* zenu mkazipitie na kesho atakuwepo hapa Naibu

Spika, wale Wabunge ambao hawajapata nafasi ya kuongea leo na ni wengi natumaini kesho mtapata nafasi. Kipekee Wabunge wanawake sasa ni vizuri mkasikika.

Kama nilivyosema kabla ukichagua kunyamaza hapa umejimaliza mwenyewe. Wananchi wako wasipokusikia, utakuwa umejimaliza mwenyewe. Kwa hiyo, fursa ni yako kusuka au kunyoa lakini naamini kabisa mtaamua kusuka.

Kwa jinsi hiyo, kwa kuwa muda wetu sasa umeisha, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.43 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 3 Februari, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*